# UKUAJI WA MUUNDO NA MAWAZO KATIKA TAMTHILIA ZA TIMOTHYAREGE MTAZAMO WA UMUUNDO

NDEGE MAGATI CHARLES

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA

MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI,

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

OKTOBA 2013

University of NAIROBI Library
0389665 1

## IKIRARI

**Mtahiniwa**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

**Sahihi:** ..........CM. Ndege.......... **Tarehe**....7-11-13....

Ndege M.Charles

(Mtahiniwa)

**Wasimamizi**

Tasinifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama washauri na wasimamizi walioteuliwa na chuo.

**Sahihi:** ................................ **Tarehe**...07/Nov/2013...

Dkt.Zaja Omboga

**Sahihi:** ................................ **Tarehe**...7/11/2013...

Dkt.Amiri Swaleh

(Msimamizi)

## TABARUKU

Safari hii imekuwa ya pandashuka nyingi kuhakikisha tumefikia mwisho wake. Kwanza kabisa namtabarukia mke wangu mpendwa, Magoma Esther Masare kwa uelewa na kujinyima kwake ili niweze kukamilisha masomo yangu. Umekuwa msaidizi kwa kujitolea kugharamia masomo yangu na wanangu. Nakushukuru kwa kujali maslahi na mahitaji yangu. Uvumilivu uliouonyesha katika safari hii yote, sina wa kukufananisha ila kukuombea Mola akubariki.

Sitaweza kuwasahau wanangu wapendwa Oongo, Sandim na Mariera kwa mchango wao katika masomo yangu kwa kustahimili machungu ya kutokuwa karibu nao kwa muda wa miaka miwili ambapo huduma zangu kwao zilihitajika zaidi.

Sitakosa kuwatabarukia kakangu Michira, Nyambane na rafiki yangu msomi Ongarora kwa mchango wao katika masomo yangu. Maulana awapige muhuri wa baraka.

# SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote ambao walichangia ufanisi wa utafiti huu kwa njia moja au nyingine. Waliosema mtu ni watu hawakukosea. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya na uwezo wa kutimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili. Ninawashukuru wazazi wangu Joseph Ndege na Rael Nyamisa walionizaa na kunionyesha milango ya shule. Shukrani za dhati na za kipekee kwa wasomi wenzangu David Nyakawa na mwalimu Karani. Ninatoa shukrani kwa wasimamizi wangu Dkt.Zaja Omboga na Dkt.Amiri Swaleh kwa ushauri wao wa kitaaluma ili kuhakikisha kuwa kazi hii imetimia. Sina cha kuwapa ila kuwaombea Mungu awazidishe kiafya na kimaarifa. Mungu awabariki sana.

Shukrani ziwaendee wahadhiri wote wa idara ya isimu na lugha kwa ushauri walionipa na uliochangia katika kuyafikia malengo yangu. Shukrani maalum kwa wafuatao: Prof.J. Habwe Dkt.Iribe Mwangi, Dkt Kinene, Dkt.Evans Mbuthia, Dkt.Jefwa Mweri, Bw. Mungania na wengineo  ambao siwezi kuwataja. Mungu na awabariki sana. Shukrani zingine ziwaendee wanafunzi wenzangu tuliokuwa tukisafiri katika chombo kimoja na kuhakikisha kuwa tumefika mwisho licha ya kuwa na vizingiti njiani.

Hatimaye ningependa kumshukuru Rachel Maina kwa kunipigia taipu na kuhakikisha kuwa kazi hii imekamilika kwa wakati unaofaa. Mungu awabariki nyote.

# MUHTASARI


Utafiti huu umechunguza ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za Timothy Arege. Tamthilia zilizoteuliwa kuhakikiwa ni tatu. Nazo ni: *Chamchela* (2007), *Kijiba cha Moyo*(2009) na *Mstahiki Meya* (2011)

Sura ya kwanza ni utangulizi, tatizo la utafiti, madhumni ya utafiti, nadharia tete, upeo na mipaka na msingi wa nadharia. Pia, tumejumuhisha yaliyoandikwa kuhusu mada, na mbinu za utafiti zizotumika katika kazi hii.

Sura ya pili imeshughulikia msuko kama mojawapo wa vipengele vya muundo na mchango wake katika tamthilia za Arege. Tumetanguliza kwa kuangazia dhana ya msuko, kanuni za ploti pamoja na mchango wao katika kuendeleza ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za Arege.

Sura ya tatu imeangazia mchango wa wahusika katika kuendeleza dhamira na maudhui. Tumeshughulikia majukumu yao na mchango wao katika kuibua maudhui na dhamira.

Sura ya nne nayo imeshughulikia mchango wa matumizi ya lugha katika kudhihirisha ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za Arege. Tumeshughulikia tamathali za lugha kama vile tashihisi, balagha, uzungumzinafsia, kuchanganya ndimi, tashbihi, dhihaka, methali, mdokezo, sitiari na kinaya.

Sura ya tano inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

## YALIYOMO

Ikirari ........ ii

Tabaruku ........ iii

Shukrani ........ iv

Muhtasari ........ v

Yaliyomo ........ vi

**SURA YA KWANZA**

**UTANGULIZI** ........ 1

1.1 Tatizo La Utafiti ........ 6

1.2 Sababu za Kuchagua Somo Hili ........ 7

1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 8

1.4 Nadharia Tete ........ 9

1.5 Upeo na Mipaka ........ 9

1.6 Msingi wa Nadharia ........ 10

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili ........ 13

1.8 Mbinu za Utafiti ........ 16

**SURA YA PILI**

**MSUKO NA MCHANGO WAKE KATIKA TAMTHILIA ZA AREGE**

2.1 Utangulizi ........ 18

2.2 Mchango wa Msuko Katika *Chamchela* ........ 20

2.2.1 Usanifu na Uibukaji wa Muundo na Mawazo ya *Chamchela* ........ 27

2.2.2 Msuko Na Mchango Wake Katika Kijiba Cha Moyo ........ 28

2.2.3 Tathmini ya ploti ........ 36

2.2.4 Mchango Wa Msuko Katika *Mstahiki Meya* ........ 38

2.2.5 Tathmini Ya Ploti ........ 46

2.3 Hitimisho ........ 47

SURA YA TATU

MCHANGO WA WAHUSIKA KATIKA KUENDELEZA DHAMIRA NA MAUDHUI

3.1 Utangulizi ........ 49

3.2 Mchango Wa Wahusika Katika Kuendeleza Dhamira Na Maudhui Katika Chamchela ........ 51

3.3 Mchango Wa Wahusika Katika Kuendeleza Dhamira Na Maudhui Katika *Kijiba Cha Moyo* ........ 55

3.3.1 Wahusika na Nafasi Zao ........ 55

3.4 Mchango wa Wahusika katika Kuendeleza Dhamira Na Maudhui Katika *Mstahiki Meya* ........ 61

3.5 Hitimisho ........ 70

SURA YA NNE

MCHANGO WA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA KUDHIHIRISHA UKUAJI WA MUUNDO NA MAWAZO KATIKA TAMTHILIA ZA AREGE

4.1 Utangulizi ........ 71

4.2 Tashhisi/uhuishi/uhaishaji ........ 72

4.2.1 Matumizi ya balagha ........ 75

4.2.2 Uzungumzinafsia ........ 77

4.2.3 Kuchanganya ndimi ........ 78

4.2.4 Tashbihi ........ 82

4.2.5 Methali ........ 84

4.2.6 Dhihaka ........ 87

4.2.7 Mdokezo ........ 88

4.2.8 Sitiari ........ 90

4.3 Kinaya ........ 91

4.4 Hitimisho ........ 92

## SURA YA TANO

## MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

5.1 Utangulizi ........ 93

5.2 Matatizo Wakati wa Utafiti ........ 94

5.3 Mapendekezo Zaidi ya Utafiti ........ 95

**MAREJELEO ........ 96**

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

Mada ya kukua kwa muundo na mawazo daima imekuwa muhimu katika uhakiki. Hii ni kwa sababu uhai wa fasihi, hutegemea kukua kwake. Kwa ujumla, kukua ni kubadilika kutoka hali moja hadi hali nyingine ya ukomavu. Katika fasihi, ukuaji sio jambo la kimaumbile kama ilivyo kwa viumbe hai. Hili ni jambo linalotokana na juhudi za wasanii wanapotunga kazi zao. Kwa vile fasihi ni sanaa inayoumbwa kwa kutumia lugha teule, jukumu la msanii yeyote ni kuyapekua maneno, maumbo, miundo na taswira zitakazooana vizuri na dhamira. Mwandishi anayekua ni yule ambaye kila kazi anayoitunga inakuwa bora zaidi kuliko ile anayoitunga mwanzoni. Hata hivyo, suala la kukua kwa mwandishi ni tata lakini tunaweza kusema kuwa kukua kwa mwandishi kunadhihirika katika kukua kwa sanaa. S.A Mohamed anafafanua zaidi suala la kukua kwa mwandishi kuwa ni yule ambaye harudii maudhui au mawazo yale yale lakini hupiga hatua ama huja na mawazo au maudhui mapya, au kuyapanua mawazo au maudhui fulani au mwandishi anayeweza kutia upya katika hata lile jambo lililozoewa na hadhira.

Sio katika kipengele cha mawazo tu ambapo mwandishi anapaswa kuonyesha upya bali pia kama anavyotia mkazo Mohamed, katika muundo na fani ya kazi kwa jumla. Suala la kukua kwa mwandishi haliwezi kutenganishwa na ukuaji au maendeleo ya fasihi hasa utanzu wa tamthilia. Kwa hivyo mwandishi ni kama nyenzo muhimu sana katika ukuaji au kuendelea kwa fasihi. Hivyo ndivyo amaanishapo Mukarovisky anaponukuliwa akisema kuwa, "Chochote kinachotukia katika fasihi, hutukia kupitia kwa upatanishaji wa mwandishi"

Kutokana na hayo yote, tunatarajia kwamba, tutakapokuwa tukijadili suala la kukua kwa Timothy Arege, tutakuwa tukijadili pia kukua kwa tamthilia ya Kiswahili katika kipindi kinachohusika (2007-2011)

Jambo hili halitakuwa kiini cha utafiti wetu lakini pia halitaepukika katika kiwango hiki. Kwa sababu hii tutakuwa tukiligusia mara kwa mara. Kazi tatu za Arege hazikutofautiana sana kiwakati. Uhakiki wa kazi hizi, hauwezi kuepuka suala la ulinganishaji na ulinganuaji wa kimuundo na kimawazo. Hii ni kwa sababu ulinganishaji utatusaidia kujibu swali hili la ukuaji wa mwandishi. Je, ni mwandishi anayepiga hatua au kutopiga hatua za kukua? Hatutajishughulisha sana na sababu za kukua au kutokua kwa mwandishi. Hata hivyo,kwa kuhitimisha, tutataja baadhi ya sababu za kukua pakiwa na haja.

Fafanuzi mbali mbali zimetolewa kuhusu dhana ya tamthilia. Maelezo kuhusu tamthilia ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu yatatuwezesha kutambua kwa kiasi fulani ukuaji si wa mwandishi tu bali wa fasihi kwa ujumla wake.

Pamoja na utangulizi wa hapo juu tunaweza kutoa fafanuzi mbalimbali kuhusu tamthilia na mabadiliko yake kimuhutasari tangu enzi za akina Aristotle hadi wakati wa Timothy Arege na utunzi wake. Neno "tamthilia" linahusiana moja kwa moja na kitenzi "kumithilisha" ambacho kinamaanisha kufananisha kitu kimoja na kingine. Hivyo basi, tunapofikiria kuhusu dhana ya tamthilia, tunafikiria kufananisha kitu kimoja na kingine. Kifananishwacho ni maisha ya binadamu na yale ya wahusika katika kazi ya sanaa. Tamthilia hivyo basi, imejikita katika mazingira fulani.

Wafula (1999) anaeleza ya kwamba, mtunzi wa tamthilia huyasawiri mawazo au fikira kwa maongezi ya wahusika kwa kuunda migogoro na mijadala baina ya wahusika katika tamthilia. Kulingana naye, mikondo na misisitizo kadha huweza kujitokeza kutokana na orodha ya baadhi ya tamthilia.

Wamitila (2000:217) ameitolea maelezo "tamthilia" kama kazi ya kidrama na ya kimaongezi ambayo huigizwa mbele ya hadhira au kazi iliyoandikwa kusomwa. Kuna sifa kadha wa kadha ambazo hutofautisha utanzu huu na tanzu zingine za fasihi:

i) Kuna matumizi ya mazungumzo kwa upana katika jukwaa. Huu ndio msingi muhimu.
ii) Usimulizi wa tamthilia hutegemea mazungumzo yanayokuwepo baina ya wahusika mbali mbali na pia uzungumzinafsi wa wahusika na maelekezo ya jukwaa (ni)
iii) Mazungumzo ya wahusika huwa ni kielelezi cha dhamira pamoja na ujenzi wa msuko.

Kulingana na Wafula na Njogu (2008) Aristotle alikuwa ni mgiriki aliyeishi katika enzi ya Urasimi wa kigiriki kati ya karne ya pili na nne ambapo Ugriki na Urumi ziliweka misingi ya viwango vya juu vya utunzi wa tamthilia ya kitanzia. Kuhusu tamthilia, Aristotle alitambua vipengele sita vya tamthilia ya kigiriki:

(i) Nyimbo
(ii) Matamshi
(iii) Mtiririko wa vitendo
(iv) Wahusika

(v) Fikra

(vi) Utumiaji wa jukwaa

Aristotle alisisitiza umuhimu wa kukata kauli kama mchezo ni wa kufurahisha au ni wa kuhuzunisha, majonzi ama tanzia. Aliigawa tamthilia katika sehemu tatu:

(a) Utangulizi

(b) Kitendo

(c) Wimbo wa tamati

Huu ndio uliokuwa muundo wa tamthilia ya kigiriki (tanzia) lakini si wanatamthilia wengi wa Kiswahili wanaofuata mtindo huu. Kuhusu matamshi, Arisitotle alisisitiza kuwa mambo katika tamthilia husemwa na kufuatia umbo lenye mizani. Wanapendekeza kuwa kitu muhimu si matamshi bali mazungumzo ya kitamthilia kama njia ya kuisukuma mbele tamthilia. Katika kufanya hivyo, mwandishi anaichezea lugha. Vitushi hupangwa kwa mtiririko. Licha ya hilo, Kitendo cha pili kinazuliwa na cha kwanza. Vitushi vinaingiliana kuunda ploti yenye mzuano na msababishano.

Horace na Aristotle walichangia sana kuhusu utunzi na muundo wa tamthilia. Kuhusu tamthilia ya Kiswahili,Wafula (1999:7) anatueleza kuwa, kutokana na orodha ya baadhi ya tamthilia, mikondo na misisitizo hii inasadifu masuala muhimu ya kihistoria yaliyowahi kutokea katika eneo la Afrika Mashariki na upwa wake.

Longino alikuwa Mgiriki aliyeishi karne ya tatu BK. Yeye alizungumzia fasihi kwa ujumla wake. Alikuwa ndiye mtaalamu wa kwanza kushughulikia fasihi kwa ujumla wake akizingatia athari za kisaikolojia. Alidai kuwa ubora wa kazi yoyote ya kifasihi hutokana na jinsi kazi yenyewe inavyoweza

kumwathiri msomaji kisaikolojia, kumteka hisia hadi ulimwengu mwingine, kujihisi kuwa mgeni kwa sababu ya uteule wa lugha ya mwandishi. Ili aweze kufaulu katika haya:

a) Sharti mwandishi aweze kutumia lugha husishi inayoweza kushirikisha kunga za fasihi kama vile jazanda, methali na tashbihi.
b) Mwandishi aweze kutumia lugha inayofungamana na muktadha.
c) Ujumbe unaozungumziwa uweze kuafikiana na matumizi ya tamathali za usemi

Tamthilia ikiwa mojawapo ya tanzu za fasihi andishi, haina budi kusawiri athari hizo tatu zinazohimili upekee wa fasihi kutoka taaluma nyinginezo. Wataalamu hawa wanapaswa kupongezwa kwani ndio walioweka baadhi ya misingi katika utanzu wa tamthila.

Mada ya kukua kimuundo na kimawazo daima ni muhimu katika uhakiki. Wanamuundo wa Kirusi hawakushughulikia maudhui bali walishughulikia muundo katika kazi ya fasihi. Badala ya kuuona muundo kama njia ya kupeleka mbele maudhui, walichukulia maudhui kama kihamasisho au motisha ya muundo; yaani kama nafasi ya kupeleka mbele aina fulani ya muundo. Kwa mujibu wa wanamuundo, kazi ya fasihi ni kongamano la mbinu mbalimbali za lugha zenye majukumu katika muundo mzima wa matini. Wanamuundo hawa walishughulikia uhakiki kutilia maanani muundo wa lugha tu na wala hawakushughulikia maudhui.

Kwa upande wa lugha wanamuundo wanadai kuwa, kitu kinachotofautisha lugha ya kifasihi na lugha nyingine ya kawaida ni uwezo wa fasihi wa “kulemaza” lugha ya kawaida. Kulemaza huku kunamaanisha kuwa lugha ya kawaida inavutwavutwa, inafinyangwafinyangwa na kupondwapondwa hivyo basi kufanywa lugha ngeni. Kwa

hivyo wanamuundo waliona lugha ya kifasihi kama ukiukaji wa kaida; jambo ambalo wengi wa wahakiki wanadai kuwa hakuna lugha inayotofautiana na nyingine. Zote zinatumia isitiara, jazanda, methali na kadhalika.

Mingi ya misingi iliyowekwa na wanamuundo kuongoza katika utunzi wa tamthilia imepitwa na wakati. Pengo hili la wakati ndilo jambo ambalo limechangia katika mada ya muundo na ukuaji wa kimawazo katika tamthilia za Timothy Arege.

## 1.1 Tatizo La Utafiti

Somo letu la utafiti linajishughulisha na uhakiki wa ukuaji wa kimuundo na mawazo katika tamthilia za Arege. Tutabainisha kwa kujadili ujumla vipengele vinavyodhihirisha kukua kwake kimuundo na kimawazo. Vipengele vya kimuundo tutakavyovishughulikia ni pamoja na ploti, maudhui, wahusika, mbinu za matumizi ya lugha kama vile methali, sitiari, tashbihi, kuchanganya ndimi, n.k. Twachukulia kuwa vipengele hivi vitaweza kudhihirisha kukua kwa mwandishi huyu.

Haipothesia yetu ni kwamba mwandishi anaweza kupiga hatua za kukua kimundo na kimawazo kadri anavyoendelea kuandika. Endapo kazi za mwandishi hazitadhihirisha mabadiliko ama upya, mwandishi hatakuwa amepiga hatua zozote. Tunaamini kuwa kwa kuzichunguza kazi za Arege, tutaweza kuamua kama alikuwa akipiga hatua za kukua kwake au hakupiga hatua zozote. Tunachukulia kuwa kwa kuchunguza miundo na mawazo ya kazi hizo tutaweza kubainisha jinsi zilivyoendelea kuimarika na kuwa bora zaidi. Hii ndiyo itakayokuwa ithibati ya kukua kwa mwandishi. Hii ni kumaanisha kuwa uhakiki wetu utakuwa na lengo la kuangalia jinsi mwandishi huyu alivyojaribu kuboresha sanaa zake kadri alivyoendelea kuandika.

Nadharia tutakayoitumia itatuwezesha kushughulikia fani pamoja na vipengele vingine vitakavyodhihirisha kukua. Tutaichukua tamthilia yake ya mwanzo kabisa ya *Chamchela* na kuisoma kwa makini. Kisha tutachunguza kwa kina namna ambavyo vipengele vikuu vya muundo, yaani ploti, maudhui na wahusika vimeumbwa. Katika kuendelea kuzichambua tamthilia zinazofuatia yaani *Kijiba* cha *Moyo* na *Mstahiki Meya*, tutaweza kutambua kama mbinu za uumbaji wa ploti maudhui na wahusika zinaendelea kuwa bora zaidi na kuboresha sanaa ya tamthilia kwa jumla, au kama haitokei hivyo. Mwelekeo kama huu ndio utakaotubainishia hatua za ukuaji wa kimuundo na kimawazo katika kazi za mwandishi huyu. Kiini cha kulishughulikia somo hili na haswa mada ya kukua kimuundo na kimawazo kwa mwandishi

Arege imetokana na sababu nyingi. Kwanza ni kutokana na hamasa ya kutaka kuendeleza fasihi ya Kiswahili kwa kuifanyia utafiti katika mada hii ambayo haijashughulikiwa. Pili, ni kwamba tunaamini kuwa suala la kukua kwa mwandishi au kukua kwa fasihi, ndilo tegemeo la uhai wa fasihi. Ndiposa tukaonelea kuwa ni muhimu kulichunguza suala hili.

### 1.2 Sababu za Kuchagua Somo Hili

Usomi na tafiti nyingi zilizofanywa juu ya tamthilia katika fasihi ya Kiswahili zimekuwa zikiangazia masuala ya kimaudhui, kifani/kimtindo, usawiri wa wahusika na matumizi ya lugha. Suala la muundo na matumizi yake na ukuaji wa mawazo ya mwandishi au hata mawazo ya utanzu huu, kama limeshughulikiwa, ni kwa ufinyu sana. Kwa sababu hii, tafiti nyingi zimekuwa zikikazania kuonyesha mambo yale yale japo kwa kutumia misimamo na mitazamo tofauti au kwa kuyaangalia kwa kuyahusiana na kazi fulani fulani mahususi. Mbali na kwamba muundo ni chanya na suala tata na ambalo

kwingineko ni suala la kimsingi katika utanzu na usomi wa tamthilia. Tafiti nyingi zilizoko katika utanzu huu hazionekani kuweka umuhimu na kipaumbele katika muundo. Tafiti nyingi zinazofuata mielekeo hiyo ya awali mara nyingi zimesukuma suala la muundo pembeni. Hii ina maana kwamba kutozingatiwa kwa muundo katika kila tamthilia kunabana mambo mengi muhimu na ya kimsingi katika tafiti za tamthilia. Kuna haja na sababu halali kuangalia muundo kama njia ya kukadiria ukuaji wa mawazo, mitazamo na uchangamano wa mambo yanayoshughulikiwa katika tamthilia.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Lengo la kimsingi katika utafiti huu ni kutalii na kuchanganua jinsi ambavyo dhana ya muundo wa tamthilia na ukuaji wa mawazo ya mwandishi ilivyowahi kushughulikiwa katika fasihi ya Kiswahili. Nia hasa ni kuonyesha jinsi ambavyo dhana hii ilivyo tata, isiyokuwa na uelewa wa aina moja au hata ufafanuzi halisi ulio na mwafaka miongoni mwa wasomi na wahakiki wa tamthilia ya Kiswahili, jinsi ilivyowahi kushawishi usomi na utafiti mbalimbali, na kwa kufanya hivyo ikaishia kujenga uelewa changamano wa malengo ya muundo katika usomi na utafiti wa tamthilia. Mbali na uelewa wa aina hiyo, kuna haja na sababu za kutosha kutaka kuiweka dhana ya muundo katika mahali pake pa sawa kiusomi. Kwa kuwa tafiti nyingi juu ya tamthilia zimekuwa zikitilia mkazo masuala ya maudhui, matumizi ya lugha, miundo ya wahusika na baadhi ya masuala ya ufanisi wa tamthilia-iwe inaangalia kama kazi ya kusomwa au kuigizwa jukwaani. Uelewa wa aina hii katika mikabala ya nadharia na ufahamu wa sasa katika tamthilia unaweza kutiliwa shaka, kwa kuwa muundo una athari za wazi na athari fiche katika kubainisha maana na tasnifu ya kazi husika.

Kwa kujikita katika uhalisi huu, utafiti huu unalenga kuonyesha kwamba kuna sababu za kutaka kuonyesha kuwepo kwa mahusiano ya karibu kati ya muundo wa tamthilia na ukuaji wa mawazo ya mwandishi. Hili ni suala ambalo, kutokana na tafiti zetu halionekani kama limetiliwa maanani sana. Baadhi ya sababu za kimsingi zinazochangia kuwepo kwa miundo anuwai ya tamthilia ni pamoja na kutambua kwamba tamthilia huibuka katika miktadha mahususi ya kiwakati, kimazingira na kiusomi, kwa hivyo tamthilia zote haziwezi kuwa na miundo sawia.

### 1.4 Nadharia Tete

i) Ukuaji wa kimuundo na kimawazo hudhihirika kupitia kwa matumizi ya tamathali za usemi, muundo imara zaidi na ujenzi bora.

ii) Kubadilika kwa maudhui kumetokana na mabadiliko ya wahusika katika tamthilia teule.

### 1.5 Upeo na Mipaka

Katika kuchunguza dhana ya ukuaji wa kimuundo na mawazo, tumeshughulikia tamthilia tatu za Timothy Arege: *Chamchela*, *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Tumetumia Nadharia ya Umuundo katika utafiti wetu. Baadhi ya masuala yaliyoshughulikiwa kwa mujibu wa tatizo letu la utafiti ni vipengele vya kimsingi vya muundo wa tamthilia tangu enzi za akina Aristotle. Pia baadhi ya kanuni na sheria zilizotawala utunzi wa tamthilia zimeangaziwa.

Ukuaji au matumizi ya baadhi ya kanuni na sheria hizi umeangaziwa kwa lengo la kudhihirisha mada ya utafiti. Katika kuangalia muundo wa tamthilia, tulipaswa kukumbuka kuwa tamthilia huwa imekusudiwa kuigizwa jukwaani. Hata hivyo hatukusisitiza kipengele cha uigizaji kwa kuwa dhamira yetu haikuwa kuwaongoza

waigizaji bali ni kutusaidia kuhakiki ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za Arege.

Tumeamua kushughulikia suala hili kwa sababu halijatafitiwa na pengo ambalo limetajwa la kiwakati tangu enzi za akina Aristotle hadi hivi karibuni ni kubwa kiasi cha kuwepo kwa mabadiliko makubwa. Kwa upande wa muundo na maasuala-ibuka katika jamii-husika ya sasa. Utafiti wetu pia umetusaidia katika kumulika jinsi masuala ya muundo yalivyohusika katika usawiri wa wahusika. Tumehitimisha kwa matokeo yetu na mapendekezo ya utafiti katika Nyanja hii.

## 1.6 Msingi wa Nadharia

Nadharia ya umuundo ina chimbuko lake katika isimu. Wataalamu wanaotumia umuundo wanaafikiana na kukubaliana kuwa mwasisi wake ni mwanaisimu wa kiswiswi Ferdinand de Saussure. Kazi zake zilichapishwa mara ya kwanza mwaka mwaka wa 1915. Mwanaisimu huyu aliieleza lugha kwa kutumia istilahi zifuatazo:

(i) *Langue*-kama sifa na kanuni za lugha mahsusi kama Kiswahili, ambapo tunapata vipengele kama vile sarufi, sintaksia, msamiati na kadhalika.

(ii) *Parole* –lugha kama inavyotumiwa na mtu binafsi na *Langage* kama lugha zote za ulimwengu.

Mahusiano ya dhana hizi yanaweza kumithilishwa na mahusiano ya vipengele vya sehemu mbalimbali za fani. Katika kitengo hiki, fasihi inaweza kutazamwa kama mfumo. Fasihi za jamii mbalimbali zinaweza kutazamwa kama *langue* za jamii hizo. Kazi ya mtunzi inaweza kutazamwa kama *parole.*

Mfumo wote wa fasihi unaweza kutazamwa kuwa una muundo mmoja ambao umejificha na unaweza kufichuliwa tu kwa kuzitalii kazi mahsusi za fasihi. Katika fasihi tunashughulikia miundo ya kazi teule ambapo vipengele vyake kama vile msuko, mandhari na vingine huweza kufichua muundo halisi wa fasihi kama asasi. Uhusiano katika kazi halisi na fasihi kama asasi umeangaziwa kwa uwazi na

Chomsky. Huyu ni mwanaisimu aliyeiangalia lugha katika viwango viwili:

i) Muundo wa nje

ii) Muundo wa ndani

Muundo wa nje unaingiliana kimaana na *parole* kwa sababu ya matumizi ya lugha na muundo wa ndani unaashiria *langue* kwa sababu ya sheria na kanuni za kisarufi ambazo humwongoza mtumizi wa lugha hiyo. Kazi mahususi ya fasihi-hasa miundo yake, ni kama muundo wa nje. Kulingana na isimu, njia ya kufikia muundo wa ndani ni kupitia ule wa nje. Hivyo ndivyo ilivyo katika fasihi. Yaani muundo wa fasihi nzima ndio muundo wa ndani wa fasihi yenyewe. Kwa jumla muundo huu ndio kielelezo cha fasihi. Kiini cha mwanamuundo katika kuhakiki fasihi ni kuzitazama kazi za kifasihi vile zinavyoingiliana na mfumo wa fasihi kwa jumla. Mhakiki hujaribu kufichua mfumo wa kazi za kifasihi na uamili wake. Kulingana na Culler (1975) anasema, "jukumu la poetiki la kimuundo ni kubainisha muundo wa undani unaoziwezesha mbinu za kifasihi kuwa taathira" Hii ina maana kuwa mpangilio wa vipengele vya muundo wa kazi ya fasihi ambao unaijenga kazi yenyewe ndio unaofanikisha dhamira ya msanii ya kumteka msomaji, mtazamaji au msikilizaji. Jukumu muhimu la mhakiki/mtumizi wa nadharia hii ya muundo ni kubainisha mpangilio huu kwa kuchunguza muundo huku akiashiria jinsi ambavyo mpangiliohusika unavyofaulu kumwathiri msomaji.

Uhakiki wa utanzu wa tamthilia uliwekewa msingi na mawazo ya Aristotle alivyoshughulikia baadhi ya vipengele vya kimsingi katika tamthilia ambavyo vitaweza kumwongoza msomaji anayetamani kuhakiki tamthilia huku akisisitiza suala la uigizaji jukwaani kama tofauti kuu na tanzu zingine za fasihi. Kuhusu msuko wa tamthilia, Aristotle alikiona kipengele hiki kama cha lazima katika muundo wa tanzia. Aliendelea kusisitiza kuwa lazima tanzia ionyeshe umoja wa mahali au mandhari, muda na matendo ili kuendeleza msuko inavyopasa. Msuko wa tamthilia hautakikani kuwa na uchangamano. Pia huhitajika kudhihirika waziwazi ili mtazamaji au msomaji aweze kutambua mapema. Msuko unatarajiwa kuwa na mantiki na taharuki. Mantiki na matendo yanatazamiwa na kuingiliana ili kujenga taharuki.

Kuhusu kipengele cha mazungumzo na masuala ya lugha, Northrope Forge(1957) anasema,"drama ni mwigo wa muhakati wa mazungumzo au maongezi. Sharti mazungumzo yaafikiane na muktadha wa wahusika, mazingira yao au tabaka lao. Wahusika waweze kuwa na lugha zinazowatambulisha kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiitikadi na kisaikolojia. Wahusika katika tamthilia wanadhihirishwa au kuelezwa haraka kwa njia ya waziwazi na zisizotatanisha. Wasiwe wengi kinyume na matarajio ya watazamaji au wasomaji. Ili kufaulu katika haya, mtunzi wa tamthilia hutumia mbinu ya mazungumzonafsi. Mazungumzonafsi yana majukumu kadha katika tamthilia:

i) Hutumika kuyamulika mawazo na hisia za ndani za mhusika.

ii) Hudhihirisha mivutano ya ndani kwa ndani aliyonayo mhusika fulani.

iii) Huendeleza msuko

Ukuaji wa dhamira na maudhui ni kipengele muhimu katika tamthilia. Dhamira ni wazo kuu linalojitokeza, ujumbe au adili ya kazi hiyo. Tamthilia inaweza kuwa na dhamira

inayotambulikana kwa uwazi. Ni sifa nzuri ikiwa dhamira ya tamthilia haisisitizwi waziwazi ili kumwezesha msomaji kufanya juhudi za kuielewa dhamira.

Matumizi ya nyimbo na mbinu nyinginezo za fasihi simulizi hayana budi kuangaliwa. Nyimbo na muziki hutumika kuwasilisha ujumbe na kuimarishwa kwa kazi hiyo. Katika enzi za akina Arisitotle, maigizo yaliimbwa na nyimbo zilitumika kuyatanguliza maonyesho. Maonyesho ni kipengele cha muundo ambacho hufanikishwa pamoja na kuvihusisha vipengele vingine kama vile mandhari, matumizi ya taa, ufungwaji na ufunguaji wa pazia, vipodozi, maleba, majuso au mafigu na mpangilio mzima wa jukwaa. Baadhi ya waandishi wa tamthilia huwaelekeza wasomaji jinsi ya kulipanga jukwaa wakati wa kuigiza. Maelezo ya jukwaa (ni) hutudokezea mandhari, wakati, matendo, ujaji na uondokaji wa wahusika, sifa za jukwaa, maleba na kadhalika. Hutumia lugha ya kinathari na hivyo, kuchukua mtindo wa kisimulizi wa kiriwaya. Njia hii ya kimaelezi humwezesha mwanatamthilia kuyasawiri mandhari vizuri na kwa kikamilifu. Pia hurahisisha utambuzi wa baadhi ya mbinu za kimathali. Ni matumaini yetu kuwa nadharia ya umuundo tuliyoichagua inaweza kutufaa pakubwa kwa sababu inatilia mkazo masuala muhimu kama vile utimilifu wa kifasihi wa kazi zilizohakikiwa.

### 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili

Udurusu wetu kuhusu yaliyoandikwa kuhusu somo hili umekusudia kutekeleza malengo kadhaa ya kimsingi. Kwanza umetuonyesha fafanuzi kadha wa kadha za muundo katika tamthilia katika misingi ya kijumla na katika misingi ya fasihi ya Kiswahili kwa nia ya kuonyesha wajibu, majukumu na mahusiko ya muundo katika kuibusha mawazo na maudhui ya kisasa. Suala la fafanuzi za muundo limetusaidia hatimaye kutathimini ujadi, upya, uchanya, ukamilifu na uchangamano wa muundo katika tamthilia za Arege hasa

kwa kumulika jinsi muundo ulivyofanikisha kumulika ukuaji wa mawazo katika misingi ya nafasi wanazozichukua wahusika katika tamthilia hizi na jinsi nafasi zao zinavyoweza kutumiwa kama msingi wa kutathmini ukuaji wa mwandishi kimawazo.

Pili, tulitaka kuonyesha muundo kama kipengele cha tamthilia unavyoendeleza wazo, uelewa na mwono-ulimwengu wa msanii, jinsi mawazo yake yalivyoibuka katika mchakato wa uchangamano wa matendo unavyowezeshwa na uchangamano wa muundo na kwa hivyo matendo tamthiliani. Kuaminika huku kutafungamanishwa na ukunjufu wa muundo unaowezesha kubainika kwa uhalisia na kuaminika kwa mazungumzo ya wahusika-mambo ambayo hatimaye yametusaidia kutathmini mchango wa muundo katika utanzu wa tamthilia ya Kiswahili. Tumefanya hivi kama njia ya kuweka misingi mwafaka tuliyoitumia hatimaye kupimia tamthilia tulizozichagua katika misingi na imani kwamba, muundo unawezesha mawazo hayo kuibushwa.

Tatu, udurusu huu unakusudia pia kumulika jinsi masuala ya muundo yanavyohusika katika usawiri wa wahusika. Muundo wa tamthilia umeshughulikiwa na wataalam na wahakiki mbalimbali. Tasnifu hii ni tokeo la tathmini za baadhi ya kazi za wataalamu na wahakiki ambao wameshughulikia vipengele vya muundo katika tamthilia mbalimbali. Musyoka (1996) ameshughulikia uhakiki wa fani katika tamthilia za Jay Kitsao. Ameshughulikia uumbaji wa wahusika, uhusika, ploti na matumizi ya lugha. Kwa kurejelea tamthilia za Jay Kitsao, utafiti huu utatuongoza katika uchanganuzi wetu wa ukuaji wa muundo na mawazo lakini kwa kuzingatia tamthilia ya *Chamchela*, *Kijiba* cha *Moyo* na *Mstahiki Meya* wala si tamthilia za Jay Kitsao.

Wafula (1999) katika *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo* yake anatoa muhtasari wa tamthilia ya *Kilio cha Haki.* Aidha anachanganua mtindo alioutumia mwandishi katika tamthilia hii kwa nia ya kubainisha ufungamano uliopo kati ya matumizi ya lugha na ujumbe wake wa kiukombozi. Pia, ameangazia baadhi ya wahusika na kuchanganua tamathali ya usemi katika tamthilia ya *Kilio cha Haki.*

Wafula amejikita katika maudhui na kutoa muhtasari wa kazi hii lakini sisi tutajikita katika tamthilia za Arege.Mwangi (2005) ameangazia kipengele cha fani katika tamthilia za K.W Wamitila. Ameshughulikia msuko, wahusika na matumizi ya lugha. Kazi hii inatufaa sana katika utafiti wetu kwa vile unaangazia vipengele hivi lakini utafiti wetu unahusu tamthilia ya *Chamchela*, *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* ya Timothy Arege. Mbatia (2009) katika *Kamusi ya Fasihi* amefasili vipengele vya kimtindo katika kazi ya sanaa ya fasihi vinavyoijenga tamthilia. Mtaalamu huyu ametoa tu fasili lakini sisi tutachanganua vipengele hivi vya muundo na mchango wao katika ukuaji wa muundo na mawazo tamthiliani mwa Arege na kuangazia namna vipengele hivi vimechangia katika ujenzi wa kazi nzima.

Mulila (2009) ametafiti kuhusu usawiri chanya wa wahusika wanawake katika tamthilia za *Chamchela* na *Zilizala.* Kazi hii hasa *Chamchela* itatunufaisha kwa kurejelea wahusika lakini hatutajikita katika wahusika wanawake tu bali wahusika kwa jumla kama mojawapo ya vipengele vya muundo katika kuendeleza mada. Makala mengine ambayo yatakuwa na umuhimu katika utafiti wetu ni miongozo ya tahakiki mbalimbali kutoka kwa wahakiki tofauti tofauti wa kazi za Arege. Tahakiki hizi zinarejelea vipengele vya umuundo katika uchambuzi wao. Mfano wa tahakiki hii ni wa Khaemba (2012) katika mwongozo wa *Mstahiki Meya.* Ameangazia vipengele vya muundo kwa kuchambua

wahusika, vipengele vya matumizi ya lugha vikiwemo mbinu rejeshi, semi, taswira, jazanda, tashihisi na kadhalika. Pia ametoa muhtasari wa kila onyesho ambao utatusaidia katika kipengele cha uendelezaji wa ploti. Mwongozo huu utatunufaisha kwa upande wa uchanganuzi wa vipengele zaidi vya muundo kama vile maudhui na fani za lugha. Hatutajishughulisha na vipengele alivyovichanganua kama vile kutoa muhtasari wa kila onyesho kwani kwa kufanya hivyo itakuwa kwamba tunautengeneza mwongozo badala ya kufanya utafiti.

Were (2012) ametafiti kuhusu fani katika *Kijiba cha Moyo*. Hiki ni mojawapo cha vipengele vya muundo tutakavyoangazia na mchango wake katika kuendeleza mada ya utafiti wetu. Wataalamu na wahakiki hawa wametilia mkazo sana masuala ya maudhui, matumizi ya lugha wahusika na baadhi ya masuala ya kinadharia hivi kwamba kumejengeka imani potovu kwamba muundo ni suala la kipekee katika usomi na utafiti wa tamthilia.Tofauti na kazi yetu, utafiti wetu unalenga kuonyesha kuwepo kwa mahusiano ya karibu ya muundo wa tamthiilia na ukuaji wa mawazo ya mwandishi. Kutokana na udurusu wa yaliyoandikwa kuhusu tamthilia za Arege tutakubaliana madhumni ya kazi yetu kuwa uhakiki wa fasihi kwa jumla hauna kikomo kwa sababu wahakiki huwa na mitazamo na misimamo tofauti kuhusu kazi moja. Kwa hivyo, utafiti wetu utachanganua ukuaji wa muundo na mawazo katika kazi za Arege kwa undani.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Kwa vile utafiti wetu ni ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za TimothyArege, tutazisoma tamthilia hizi zote kwa kina. Tutatilia maanani vipengele vya muundo kama vile matumizi ya lugha, uhusika, ploti, maudhui na dhamira. Maandishi mengine yatakayokuwa na umuhimu katika utafiti huu ni yale yanayoshughulikia nadharia

tuliyoitumia. Maandishi hayo yatatuimarisha pakubwa katika nadharia ya umuundo. Maktabani pia patakuwa ni sehemu muhimu katika utafiti wetu. Tutavidurusu vitabu, tasnifu na majarida yanayojadili umuundo. Tutashauriana na wataalam mbalimbali ambao pia ni wakufunzi wa fasihi katika idara ili kupata kupata ushauri zaidi kuhusu utafiti wetu. Tumehitimisha kwa kuonyesha matokeo yetu na mapendekezo ya utafiti zaidi katika nyanja hii.

# SURA YA PILI

# MSUKO NA MCHANGO WAKE KATIKA TAMTHILIA ZA AREGE

## 2.1 Utangulizi

Kile kitakachotushughulisha hapa ni dalili za kuimarika kwa ukuaji wa mwandishi Arege pale ambapo uumbaji wa ploti unahusika. Bila shaka uumbaji huu haukamiliki pasi na kuwashirikisha wahusika. Kuhusiana na ploti ya tamthilia hizi ni kuwa, matukio yote ya kimsingi kama yalivyopangwa yana sababu maalum;yanachangia katika muala na mtiririko wa ploti na hadithi kwa jumla. Hizi ni sifa muhimu sana katika utimilifu wa kifasihi wa tamthilia yoyote ile. Sifa zilizotajwa zinaonyesha ufundi wa mwandishi; kwamba amezifikiria na kuzipanga kazi zake kwa makini kama inavyomjuzu mwanasanaa bora. Msuko huzua maswali kama; Kwa nini ikatokea hivi? Kukatokea nini baadaye?

Maswali kama haya humsisimua msomaji na kuvutia shauku ya kutaka kuendelea kusoma ili apate majibu yake. Msuko ni mfuatano au mfululizo wa matukio yanayoijenga tamthilia na namna matukio hayo yanavyosababishana. Msuko au ploti unaweza kuelezwa kuwa matukio mchezoni au mtiririko wa vitendo hivyo vinavyozuana. Matukio haya yanasababishana na kuelekezana kwenye usuluhisho fulani.

Mpangilio wa matukio unatusaidia kuona madhumuni au dhamira ya mwandishi. Msuko ni sehemu muhimu sana katika tamthilia. Mgogoro mmoja husababisha mwingine na mivutano hiyo ndiyo inayosukuma mbele tamthilia hadi inapofikia kilele.

Harry (1984:239) anasema kuwa, tamthilia nzuri ni ile ilyojengwa vizuri kutokana na migogoro ambayo hupitia hatua mbalimbali kabla ya kutatuliwa. Anadai kwamba, lazima

kuwe na matatizo yanayomkumba mhusika mkuu na migogoro kati ya mhusika mkuu na mkinzani wake. Migogoro hii lazima iibue taharuki.

Mohamed (1995:64) ameifasili ploti kama: Majilio ya matukio mbalimbali katika kazi ya sanaa yalivyopangwa kutokana na visababisho na matokeo katika tamthilia. Anaendelea kusema kuwa ploti huenda sambamba na jinsi migogoro ya tamthilia hiyo inavyofunguka kutokana na nguvu za visababisho na matokeo.

Kwa upande mwingine Gill (1995:104) anasema kuwa ploti inahusu wahusika na yale wanayotarajiwa kuyafikia, wanayotaka na wanayotenda ili kufikia malengo yao. Mwandishi wa tamthilia huwa na jukumu la kukuza wahusika ili waweze kujenga ploti ya kazi yake.

Tukimrejelea Wamitila (2003:207) ameifasili ploti kuwa ni mpangilio wa matukio katika kazi ya fasihi kiusababishi hivi kwamba tendo moja linasababisha tendo linalofuata hadi tamati.

Aristotle naye alibainisha kuwa msuko ni uti wa mgongo katika tamthilia ya kitanzia.Alipendekeza kuwa, lazima tanzia ionyeshe umoja wa mahali au mandhari, muda na matendo ili kuendeleza msuko inavyopasa. Alidai kuwa msuko huathiri kwa kiwango kikubwa maendeleo ya kimuundo na matendo yaliyopo. Ameendelea kusema kuwa msuko lazima udhihirike waziwazi ili mtazamaji au hata msomaji aweze kuutambua kwa urahisi. Aidha, msuko unatarajiwa kuwa na mantiki na taharuki. Matukio na matendo yanatazamiwa kuoana na kuingiliana kimantiki na kwa namna ya kujenga taharuki.

Aristotle anaeleza aina mbili za mtiririko wa vitendo katika tamthilia. Mtiririrko wa tendo sahili au rahisi na mtiririko changamano. Mtiririko sahili haufuati sheria za uelekevu. Vitendo hutokea kwa njia ya kuwavutia wachezaji au watazamaji. Ilhali msuko wa ploti changamano ni ule unaofuata sheria za lazima au uelekevu.

Kimsingi, uchanganuzi wa ploti katika tamthilia hurejelea masuala muhimu ambayo ni pamoja na jinsi ploti huanza, maonyesho na visuko, kasi ya ploti, matarajio na mshangao, upeo na jinsi ploti huhitimishwa. Vipengele hivi hukuza na kuendeleza migogoro kati ya wahusika. Utafiti wetu umeangazia baadhi ya vipengele hivi kwa kurejelea kazi tulizoziteua.

## 2.2 Mchango wa Msuko Katika *Chamchela*

Kazi ya mwanzo ya msuko tutakayoiangalia katika sehemu hii ni *Chamchela.* Katika utangulizi wa kazi hii, mwandishi mwenyewe anatupa fununu juu ya mambo yanayosimuliwa humo. Anatwambia hivi kwa muhtasari katika aya ya kwanza inayofuata:

*Chamchela* ni tamthilia inayotathmini mkinzano uliopo kati ya pande mbili za wanajamii; mmoja wenye kuvutia katika jana na leo na mwingine katika leo na kesho. Kwa muhtasari hadithi hii inamhusu kijana maskini, Mayaka ambaye anajikuta baina ya kauli mbili ambazo zinamzonga. Kwa upande mmoja, jamaa zake wanamsukumia shinikizo la kumtaka aukate uhusiano wake na Bisase. Kwa upande mwingine, Bisase ni mfadhili wake mkuu katika hali yake ya uhitaji.

Tamthilia inapoanza, tunamkuta mzee Sure akiwa na Atisa. Dhamira ya kukutana naye ni kumtaka Atisa amkabidhi nduguye Mayaka risala ya kuja nyumbani ili kujadili kuhusu uamuzi wake wa ndoa anaoudhamiria kuuchukua kinyume na matarajio ya jamii. Kama tunavyoarifiwa baadaye, Kijana Mayaka mwenye umri wa miaka ishirini na sita, anauchukua uamuzi wa kumwoa Bisase ambaye ni ajuza wa miaka sitini na mitano. Hili ni pigo kuu katika jamii ya Chamchela. Kwa Atisa, suala la kumtafuta na kumpata aliko nduguye Mayaka ni sawa na kuitafuta sindano ndogo katika shamba kubwa la ngano. Kwanza kabisa, Atisa hajui alikokuwa amehamia nduguye Mayaka. Pili, haoni vyema kuingilia uamuzi wa nduguye hasa kuhusu suala hili nyeti la ndoa. Ami yake mzee Sure hakubaliani na Atisa kuhusu sababu hizo. Anapinga vikali na kusisitiza kuwa sharti Atisa autekeleze wajibu huo kwa niaba ya familia. Kutofuatilia katika jambo hilo ni kukubali kushindana katika kupigania ukoo wa jamii yao.

Baada ya Sure na Atisa kuachana, keshoye asubuhi katika onyesho la pili, Sure anaraukia kwa marehemu nduguye kuwajulia hali. Kutokana na kurundikana ovyo kwa vifaa na makochi makuukuu kwao kina Mayaka ni ishara tosha kwamba hii ni jamii maskini. Kupitia mazungumzo kati ya Mbiki na Sure, Mbiki anasikitika kugundua kwamba, mke wa nduguye kwa jina Rosa ni mgonjwa na chanzo cha maradhi yake ni habari aliyokuwa amepokea kuhusu mpango wa ndoa ya mwanawe Mayaka na Bi. kikongwe Bisase. Fikira nyingi za Rosa kutokana na balaa hii zinasababisha hata aanze kujizungumzia binafsi. Sure anaukata ushauri kuwa Rosa apelekwe hospitali ilhali Rosa haoni umuhimu kwani anadai kuwa atapata nafuu. Kwingine Rosa anaona heri afe badala ya kuendelea kuishi kushuhudia maovu kama hayo katika maisha ya mwanawe ampendaye. Yaelekea kuwa wote hawa walikuwa wameshindwa kumzuia Mayaka kumwoa kikongwe huyu Bisase.

Walikuwa wamemwita mara tatu ili aje nyumbani wasuluhishe jambo hili lakini Mayaka alikuwa hauitikii wito huo. Ni bayana kuwa hiki kilikuwa ni kizazi tofauti kabisa kulingana na maoni ya mzee Sure.

Mama Bisase anaishi katika jumba la kifahari kutokana na mandhari ya sebuleni ambayo yamepambwa makochi ya kifahari. Licha ya hayo, Bisase haonekani kuwa na utulivu jioni hiyo kutokana na kurandaranda kwake hapa na pale. Kupitia kwa mawazo yake moyoni, yanathibitisha hali ngumu ya mateso ya ujane anayoyapitia. Malezi ya mjukuu wake Lema aloachiwa na bintiye Sera pia ni mzigo kwake. Akiwa katika hali hii ya uzungumzinafsia, ndipo kisadfa anaingia mjukuu wake Lema kutoka shuleni. Lema naye hana utulivu shuleni kwani kila siku hubaki akichekwa na wanafunzi wenzake anaposhindwa kumtambua babake mzazi na kazi wazifanyazo wazazi wake. Mbali na kusomea shule nzuri, lishe bora na mavazi mazuri, bado Lema ana pengo moyoni ambalo limemtia shaka. Kufikia hapa mtunzi anataka kusawiria picha kuhusu jukumu muhimu la baba mzazi katika jamii. Mama Bisase ana kila kitu ila ni mjane. Mjukuu wake Lema naye ni vivyo hivyo kwani hata yeye hana baba mzazi.

Keshoye nyumbani kwa Bisase, anaonekana akiketi tayari kukabiliana na bintiye Sera kumhusu mjukuu wake Lema. Sera amekuwa kiruka njia. Yeye anadai kuwa mali aloachiwa na marehemu babake yanatosha kumlea mwanawe Lema. Bisase naye anapinga hili kwa kujitetea kuwa mali peke yake hayatoshi katika kumlea mwana kwani mapenzi ya mama kwa mwanawe ni jambo muhimu na ni haki pia ya mtoto kumjua babake mzazi ni nani. Bisase anajaribu kumkanya na kumwonya dhidi ya shughuli zake za usiku usiku anazozitekeleza mjini. Wakiwa katika makabiliano hayo Mayaka anaupisha mlangoni akitaka kuingia. Sera anaushuku uhusiano wa mamake na Mayaka

jambo ambalo amemthibitishia kuwa Mayaka amekuwa akimfaa katika kumtekelezea majukumu muhimu ya kimsingi na zaidi ya hayo kumwondolea upweke. Kwa Sera hili ni jambo la aibu lakini mamake hajali.

Huku hayo yakiendelea mle chumbani mwa Mama Bisase walinzi wa mlango nje ya makao ya Bisase walikuwa katika mazungumzo yao kuhusu uhusiano uliokuwa umechibuka kati ya kijana Mayaka na mkongwe Bisase. Atisa, ambaye pia ni nduguye Mayaka alikuwa nje ya lango kumletea Mayaka risala kutoka nyumbani kuwa alikuwa anahitajika na amu yake pamoja na mamake Rosa ambaye alikuwa mgonjwa. Wanajadiliana pia kumhusu Salima ambaye alikuwa mchumba wake Mayaka. Mayaka alikuwa ameukata na kuutupilia mbali uhusiano wake na Salima. Hata hivyo, alikuwa amemwahidi nduguye kuwa atawatembelea nyumbani ila hakuwa na uhakika ingekuwa ni lini.

Katika onyesho linalofuata, tunakutana na vijana wawili Rukia na Kofa. Vijana hawa ni wasomi na wote wana shahada za digrii. Wamo barabarani katika mazungumzo yao kuhusu ugumu wa maisha. Hata ingawa wamo vibaruani, vipeni vya kulipia nyumba, chakula na mavazi wanavyovipata mwishoni mwa mwezi havitoshi kugharamia hayo. Wakiwa katika mazungumzo hayo, Lema anafika na vitabu mgongoni akionekana mchovu. Baada ya kupokezana salamu waliendelea na mazungumzo yao kuhusu kutowajibika kwa wanaume katika ndoa. Wanadai kwamba wanaume wanawazaa watoto wazuri kama vile Lema na kuuachia ulimwengu kuwalea. Jambo hili linapingwa vikali sana na Kofa kwa madai kuwa wanaume hawa ndio mihimili mikubwa katika familia. Pia akina mama wengi wamekuwa wakiwakosea heshima vijana wa kiume wengi huku Mayaka akiwa mfano mzuri. Msimamo wa Kofa

kuhusu ndoa ni kuwa ndoa ni uamuzi wa mtu binafsi kwani kipendacho roho hula nyama mbichi.

Nyumbani kwa Bisase, Mayaka hana utulivu. Tayari amebandikwa majina kama vile goigoi kuhusu hatua aliyokuwa ameichukua pamoja na Bisase kuhusu suala la ndoa. Kwake Bisase Mayaka amekuwa mfadhili mkuu. Mayaka anadai kuwa hata Bisase anaungana na dunia kumcheka. Anasumbuliwa na nduguze Atisa na Sera wanaomtembelea mara kwa mara. Ugonjwa wa mamake pia ni jambo linalomkera. Bisase anapendekeza mamake Mayaka ambaye pia ni mgonjwa apelekwe kwake kwa matibabu zaidi lakini Mayaka anaona ugumu wa mamake kukubali ombi hilo. Bisase anahitimiza onyesho hili kwa kumkumbusha Mayaka kuwa na msimamo katika jambo lolote liwe ni baya au zuri, gumu au rahisi, refu au fupi. Kwa Mayaka imemwia vigumu kujinasua kutoka mtego huu hatari wa mapenzi.

Baada ya wiki moja jioni, Sure, Kobia na Atisa walikuwa wameketi nje ya nyumba ya Sure huku wakionekana wenye jambo lililokuwa linawatatiza. Abaya na Kobia ni wazee wa kijiji. Walikuwa wameitikia mwito wa Mzee Sure huku wakiwa na wingi wa matumaini kuwa penye wazee habaharibiki jambo. Linalomshangaza sana Sure ni kuhusu wimbi la mabadiliko analolishuhudia ulimwenguni.

Wanadai ya kwamba, dunia ya sasa yaenda kinyume na matarajio. Hatua aliyoamua kuichukua Mayaka kuhusu suala la ndoa ni thibitsho tosha. Hili lilikuwa moja kati ya mambo ambayo yangejadiliwa katika kikao hicho. Salima mchumbawe Mayaka pia alikuwa aangaziwe katika kikao hicho. Kikao hicho kilijaribu kulinganisha na kulinganua

maisha ya kisasa na ya kale. Teknolojia ni njia mojawapo ambayo imechangia katika hili. Abaya na Atisa wanaelekea kuwa na msimamo mmoja wa kumuunga mkono

Mayaka ilhali Sure na Kobia wana msimamo tofauti. Baada ya Atisa kuhakikishiwa na kikao kuwa Mayaka hasemeseki wala kuambilika, Sure anampendekeza Atisa aseme na Salimu kuhusu hatua ya Mayaka ili awe huru.

Siku ya pili, tangu kuvunjika kwa kikao kile, Atisa anaonekana nyumbani kwake akiwa na mawazo tele. Mapenzi ni kizunguzungu hasa akiyarejelea mapenzi kati ya Mayaka na mamake mzazi Rosa. Mara mlango unabishwa na anaingia Salima. Baada ya kujuliana hali na Salima, anamdokezea Atisa kuwa anatoka hospitali kumtembelea mgonjwa (Rosa). Atisa anaonelea kukivunja kimya kwa kuwasilisha jukumu aliloachiwa na kikao kile. Salima anafichuliwa ukweli kuhusu msimamo wa Mayaka. Salima naye anajitetea kuwa ndoa ni suala la watu wawili na mbali na kupendwa na wazee na familia ya Mayaka, tayari naye alikuwa ameufikia uamuzi wa makataa waliokuwa wameuweka kati yake na mchumbake.

Baadaye mchana tunakutana tena na Atisa akiwa hotelini bado akionekana ana wasiwasi mwingi kadri muda ulivyokuwa unaendelea kusonga. Pembeni mwa Atisa palikuwa na watu wawili waliokuwa wanaendelea kujiburudisha. Majukumu aliyopewa Atisa kumhusu nduguye Mayaka hayamwachi kujizungumzia peke yake. Wawilli hao wanashituliwa na hali hii ya Atisa kiasi kwamba, wanamwamuru mhudumu amtoe Atisa nje lakini mhudumu huyu anawakataza huku akitoa sababu kuwa Atisa hakuwa amesababisha vurugu lolote. Pili, mhudumu huyo anadai kuwa Atisa alikuwa anasumbuliwa na majukumu ya nyumbani aliyotakiwa kuyatekeleza kumhusu nduguye

Mayaka aliyemwacha mchumba wake nyumbani kwenda mjini kutafuta kazi na kuishia mikononi mwa mama Bisase kama mumewe

licha ya mama huyo kumzidi umri. Kulazwa kwa mamake Atisa hospitali pia ni sababu nyingine ya kuchangia Atisa kuwa na wingi wa mawazo. Mara anaingia Mbiki, dadake Atisa anayewadokezea kuwa hali ya mamake Mayaka pale hospitali haikuwa nzuri. Ombi la mgonjwa ni kuwa alitaka amwone mwanawe Mayaka na aseme naye. Punde si punde Mayaka anaingia na kujiunga nao. Kutokana na mazungumzo yao, Mayaka bado anaonekana kushikilia msimamo wake kuhusu uamuzi wake wa kumwoa Bisase. Mayaka aliwahi kumfaa sana dadake Mbiki alipokuwa karibu aolewe na mzee wa miaka sitini.

Kulingana na Mayaka kila binadamu anao uhuru wa kuchagua, kubadilli mipango na mawazo pia. Mayaka anadai kuwa ndoa inaweza kukamilika bila watoto. Ni kupitia kwa Mayaka ambapo kumbukumbu za marehemu babake zinajitokeza wazi. Babake alikuwa ni mtu aliyeshindwa kutekeleza majukumu muhimu ya kimsingi katika familia. Mara ya kwanza kuonekana alikuwa ameletwa nyumbani akiwa mgonjwa. Alitumia muda wake mwingi akiwa Tanzania kupasua mbao. Alirudi nyumbani bila mali wala pesa. Mayaka anakuja kwa nia ya kumpeleka mamake mjini kwa matibabu zaidi jambo ambalo halingewezekana kulingana na maoni ya Mbiki na Atisa.

Siku ambayo Rosa alikuwa anamtarajia mwanawe Mayaka kuonana naye uso kwa uso hatimaye iliwadia. Mayaka aliongozwa na nesi hadi chumba alimokuwa amelazwa Rosa.Mamake Mayaka kusikia habari za kufika kwa Mayaka haamini masikio yake. Mayaka anapomkaribia mamake kwa mazungumzo, mamake alinyamaza kabisa na kukataa kuongea naye. Badala yake anageuka kitandani na kumpa kisogo. Alijaribu

kumgusa lakini mamake hakugeuka kabisa. Anapiga magoti kumwomba mamake msamaha lakini akiwa katika hali hiyo, nesi anajitokeza tena mahali analala mgonjwa Rosa na kuanza kumfunika kitambaa huku akionekana anayekosa makini. Nesi anamsihi Mayaka arudi baadaye kwani mgonjwa anatakiwa apate muda wa kutosha wa kupumuzika. Hapa ndipo hadithi inapoishia.

### 2.2.1 Usanifu na Uibukaji wa Muundo na Mawazo ya *Chamchela*

Katika kijisehemu cha kwanza cha uhakiki wa tamthilia ya *Chamchela*, tumejaribu kuyachagua matukio muhimu zaidi katika tamthilia na sababu za kutokea kwayo. Kufikia hapa tunaweza kujadili iwapo Timothy Arege alikuwa anapiga hatua yoyote katika kukua kwake pale ambapo uumbaji wa ploti unahusika. Jambo ambalo linabainika wazi katika mtazamo wa ploti ya *Chamchela* ni kuwa kuna matukio machache ikilinganishwa na *Kijiba Cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Kipengele hiki kinachangia sana katika kuifanya tamthilia ya kwanza kuwa ya kuvutia zaidi kuliko ya pili. Matuko katika tamthilia hii yameoana vizuri na yanafuata mkondo madhubuti wa moja kwa moja wa kimantiki. Yote yana wiano mkubwa na mhusika mkuu Mayaka.

Aidha, *Chamchela* ikiwa ni ndiyo tamthilia ya kwanza kabisa aliyoitunga Arege, inakuwa ndiyo msingi wa kupimia hatua ya ukuaji wa kimuundo na mawazo katika tamthilia za baadaye. Itadhihirika pia kwamba, urefu wa kazi, mpangilio wa matukio pamoja na mvuto wao ndivyo vitakavyokuwa vigezo vya kupimia kukua kwa Arege kulingana na kipengele hiki.

Mwandishi amefaulu katika hili kutokana na matumizi ya mgogoro katika viwango viwili tofauti:

Kwanza, katika nafasi ya muhusika mkuu Mayaka na wazazi wake kunao mgogoro kwani wazaziwe wanaupinga uhusiano wa Mayaka na kikongwe Bisase. Pili kuna mgongano kati ya Mayaka na kaida fulani za kijamii hasa katika suala ndoa. Mgala muue na haki umpe. Kasoro moja katika ploti, hatuoni hatuoni sababu ya Mayaka kutokea mwishoni mwa tamthilia. Mamake anabaki kimya hadi dakika ya mwisho. Haieleweki aliokoa hali ya mamake vipi. Hii ni sadfa ambayo inadhoofisha mtiririko wenye mantiki na matukio. Kwa kiasi kikubwa inaathiri mada ya utafiti wetu.

### 2.2.2 Msuko Na Mchango Wake Katika Kijiba Cha Moyo

Tukizingatia tarehe ya kuchapisha (2009), *Kijiba cha Moyo* ndiyo tamthilia ya pili ya Arege. Ni tamthilia yenye ploti changamano ambayo imekuza na kujenga mgogoro na mivutano kwa ubunifu zaidi ya ile ya *Chamchela*. Tamthiia hii imegawanywa katika sehemu sita ambapo kila onyesho linachangia katika kuendeleza msuko wa tamthilia hii. Kama muhtasari wa ploti unavyoonyesha, matukio ni mengi kuliko *Chamchela*. Kwa kifupi na kwa ujumla, *Kijiba Cha Moyo* imedhamiriwa kuisuta kila jamii kukitambua kijiba cha moyo (tiba) ilicho nacho kusuluhisha matatizo iliyo nayo.

Katika familia ya Sele, kumekosa utulivu kwa kughasiwa na ugonjwa wake. Kwa Sele, kila tendo analiona kuwa ni uonevu. Moyo wake umeingia kutu. Si rahisi kujua umeponzwa na nini.

Hivyo ndivyo ilivyo hata kwa mataifa nayo. Vijiba hivi vya moyo vinazuia uhusiano mwema baina yao. Tamthilia hii inafanya mataifa kujipekua na kujichunguza kuhusu vijiba vinavyoyaandama mioyoni ili kupata tiba na uhusiano ufaao katika karne hii kwani kila moja ina kijiba chake cha moyo.

Mwanzoni mwa tamthilia, Arege anatudokezea tendo la kidrama. Tamthilia yenyewe inaanzia nyumbani

kwa Sele na mkewe Aisha. Kwa mara ya kwanza kabisa tunakutana na Aisha akiketi akisoma gazeti huku mumewe Sele akishika tama akiwazia mengi-hali ambayo inamhuzunisha Aisha sana na kuitia jamaa yake wasiwasi mwingi.

Aisha anaamua kumkabili mumewe akitaka kujua kilichokuwa kinamsumbua moyoni lakini Sele anakiri na kudai kuwa yeye ni mzima kabisa wa afya wala hahisi maumivu yoyote. Mazungumzo kati ya Sele na mkewe Aisha yanaonyesha kutokubaliana katika jambo fulani. Katika kupitisha wakati, Aisha anamkumbusha Sele kuhusu safari waliyokuwa wameifunga kwenda baharini. Baadaye, tunadokezewa kuwa safari hii haikumfurahisha Sele kamwe. Anatoa sababu zifuatazo:

i) Mapambano makali dhidi ya mawimbi baharini hasa mtu anapopiga mbizi.

ii) Mawimbi hatari ambayo yanaweza kusababisha kifo.

iii) Licha ya kuwa na polisi na waokoaji, Sele anadai kuwa hata wao ni binadamu ambao hawawezi kushindana na mapepo ya baharini.

Ili kumwondolea mumewe upweke, Aisha anampendekezea Sele wacheze ngoma akidai kuwa muziki una uwezo wa kuhimiza nafsi kwa viumbe. Sele anapinga wazo hili kwa kudai kuwa moyo unaweza kutulia huku mwili ukijitesa. Wanaanza kwa muziki wa taarabu unaoeleza kuhusu misukosuko ya maisha. Sele haridhiki na muziki huu. Anadai kuwa anapenda zile nyimbo za haraka haraka.

Anapochezewa zile za mwendo wa kasi, Sele anadai kuwa zinamfanya kurusha viungo vya mwili ilhali moyo wake hauruki. Anaendelea kudai kuwa wimbo wenyewe

unamuumiza na kujihisi mtumwa hata katika wimbo wenyewe.Sele kamwe hawezi kuridhishwa na ngoma yoyote ile. Anabaki pale pale kama alivyokuwa katika hali ya mwanzo. Chanzo cha mabadiliko hayo ni kuachishwa kazi.

Matukio katika onyesho la pili yanafanyika ukumbini nyumbani kwa wazazi wa Sele. Zainabu mamake Sele, anaonekana ameketi ukumbini akifuma kitambaa. Mara mlango unabishwa na anaingia Bi.Rahma (shangaziye Zainabu) kuja kumjulia hali. Zainabu anamdokezea Bi.Rahma kuwa hali ya mwanawe si nzuri kwani anaonekana kama mtu anayejitenga sana na watu. Hamu ya chakula pia hana lakini halalamikii kuumwa popote. Bi.Rahma anamsingizia mkewe Sele kuwa ndiye hampikii vizuri, jambo ambalo linapingwa vikali na Zainabu. Sele hali vidagaa kwa kuvihurumia wala hali papa kwa kudai kuwa papa wanakula vidagaa. Bi.Rahma anamhimiza Zainabu ampeleke Sele kwa mganga au afanyiwe kafara.

Wakiwa katika mazungumzo hayo, mara anatokezea Aisha na baada ya kupeana mkono na Bi.Rahma anaelekea chumbani na kuanza kuchakurachakura vitabu. Jambo hili halimpendezi Bi.Rahma Anadai kwamba hivi ni kuwapuuza wao kama wazee. Anamsihi Aisha ajaribu kutumia maneno matamu kwa mumewe ili amweleze shida zake. Watatu hao wanaachana huku wakikubaliana kuwa Zainabu atafute waganga wa kumtibu.

Magharibi moja nyumbani kwa Zainabu akiwa anaendelea kuosha vyombo karoni anaingia Musa (Babake Sele) na kusimama mlangoni mwa jikoni bila ya Zainabu kutarajia. Baada ya kukata kiu kwa maji, wanafungulia majadiliano kuhusu wasiwasi dhidi ya mwanao Sele. Shida hii imeibuka baada ya Sele kuachishwa kazi. Kulingana na maoni ya Musa ni kuwa Sele haumwi popote na ingemfaa kushirikishwa kwanza kabla ya

kuchukuliwa hatua yoyote. Pia anamsihi mkewe Zainabu asikubali kushinikiza mambo kabla ya kuondoka kwake na kumuacha Zainabu akiendelea na shughuli zake za kusafisha vyombo.

Siku hiyo jioni nyumbani kwa Sele anaonekana mwenye mawazo mengi lakini mtulivu. Alikuwa ameketi kochini. Mara Bi.Rahma anabisha hodi na baada ya kujuliana hali, Sele anakiri kuwa yeye si mgonjwa ila ni mzima na buheri wa afya kabisa. Mazungumzo yao yanapozidi kuendelea inadokezea baadaye kwamba chanzo cha shida za Sele ni kule kusimamishwa kazi. Kunyamaza kwake na kujitenga kwake kutoka kwa watu ni kutaka kupima uhusiano wake na watu wenye nguvu na wasio na nguvu.

Kimya hiki ndicho kinachomtia kila mtu wasiwasi kijijini na hivyo basi Bi.Rahma anamsihi Sele kukivunja kimya chake.Baada ya siku kadha kupita, Sele anatokezea tena asubuhi akiwa mbele ya kioo katika chumba chake cha kulala akigusagusa pua yake kwa makini na kujitazama huku akionekana mwenye wasiwasi. Akiwa katika hali hiyo mara anashitukia kuingia kwa Aisha pale chumbani lakini hatoki kwenye kioo. Kuingia huku kwa fujo kunamkasirisha Sele ambaye anamfukuzilia mbali Aisha lakini yeye hatoki mle kwa kutaka maelezo kuhusu kioo.

Sele anataja mambo yanayomsumbua kama vile pua lake na uso mbaya kwa jumla. Rangi ya ngozi yake pia haithamini. Inamkera. Hatimaye Aisha anaanza kumbembeleza Sele aketi amweleze shida zake. Anamsihi na kumhimiza Sele umuhimu wa kujithamini. Kuhusiana na ugonjwa wa Sele, daktari anapendekeza Sele afanyiwe "*plastic surgery*" muradi moyo wake upate kutulia. Mazungumzo hayo hayaishii hapo. Mjadala kuhusu papa unashuka. Kuwala vidagaa, kupigana wao kwa wao na bahari kuchafuka.

Siku hiyo alasiri, nyumbani kwa Sele tunamkuta akiketi huku akishika tama na kuwa katika hali ya kujiinamia. Anatikisa kichwa kama anayekubali jambo fulani na mara kama anayekataa jambo.

Wanapoingia Zainabu na Bi.Sele wanamkuta katika hali ya kujiinamia. Sele anaanza kuinua mikono yake juu kama mtu anayekifukuza kitu fulani. Kisha anaanza kusema kama anayenong'ona, halafu anacheka kicheko kirefu ambacho kinawashitua Zainabu na Bi.Rahma. Zainabu anamwita Sele kwa sauti ya juu lakini anapoulizwa kama anaumwa anakataa kata kata. Anaonekana kama mtu anayepigana na upepo. Baada ya kimya kifupi, Mjadala kuhusu vidagaa unaanza. Habari kuhusu vidagaa na papa pia zinaanza. Kuhusu uso, Sele anakiri kuwa unamsumbua. Pia Wanajadili vile vile kuhusu maisha yao ya utotoni. Sele anapendekeza aimbiwe wimbo wa Siti binti Saadi. Anaonekana kama mtu aliyechanganyikiwa lakini asiyeweza kushindwa katika kusema.

Jioni moja, nyumbani kwa wazazi wake Sele, tunamkuta Musa (Babake Sele) akiketi ukumbini akisoma gazeti. Mara anaingia Aisha na sharubati mkononi bila ya Musa kumwona.Amemtembelea mwanawe ili kumjulia hali kuhusu maradhi yake. Anamdokezea kuwa Sele tayari alikuwa ameamua kwenda kumwona daktari wa kigeni kuhusu maradhi yake ya moyoni. Madaktari wengi walikuwa wamemtazama ila Sele hakuwa ameonyesha mabadiliko yoyote. Baada ya majadiliano mafupi kati ya Musa na Zainabu kuhusu ugonjwa wa mwanao Sele, anaingia Sele na kukiri kuwa bado ni mzima wala hasumbuliwi na chochote. Kwa vile anaona ugumu wa kulishughulikia jambo hili peke yake, anamwita mkewe Zainabu pamoja na Aisha ili kujadiliana.

Magharibi ilikuwa inakaribia. Sele alikuwa ameketi kitandani akiwa mtulivu. Sele alikuwa tayari kwa matibabu lakini kwanza alikuwa na maswali ya kujibiwa. Anataka kujua kuhusu muda ambao angekaa pale hospitalini. Pia ana wasiwasi kuhusu mabadiliko ya rangi ya ngozi yake na gharama za matibabu yake.

Maswali haya yanamkasirisha sana daktari anayedai kuwa yanampotezea muda wake kwani kulingana naye "*time is money*" Sele anakiri kwamba bado hata kama alikuwa hospitalini alikuwa haumwi na hivyo basi anaomba arudishiwe pesa zake. Hatimaye daktari anamhakikishia Sele uwezekano wa kumpa dawa za kubadilisha ngozi. Siku inayofuata hospitalini katika chumba cha Sele, anaonekana ameketi pembeni mwa kitanda chake. Anaingia Jamila (nesi) na vifaa vya kumpimia ambavyo anaviweka mezani. Hawa wawili walikuwa wamesoma pamoja katika shule ya upili ya Mikanjuni. Sele anapimwa lakini matokeo yake yanahifadhiwa asiambiwe habari yoyote kuyahusu. Pia kwake ananyimwa uhuru wa kuchagua chakula anachotaka kula pale hospitalini. Jamila anadai kuwa ni daktari aliye na uwezo wa kutoa maelezo kuhusu hali ya mgonjwa, jambo ambalo Sele haelekei kukubaliana nalo.

Ni adhuhuri nyumbani kwa Amri (Babake Sele) ambapo Amri ameketi kwenye mkeka akinywa kahawa chungu pamoja na Musa. Musa alikuwa amepeleka ujumbe kuwa Sele alikuwa hajatoka nyumbani tangu atoke hospitalini. Licha ya kuziharibu pesa zake bila matibabu yoyote, Musa anaendelea kudai kuwa Sele hamsikilizi wala kujali maslahi ya mtu yeyote. Si wazazi si mkewe. Alikuwa ni kama sikio la kufa. Amri anamnyooshea Musa kidole cha lawama kwamba ndiye aliyempa Sele uhuru kupita kiasi-uhuru ambao umefika ukingoni kama anavyodai Mzee Amri.

Jioni hiyo barazani kwake Amri, anaonekana ameketi huku akiunga wavu wa kuvulia ambao ulikuwa na mianya. Mara anaingia Sele kutoka hospitalini huku akidai kuwa iwapo angeenda moja kwa moja hadi nyumbani kwao, angesumbuliwa na maswali. Analalamikia kufuatwafuatwa kama mfungwa. Jambo analoliona kuwa utumwa. Kuhusu uhuru anaoutaka Sele, babake hakubaliani naye. Anasisitisa kuwa hata katika huo uhuru kuna utumwa. Wakiwa katika majadiliano hayo, Aisha anafika huku akihema.
Alikuwa ameenda kumwangalia Sele huku akithibitisha kuwa hakuna aliyekuwa ametulia tangu kutoweka kwake. Baada ya kuamrishwa kurudi na Amri, anamkumbusha Sele kuhusu matakwa ya mke kama vile upole na maneno matamu. Msimamo wa Amri ni kuwa imani ni bora kuliko uhuru.Baada ya siku kadha kupita, Daktari anarudi nyumbani kwa Sele na kumkuta akiwa chumbani mwake.

Tunatarajia kumwona Sele akitibiwa lakini anaanza kumdadisi Daktari kwa maswali ambayo hayahusiani na ugonjwa wake. Kwa mfano, anataka maelezo kuhusu ni vipi mbili mara mbili inaweza kuwa nne na sio ishirini na mbili. Pia anataka kujua ni vipi hesabu ya kujumlisha na mara vinaweza kuwa kitu kimoja. Maswali mengine ya kudadisi ni kama vile refa anapocheza mchezo mpaka kati yake na yeye kama refa na uso-refa wake unaanza na kuishia wapi. Inakuwa ni vigumu kwa Daktari kuyatolea majibu maswali ya jinsi hii.

Siku chache baadaye, Zainabu anaamua kumtembelea Sele nyumbani kwake kwenda kumjulia hali. Sele anakiri kuwa hali yake ni timamu na wala haumwi popote. Pia haelewi ni kwa nini alikuwa anatembelewa mara kwa mara na madaktari nyumbani kwake kwani kila wakati ni mgonjwa humtafuta. Daktari na wala si kinyume chake. Ajabu zaidi ni kuwa, walikuwa wanaufanyia mwili wake biashara ili kujinufaisha wao

wenyewe. Kuhusu waganga wa kijijini anadai kuwa vifaa wanavyovitumia ni vichafu kiasi cha kumwambukiza mgonjwa kabla ya ugonjwa wenyewe. Anajaribu kuelezea jinsi madaktari wanavyokimbilia matabishi yake alipokuwa amelala. Jambo hili linamfanya asiwaamini madaktari wowote. Zainabu anamsihi Sele kuwa ni muhimu kuwa na imani na wala sio kutilia shaka katika kila jambo kwani anaweza kujikuta akiishuku hata imani yake mwenyewe, Jambo ambalo ni hatari.

Jioni moja nyumbani kwa Sele tunamkuta Bi.Rahma. Wanazungumzia kuhusu kazi ya malezi ya watoto na hasa kumhusu mwanawe Sele. Wanashindwa kuafikiana kuhusu uwezekano wa athari za dawa za kulevya au wa mtu kumfanyia mwanawe Sele uchawi. Bi.Rahma anampendekeza Jamila binti Hasani, aliyesomea udaktari aletwe kwani ndiye angeweza kuwaelezea vizuri kwa vile walikuwa wamesoma pamoja na Sele katika shule moja. Mara hiyo hiyo wanamtuma Aisha apeleke risala ya kumwomba aje pale nyumbani. Aisha anapoondoka nyumbani, Bi.Rahma na Zainabu wanaanza kushuku kuachishwa kwa kazi kama sababu ya kubadilika kwa Sele. Zainabu naye anakubaliana na Bi.Rahma kwani hata yeye aliyapitia hayo. Sababu kuu ya kuachishwa kazi ni kutokana na kapu la dunia na masharti yake. Bi Rahma anakiri ukweli kuwa "Dunia ni mseto wa mambo"

Nyumbani kwa Sele, Zainabu na Bi.Rahma walikuwa wameketi wakitazamatazama mlango wa kuingia katika chumba kingine cha ndani kama wale waliokuwa wanangojea kitu fulani. Mara mlango unafunguliwa na wote wanatazamana. Jamila ambaye anatoka ndani katika mavazi yake rasmi ya uuguzi, anawafichulia kuwa Sele anaugua kutokana na hali ijulikanayo kuwa'*Body Dysmorphic Disorder.*"Hii ni hali ya mtu kujikuta kutoipenda sehemu ya mwili wake na kuichukia. Muda wake mwingi mgonjwa hufanya

kila namna kuona kuwa hali hiyo imerekebishwa na kuwa anavyoitamani iwe. Jamila anawajulisha kuwa hali hii inaweza kudhibitiwa ila inahitaji muda. Kwanza yahitaji mgonjwa kuraiwa, aelewe na kukubali kuwa ni mgonjwa. Maelezo haya yanawaondolea Bi.Rahma na Zainabu wasiwasi na hatimaye wanamshukuru Jamila kwa kazi yake nzuri. Njiani akimsindikiza Jamila, anaonekana mwenye wasiwasi kuhusu hali ya mumewe Sele. Jamila anamuelezea kuwa kilichokuwa kinamsumbua Sele ni nafsi yake na wala si maumivu ya mwili. Jamila anampa moyo kwa kumpigia mfano wa kutokeza na kutua kwa mbalamwezi. Hata hali yake ya mhangaiko na shaka katika ndoa ina mwisho wake. Sele akiwa nyumbani kwake anaonekana akijinyoosha kitandani. Mara anarandaranda kidogo, mara anatazama darini, mara anainua kichwa chake na mara akiketi. Anapiga hatua moja moja na kutazama juu. Anabaki akijiulizauliza maswali pekee bila majibu. Anashindwa kutambua ugonjwa wa wake huku akidai kuwa yeye si mgonjwa. Anadai kuwa madaktari wamekuwa kama watungaji waigizaji na waelekezaji wa mchezo. Anahitimisha kwa kushindwa ni vipi angeliamini tiba yao kama madaktari hawazithamini fikra zake.

### 2.2.3 Tathmini ya ploti

Kuhusiana na ploti ya *Kijiba cha Moyo*, ni kwamba matukio yote ya kimsingi kama yalivyopangwa, yana sababu maalum. Licha ya matumizi ya mafumbo kama tulivyotanguliza kutaja hapo juu, matukio yanachangia katika muwala na mtiririko wa tamthilia kwa jumla. Sifa hii inaonyesha ufundi wa mwandishi-kwamba ameipanga kazi yake kwa makini ipasavyo. Mwandishi ametumia mgogoro katika viwango tofauti tofauti. Muhusika mkuu yuko katika mgogoro na mkewe na jamii yake kuhusu karibu kila suala. Mwandishi amemtumia muhusika mkuu Sele kudhihirisha jinsi uhusiano kati

ya mataifa mbalimbali ulivyozorota. Mataifa yaliyo na mamlaka na nguvu zaidi za kiutawala, yanawakandamiza zaidi yale yasiyo na uwezo huo. Sele anawakilisha mataifa yanayotawaliwa na kukandamizwa. Uhuru wake umethibitiwa na jamaa yake na hata madaktari wanaomtibu. Jamaa yake ndiyo inayoamini kuwa yeye ni mgonjwa hata kumletea madaktari kuja kumtibu nyumbani kwake huku yeye akiamini kuwa yu buheri wa afya kabisa.

Mgogoro mwingine ni kati ya mhusika mkuu na madaktari wanaomtibu. Kwa upande wao, wote wanajaribu kubainisha ugonjwa wa Sele kwa kuufanyia mwili wake majaribio. Sele anafikia kiwango cha kujidharau hata kuyachukia maumbile yake. Wajihi wake wa uso haumfai. Hata baada ya kuhakikishiwa kuwa sura yake bado ni nzuri anakubali kufanyiwa "plastic surgery"Hili ni dhihirisho kwamba baadhi ya watu katika mataifa yanayotawaliwa hawaoni fahari ya kuwa wananchi wa nchi hizo. Wanatamani kuwa na uraia wa mataifa yanayotawala. Madaktari wametumiwa na mwandishi kurejelea mataifa yenye nguvu za kiutawala. Sele anawakilisha wanyonge. Nia ya mataifa haya ni kujinufaisha kutokana na wanyonge. Wanalazimisha kufanya huduma bora wapate pesa. Watawala ni kama "papa" ambao wana uwezo wa kuwala "vidagaa" ambao ni wanyonge. "Bahari" ni ulimwengu tunamokaa na kuishi.

Uchangamano wa ploti na matumizi ya mbinu ya taharuki ndicho chanzo cha mvuto wa ploti yenyewe. Ujenzi wa taharuki kama vile kutoweka kwa Sele kutoka nyumbani, kimya chake, kucheleweshwa kwa matokeo ya daktari na vile vile chanzo cha kuugua kwake, vinastawisha na kuendeleza mvuto wa ploti.

Tunatarajia kuwa kati ya wale madaktari wawili pamoja na mganga mmoja wao angeweza kumtibu Sele. Inatokea kwamba hakuna hata mmoja kati yao anajiamini ila kila mmoja amekuja kumfanyia majaribio na kuipa familia matumaini kwa ajili ya kujinufaisha. Mwishoni mwa tamthilia Sele anabainisha mahali tatizo lilipo lakini hatupati suluhisho la tatizo hili. Tunatambua kuwa Sele haugui lakini kutokana na kujisemea kwake, ni namna uhuru wake ulivyothibitiwa. Yu jukwaani na wanaomthibiti wanaigiza mchezo uliotungwa na watawala wake. Anakuwa mwigizaji na wao waelekezi naye lazima aigize sehemu yake kama wanavyotaka wao. Aidha, matukio kwenye tamthilia hii ni mengi ikilinganishwa na *Chamchela*. Ni ithibati ya kukua kimawazo na muundo kwa mwandishi Arege.

### 2.2.4 Mchango Wa Msuko Katika *Mstahiki Meya*

Kulingana na mwaka wa uchapishaji (2011), *Mstahiki Meya* ndiyo tamthila ya tatu aliyoitunga mwandishi Arege. Ikilinganishwa na kazi zake za awali bila shaka hatuna budi kudhihirisha kuwa ni mojawapo ya kazi ambazo zimetia fora kabisa katika vigezo vya upimaji wa mwandishi anayeendeleza kipawa cha uandishi. Vile muhtasari wa ploti unavyoonyesha, matukio katika tamthilia hii yamepangwa kimantiki na yanafuatana kwa namna ambayo ni rahisi sana kuyafuatilia na kueleweka ikilinganishwa na *Kijiba cha Moyo.* Mkondo wa kwanza wa tamthilia unalenga kutudokezea matatizo wanayoyapitia wanaCheneo na kutupa suluhisho la matatizo hayo.Sifa hii ya ujenzi mzuri wa ploti kwa jumla inatokana na uzuaji wa taharuki pamoja na matumizi ya lugha iliyoshehenezwa ubunifu wa kisanaa. Katika utangulizi wa kazi hii, mwandishi Arege anatupa fununu juu ya mambo yanayosimuliwa humo.

*Mstahiki Meya* inachunguza uongozi wa Mstahiki Meya ambaye fauka ya kuendeleza

baraza kwa njia isiyofaa, anapotoshwa na washauri wake kuhusiana na maamuzi ya kimsingi na huduma za umma kwa jumla. Usimulizi wake ni wa kitashtiti. Uongozi wa Mstahiki Meya unafichua siri ya uovu uliokithiri katika mabaraza ya miji.

Matukio yanaanza pale zahanatini ambapo tunampata Daktari Siki akitingwa na mawazo kweli kweli. Ni kutokana na matatizo ambayo hayajui namna ya kuyatatua. Waridi msichana muuguzi anapoingia, wanaanza kuongea kuhusu idadi kubwa ya wagonjwa waliopo ilhali hakuna dawa zahanatini. Wakati huo anaingia mama mmoja na mtoto mgonjwa. Badala ya kumrudisha mgonjwa nyumbani kutokana na ukosefu wa madawa, Daktari anaamua mgonjwa alazwe ili angalau awe na matumaini kuwa atashughulikiwa. Waridi anaeleza kuwa madawa yaliyoagizwa kutoka nje yalikuwa njiani yakija lakini Daktari Siki anasema kuwa hizo ni porojo tu hasa za wanasiasa akiwemo Meya. Daktari anamwagiza Waridi amwandalie mgonjwa mchanganyiko wa sukari na chumvi ili kumlaza mgonjwa na matumaini. Tunaelewa kuwa hata kama madawa yangekuwepo kuna shida ya gharama kubwa za huduma hapo hospitalini.

Siku ya pili, Meya yuko nyumbani kwake anapata kiamsha kinywa. Baada ya Meya kumkemea Dida, mhudumu wa nyumbani, Meya Sosi anatembelewa na Daktari Siki. Siki anamweleza kuwa watu wana matatizo mengi yanayohitaji suluhisho. Matatizo yenyewe ni pamoja na njaa, kiu na maradhi tele katika jamii na watu waliomchagua Meya wanamlilia kutatua shida zao. Meya Sosi hataki kusikia mambo kama haya na badala yake anajitapa kwa kusema kuwa Baraza la Mji wa Cheneo lina ufanisi mkubwa sana unaohitaji kuigwa na wengine. Anamwona Siki kuwa mchochezi. Anamtuma Gedi mpambe wake amwambie Mhazili wahakikishe kuwa vyombo vya habari kote vinaimba

nyimbo za kizalendo kabla na baada ya kipindi maalum. Siki anapinga msimamo wa Meya. Anamwamrisha Gedi kumwondoa Siki nyumbani kwake na kumpa marufuku asirejee hapo tena. Meya anamwamrisha mhasiri wake kuandaa mkutano wa dharura na wanakamati wa baraza la madiwani wakati wa alasiri. Onyesho linalofuata linatokea afisini mwa Meya ambamo wanakutana wanakamati watatu wa Baraza la Mji wa Cheneo. Wao ni Diwani I ambaye ndiye kinara wa masuala ya usalama, Diwani II-kinara wa masuala ya uhusiano mwema na Diwaani III ambaye ni kinara wa masuala ya uchumi na kazi.

Meya anapoingia anawaambia kuwa hali si ya kawaida kwani baadhi ya madiwani wanawachochea watu dhidi ya baraza na kusema kuwa linashindwa kutekeleza majukumu yake. Meya anagusia kuwa hata Daktari Siki ni miongoni mwa wachochezi. Wakati huu Meya analalamikia kuwa maji aliyoletewa ya kunywa ni machafu kwani yana harufu mbaya lakini Gedi anamwambia kuwa si harufu ya maji bali ni ya uvundo wa uchafu ulioenea mjini. Baadaye Meya anamwambia kila diwani aseme mkakati wake kukabiliana na tatizo lililopo la uchochezi na miongoni mwao wanasema akiwemo Diwani I kuwa tayari vikosi vya usalama vipo ili kukabiliana na tatizo lolote ilhali Diwani II anatumia propaganda ya vyombo vya habari kuwatuliza watu ili kuamini kuwa hamasa za umma kuhusu matatizo yanayowakumba.

Diwani wa pili anaendelea kupendekeza kuwa madiwani katika mabaraza waendelee kupatiwa mamlaka zaidi. Meya anaamua kuwa ombi la kuondolea mzigo wa kutozwa kodi likubaliwe na kutimizwa.

Diwani III anapinga hoja hizi na kudai kuwa kuna matatizo ya ukosefu wa ajira kwa vijana waliohitimu na kutolipwa mishahara au kulipwa mishahara kama imechelewa.

Licha ya hayo,uamuzi unaotolewa unaunga mkono maoni ya Meya na wenzake wawili (Diwani I na Diwani II) yanapitishwa kwa vile ni wengi na hoja za Diwani III zinakataliwa kwa vile ni mmoja tu huku wakidai kuwa hiyo ni demokrasia.

Ni baada ya mwezi mmoja. Sosi yu ofisini akipanga mikakati ya kupokea mameya wageni kutoka nchi za nje. Anafikiria na kujivuna licha ya kuwa na bajeti ya gharama kubwa ya sherehe anayodhamiria kuwafanyia. Anaingia rafikiye Bili. Kwanza wanajadiliana kuhusu wanawe Meya wanaosomea ng'ambo ambao mkewe Meya ameenda kuwaona. Meya Sosi anaringia wingi wa fulusi anazomiliki kutokana na kuuza viwanja vya baraza alivyonyakua. Anagusia kisa cha mwanakandarasi aliyepewa zaburi ya miaka kadhaa na uongozi wa baraza uliopita. Meya anasema kuwa alisisitisa kandarasi hiyo na mwanakandarasi huyo amemshitaki. Bili anamshauri aache kesi iendelee mahakamani na uamuzi ukitolewa dhidi ya Baraza la Mji, Meya azichukue pesa za Baraza za Mji amlipe fungu fulani kutokana na pesa hizo. Yeye Meya hatapata hasara yoyote. Badala yake ana faida. Baraza la Mji ndilo litakalohasirika. Bili anamwambia Meya kuwa akipata amkumbuke. Wakati huu yanasikika makelele ya wafanyikazi wa baraza wanaogoma. Wanataka mishaara yao iongezwe, ilipwe kikamilifu, madawa yapelekwe hospitalini, Meya asikilize malalamiko yao n.k. Meya Sosi anaonya kuwa wataachishwa kazi wasipositisha mgomo. Anaita polisi kupambana na wagomaji. Mara hiyo, Bili anamshauri Meya atafute huduma za mhubiri.

Ni ofisini mwa Daktari Siki. Haya yanatokea wakati ule Bili anapokuwa afisini mwake. Waridi, mwenzake katika kazi ya zahanatini, anamwambia kuwa yeye katoka Baraza la Mji kwa sababu haoni namna watakavyowahudumia watu katika kituo hicho cha afya. Baadaye Tatu aliyekuwa amemtaarifu Siki kupitia kwa simu kuwa anakuja. Anawasili na Waridi anaondoka. Tatu, mwakilishi wa wafanyikazi wa Mji wa Cheneo anamwambia kuwa wamekubaliana na viongozi wengine na wafanyikazi kuwa waongee na Daktari Siki ambaye ni binamuye Meya ajaribu kuongea na Meya asikilize vilio vyao kuhusu hali yao ya maisha-yaani ukosefu wa madawa hospitalini, mishahara kuchelewa kulipwa, gharama kali za hospitalini n.k. Sele anajibu kuwa amejaribu kumshawishi Bw.Meya asaidie. Wanaamua kuwa kwa vile kuna mameya wageni watakaotembelea jiji hili, basi wafanyikazi watumie fursa hiyo (kwa kutumia migomo) kumshurutisha Meya afanye inavyotakikana.

Onyesho linalofuata linafanyika afisini mwa Meya. Anakutana na Mhubiri. Kwa uzandiki wake, Meya anajifanya kuwa msahilina. Ni katika kujifanya kuwa wamehemkwa na hisia za kidini kwa kutoa matamko ya kidini, wanavuta nadhari ya Gedi na askari huko nje wanadhani kuwa wagomaji wamewaingilia afisini. Askari wanaingia na kuamuru kila mtu alale chini kabla ya kutambua kosa lao.

Halafu baadaye askari na Gedi wanaondoka. Meya anamwahidi mhubiri wake awe anakuja kuombea Baraza la Mji mara moja kwa juma na kwamba, watagharamia safari zake licha ya kutoa shilingi laki moja kama sadaka kila mwezi. Ni siku ya pili alasiri. Bw.Kheri (Diwani III au Bwana Uchumi na Kazi) yuko kwake nyumbani ambako ametembelewa na Daktari kumwona Meya kuhusu suala la matatizo ya Baraza la Mji wa Cheneo. Siki anapomuuliza Bw.Kheri kwa nini madiwani wameshindwa kumshauri

Meya atende mambo inavyostahili, Bw.Kheri anasema kuwa yeye anamshauri ila Meya kalewa na mamlaka yanayomzuia kusikiliza ushauri. Pia, yeye Meya anazungukwa na washauri wapotovu wenye tamaa kubwa ya kujinufaisha wao wenyewe. Kikwazo kingine huwa ni kutowahusisha raia katika utatuzi wa matatizo ya uongozi.

Licha ya hayo, Bwana Kheri anasema kuwa hatakata tamaa bali atazidi kumshauri Meya na viongozi wengine wapate kuwa waadilifu na wenye kuwajibika. Anaongeza kuwa viongozi ni picha ya umma uliowachagua na kwa hivyo ni kama anawalaumu raia. Kwa kiasi fulani kwa uchaguzi wao mbaya na kuwahimiza kusaidia katika kusahihisha makosa yao nao wana hatia. Siku inayofuata, Bw.Kheri na Daktari Siki wanakutana kwake Bw.Kheri. Hapa ni afisini kwa Meya. Meya anamwambia Bw.Kheri (Diwani III) kuwa anataka madiwani waongezewe malipo yao mara moja. Ijapokuwa Bw.Kheri anasema kuwa wafanyikazi wamegoma wakitaka nyongeza ya mishahara na tayari mishahara ya madiwani ya mwezi huu yamekwisha kutayarishwa, Bw.Meya haridhiki. Anasema kuwa ukilinganisha na watu wengine na hivyo lazima wapate nyongeza. Nao wafanyikazi wakiendelea kugoma, wataachizwa kazi na watu wengine kuajiriwa mahali pao. Malalamiko ya Bw.Kheri ni kuwa tayari wafanyikazi wanagoma kwa sababu ya kutopata nyongeza ya mishahara. Mishahara ya madiwani ya mwezi huu tayari ilikuwa imekwisha andaliwa na kuna mameya wageni watakaotembelea jiji na yafaa wasipate jiji likiwa chafu kutokana na mgomo wa wafanyikazi. Zaidi ya hayo, Baraza la mji wa Cheneo lina matatizo makubwa ya kifedha.

Maoni ya Meya ni kuwa madiwani ni watu mashuhuri wasioweza kupuuzwa. Hivyo basi, wafanyikazi wakiendelea na mgomo watafutwa kazi na wengine waajiriwe. Anaonelea

kuwa, nuksi ya pesa katika baraza la mji litapata afueni kutokana na misaada ya wageni wanaokuja kutembelea jiji. Kwa vile Meya ni dikteta, Bw.Kheri anaishia kuridhia matakwa yake japo shingo upande.

Katika onyesho linalofuata, Meya yu ofisini mwake. Kuna maandamano ya wafanyikazi nje wakilalamikia kuwa wamenyanyaswa vya kutosha. Polisi wanawafyatulia risasi kwa ukatili mkubwa.

Meya anafurahia kitendo hicho. Mara anaingia Gedi anayetangaza kufika kwa Bili (rafikiye Meya) Diwani I na Diwani II wanafurahia kitendo cha polisi kuwashambulia waandamanaji kwa ukatili. Wanakubaliana kuwa propaganda ya vyombo vya habari itumiwe kuonyesha kuwa kuna utulivu wakati mameya wataingia ili sifa ya Baraza la Mji wa Cheneo isiharibiwe. Baadaye madiwani wanataka marupurupu kidogo na Meya anaposema kuwa hakuna pesa, Bili anapendekeza kuwa fimbo ya Meya (ambayo ni ishara ya mamlaka ya baraza la jiji) waiuze kisiri na wadai kuwa ilipotea wakati wa rabsha za wafanyikazi. Wanakubaliana na kuamua kuliweka siri jambo hilo.

Nyumbani kwa Meya, siku mbili baadaye Dida yu kazini akifagia huku akihoji namna jamii imejigawa kuwili. Wanaojiona watu na wasio watu ila ni viatu. Meya anajiona kuwa ni mtu; amewapeleka wanawe kusomea ng'ambo na raia wa kawaida ni viatu. Wanapata elimu iliyo duni hapa hapa nyumbani. Dida anafikiria haya na kutoa kicheko kikubwa. Chake ni kicheko cha dhihaka cha uongozi wa Meya mwajiri wake aliyechaguliwa na watu kuwaongoza lakini anawapoteza na kuwaua.

Siku moja kabla ya kuwasili kwa mameya wanaotarajiwa kuzuru baraza la mji wa Cheneo, Meya Sosi anakutana afisini mwake na wawakilishi wa wafanyikazi.

Wawakilishi hao wanamlaumu Meya na uongozi wake wa baraza kwa kutojali maslahi yao. Wanalalamikia kuihusu mishahara yao kuwa haiongezwi ilhali ya madiwani huongezwa mara kwa mara. Mishahara yao iko chini ilhali ya madiwani iko juu na huongezwa mara kwa mara. Jambo jingine kuihusu mishahara yao ni kuwa hailipwi kila mwezi. Ikiongezwa huwa ni nyongeza ndogo tu ilhali nyongeza ya madiwani ni kubwa. Wao hawana huduma nyingine ilhali viongozi wa baraza huletwa kazini na kupelekwa kwa magari nyumbani.

Wao huambiwa hakuna madawa hospitalini au huyalipia yanapokuwepo lakini madiwani huwa na bima ya afya.Isitoshe, watoto wao hufukuziwa karo shuleni ilhali wa madiwani hulipiwa karo. Aidha, wanafanya kazi bila vifaa kama vile glavu. Wanapenda washiriki katika vikao vya baraza la mji ili wawajulishe shida zao na kama utatuzi haupo kwa matatizo yao, mgomo uendelee. Naye Meya anasema kuwa tayari wafanyikazi wana ajira na wanalipwa, hivyo hakuna haja ya kulalamika. Wakiendelea na mgomo, watafutwa kazi na wengine waajiriwe. Anaendelea kudai kuwa baraza la mji wa Cheneo ni miongoni mwa yale yanayowalipa wafanyikazi vizuri. Kwa hivyo, katika kazi yoyote lazima kuwe na mwelekezi na mwelekezwa. Hivyo basi yafaa wafanyikazi wote wasubiri mpaka baada ya ziara ya mameya wageni barazani na kumalizia kuwa hakuna pesa za kuwalipa wafanyikazi.

Baada ya siku moja kupita tangu mkutano baina ya Meya na wawakilishi wa wafanyikazi, Meya yu afisini mwake kukutana na Diwani I na II. Wandani wake wanaongea kuhusu kuwasili kwa mameya wageni ilhali mji ni mchafu kweli kweli na wenye ghasia za mgomo unaoendelea. Wanapendekeza kuwa wawatangazie vijana wasiokuwa na kazi kuwapa kazi ya kunadhifisha mji. Hapa ni kama Meya anagutuka na

kujuta kuwa laiti angeufuata ushauri wa sahibuye mkubwa Bili ambaye haijulikani kwa sasa alipo. Wakati huu anaingia Gedi akihaha. Anapotulia, anasema kuwa kuna mgomo katika uwanja wa ndege na kwa hivyo, wageni waliotarajiwa hawaji na ni kama walihofia kupata ugonjwa wa kipindupindu kutokana na uchafu ulioenea na uhaba wa maji mjini. Meya sasa anamhitaji mhazili wake.

Anaambiwa kuwa hayupo na kaondoka na harejei kwa vile hakuna usafiri kwa ukosefu wa mafuta. Meya anasema kuwa hakuna namna nyingine ya kuyadhibiti mambo ila kwa kutumia nguvu za dola.

Wakati huu anaingia askari I na II ambao Meya na madiwani wanawafurahia wakidhani sadfa imewaleta kuwahudumia. Askari wanawaarifu kuwa safari iliyotarajiwa ya mameya wageni kuwasili ilikuwa imeahirishwa na wametumwa na makao makuu kuwakamata Meya na madiwani waende mbele kuelezea vizuri hali ya mambo. Meya anashtuka na kuanguka, madiwani wanaduwaa na wote wananaswa.

### 2.2.5 Tathmini Ya Ploti

Baada ya kuyaratibu matukio muhimu ya ploti kwa muhtasari, sasa tunaweza kuchunguza mafanikio na kasoro zake katika kuviumba vipengele vyake. Ploti ya tamthilia ambayo tunashughulikia inatokana moja kwa moja na tukio maalum-uongozi mbaya uliotawaliwa na tamaa ya Mstahiki Meya pamoja washauri na marafiki wake wakuu katika baraza lake la mawaziri. Kusahauliwa huku kwa wananchi na Mstahiki Meya kama kiongozi wao ni kama shina ambapo matukio yote mengine yanatokezea kama matawi. Hivi ni kusema kuwa hakuna tukio muhimu lisiloweza kuhusishwa, kwa njia moja au nyingine na tukio hili la kimsingi.

Mbinu hii ya kukuza na kuzua tukio la kimsingi na kuliambatisha na matukio mengine yote, imetumiwa vizuri na kufaulu kutimilika kifasihi kwa njia kadha wa kadha.Kwanza mbinu hii imeipa tamthilia hii mwelekeo madhubuti, ambapo msomaji hatatiziki kuoanisha matukio yote. Pili, tamthila hii imepata muala ambao unajitokeza waziwazi. Kwa jumla mbinu hii imechangia sana kuleta wiano wa kisanaa ambao ni muhimu sana katika muundo wa tamthilia yoyote ile. Kwa maoni yetu, ploti katika tamthilia hii imetimiza sheria hizi kwa kiwango kikubwa sana na hivyo basi kuwa ithibati ya kuendelea kukua kwa mwandishi Arege.

## 2.3 Hitimisho

Katika kijisehemu cha kwanza cha uhakiki wa *Chamchela*, tumejaribu kuyachagua matukio muhimu zaidi katika tamthilia na sababu za kutokea kwayo. Kufikia hapa tunaweza kujadili iwapo Timothy Arege alikuwa anapiga hatua yoyote katika kukua kwake pale ambapo uumbaji wa ploti unahusika. Jambo ambalo linabainika wazi katika mtazamo wa ploti ya *chamchela* ni kuwa kuna matukio machache ikilinganishwa na *Kijiba Cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Kipengele hiki kinachangia sana katika kuifanya tamthilia ya kwanza kuwa ya kuvutia zaidi kuliko ya pili. Matuko katika tamthilia hii yameoana vizuri na yanafuata mkondo madhubuti wa moja kwa moja wa kimantiki. Yote yana wiano mkubwa na mhusika mkuu Mayaka.

Aidha, *Chamchela* ikiwa ni ndiyo tamthilia ya kwanza kabisa aliyoitunga Arege, inakuwa ndiyo msingi wa kupimia hatua ya ukuaji wa kimuundo na mawazo katika tamthilia za baadaye. Itadhihirika pia kwamba, urefu wa kazi, mpangilio wa matukio pamoja na

mvuto wao ndivyo vitakavyokuwa vigezo vya kupimia kukua kwa Arege kulingana na kipengele hiki.

Kuhusiana na ploti ya *Kijiba cha Moyo*, ni kwamba matukio yote ya kimsingi kama yalivyopangwa, yana sababu maalum. Licha ya matumizi ya mafumbo kama tulivyotanguliza kutaja, matukio yanachangia katika muwala na mtiririko wa tamthilia kwa jumla. Sifa hii inaonyesha ufundi wa mwandishi-kwamba ameipanga kazi yake kwa makini ipasavyo.

*Kijiba cha Moyo* ni tamthilia yenye msuko changamano. Uchangamano wa msuko huu umejengwa kwa kukuza mgogoro wa kibinafsi kupitia kwa mhusika Sele. Mtunzi amebainisha migogoro inayoyakumba mataifa mbalibali kupitia kwa Sele. Aidha, vijiba vya moyo vya mataifa mbalimbali vimewasilishwa kama vikwazo vya kutatua matatizo ya utawala mbaya kutokana na mataifa yenye nguvu.*Mstahiki Meya* ndiyo tamthila ya tatu aliyoitunga mwandishi Arege. Ikilinganishwa na kazi zake za awali bila shaka hatuna budi kudhihirisha kuwa ni mojawapo ya kazi ambazo zimetia fora kabisa katika vigezo vya upimaji wa mwandishi anayeendeleza kipawa cha uandishi. Vile muhtasari wa ploti unavyoonyesha, matukio katika tamthilia hii yamepangwa kimantiki na yanafuatana kwa namna ambayo ni rahisi sana kuyafuatilia na kueleweka ikilinganishwa na *Kijiba* cha *Moyo*. Mkondo wa kwanza wa tamthilia unalenga kutudokezea matatizo wanayoyapitia wanaCheneo na kutupa suluhisho la matatizo hayo. Sifa hii ya ujenzi mzuri wa ploti kwa jumla inatokana na uzuaji wa taharuki pamoja na matumizi ya lugha iliyoshehenezwa ubunifu wa kisanaa.

# SURA YA TATU

# MCHANGO WA WAHUSIKA KATIKA KUENDELEZA DHAMIRA NA MAUDHUI

## 3.1 Utangulizi

Wahusika ni kipengele mojawapo cha muundo ambacho ni muhimu katika uandishi wa tamthilia. Wahusika ni viumbe wa kisanii ambao hupewa uhai na mwandishi ili kuikuza dhamira na maudhui ya kazi yake. Mohamed (1995:62) anaeleza kuwa wahusika wa tamthilia kwa upande mmoja ni vivuli vya maandishi ya tamthilia yenyewe na kwa upande mwingine (katika hali ya utendaji) ni watu bayana wenye mashiko ya kimwili na roho.

Naye Wamitila (2003:211) anasema kuwa wahusika tunaokumbana nao katika tamthilia wanahusiana na tunaowaona katika riwaya. Hata hivyo zipo tofauti lakini ni ndogo sana. Kwa mfano tamthilia haina msimulizi anayeweza kupenya akili ya wahusika na kuyaeleza mawazo yao.

Waihiga na Kamau (2012) wanasema kuwa, katika kazi yoyote ya fasihi mwandishi hutumia wahusika kwa njia mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe alionao. Mtunzi "huongea" na hadhira yake kupitia kwa wahusika aliowaumba. Wanaendelea kusema kuwa mtunzi haongei kama anavyofanya mhubiri kanisani au kadhi msikitini au mhadhiri chuoni, bali huwatumia wahusika wake kupitisha yaliyo moyoni mwake kwa wasomaji, watazamaji au wasikilizaji wa kazi yake. Kwa njia hii, hadhira hupata ujumbe wa mwandishi kwa kuyachunguza yale ya wahusika wayasemayo, wayatendayo,waonekanavyo, wasemayo na kila wakati wahusika hawa huwakilisha mtu

au kundi la watu katika jamii.Ni bayana kwamba katika tamthilia za Kiswahili wahusika wengi huwa ni binadamu lakini kuna baadhi ya maandishi yanayotumia viumbe wengine kama wanyama na ndege. Kwa upande mwingine, maudhui ni yaliyomo au masuala makuu ambayo mwandishi huwasilisha katika kazi yake. Maudhui katika tamthilia huwasilishwa na mwanatamthilia kupitia kwa dayolojia. Mtunzi huwa na jukumu la kukuza mazungumzo au usemi wa wahusika wake kwa kuhakikisha kwamba mazungumzo hayo yanachangia katika kuwasilisha maudhui yake. Katika tamthilia za Arege, mwandishi amewasilisha maudhui mbalimbali kupitia kwa mazungumzo ya wahusika wake.

Tutaangazia baadhi ya maudhui yaliyowasilishwa na waandishi.Katika sehemu hii, tumejadili namna ambavyo Timothy Arege amewaumba wahusika na jinsi ambavyo maudhui mbalimbali yamekuzwa na kuendelezwa na wahusika mbalimbali. Ni kutokana na maudhui hayo ambapo dhamira ya mwandishi hujitokeza. Katika kufanya hivyo, tunatumai kwamba tutaweza kubainisha hatua ya kukua aliyoipiga katika kushughulikia kipengele hiki mkabala na kazi zake za *Chamchela*, *Kijiba Cha Moyo* na *Mstahiki Meya.*

Haiwezekani kujadili wahusika bila kujadili maudhui wakati huo huo. Hii ni kwa sababu mwandishi huyu huwatumia kama makaragosi wa kuwasilisha mahubiri yake. Hivi ni kusema, dhamira kuu ya mwandishi huwa ni kuonyesha sifa na tabia anazopaswa kuwa nazo mwanadamu yeyote aliyekamilika.

Yaani vielelezo ambavyo vinafaa kuigwa na binadamu. Hata ingawa Arege amefaulu katika kipengele hiki kwa kuyashughulikia maudhui mbalimbali katika kazi zake, urudiaji wa maudhui ya umuhimu wa uwajibikaji wa viongozi kuanzia jamii hadi wa

kitaifa unajitokeza; jambo ambalo kwa kiasi fulani linaathiri mada yetu ya utafiti. Tutatanguliza na *Chamchela* katika kushughulikia kipengele hiki.

### 3.2 Mchango Wa Wahusika Katika Kuendeleza Dhamira Na Maudhui Katika Chamchela

Mhusika mkuu katika *Chamchela* ni Mayaka. Kupitia mhusika huyu mwandishi anawasilisha msimamo ambao kwa maoni yake vijana wanapaswa kuwa nao juu ya masuala ya ndoa, mapenzi na malezi. Mayaka amesawiriwa kama mhusika mkuu.Yeye ni kielelezo cha matatizo ya vijana katika jamii ya sasa. Wahusika wengine ni wajenzi wa mhusika mkuu na wana umuhimu katika ukuaji wa muundo na mawazo tamthiliani. Wao ni pamoja na Rosa (Mamake Mayaka ) Atisa (Kakake Mayaka) Mbiki (Ndugu wa kike wa Mayaka) Sure (Ami wake Mayaka) Bisase (Mpenziwe Mayaka ambaye ni mama wa miaka sitini na tano), Lema(Mjukuu wake Bisase), Sera (Bintiye Bisase na mamake Lema) Rukia na Kofa (Vijana wenye shaada) Abaya na Kobia (Wazee wa kijiji) Mlinzi I na II wa nyumbani kwa Bisase.

Pia kuna wateja wa I na II, Mhudumu wa pale hotelini na Nesi. Arege amemtumia mhusika mkuu Mayaka kuendeleza mawazo yake kuliko alivyowatumia wahusika wengine. Kwa sababu hii, katika uchunguzi wetu wa namna wahusika wamesawiriwa, tutamtilia mkazo zaidi mhusika Mayaka. Kwa kufanya hivyo twatarajia kwamba, tutaweza kubainisha iwapo Arege amepiga hatua yoyote ya kukua katika ujenzi wa wahusika tukilinganisha kazi hii na kazi zingine tutakazozihakiki.

Kuhusu maudhui ya ndoa na mapenzi, Arege ameangazia matarajio ya jamii na masharti

yanayohitajika kutimizwa kuhusiana na masuala hayo. Ni kupitia kwa muktadha huu wa kimaudhui ambapo tunamwona Sure akimtaka Atisa aelekee kumtafuta nduguye Mayaka ili aje kuwahakikishia kuhusu msimamo wake kuhusu mapenzi na ajuza Bisase. Uamuzi anaoufikia Mayaka ni kinyume na matakwa na matarajio ya jamii. Kulingana na ami yake Sure, huo ni kuiga uzungu.

> **Sure:**........ ulimwengu!ulimwengu hiki ni kinyume
> ....labda uzunguni....uzungu unatumeza kwa pupa (Ukurasa 1).

Hapa tunadokezewa wazi kuwa suala la umri ndicho kikwazo kikuu katika uhusiano kati ya Mayaka na Bisase ambaye anamzidi pakubwa kwa umri. Mayaka ni kijana wa umri wa miaka ishirini na sita akilinganishwa na ajuza Bisase mwenye umri wa miaka sitini na mitano. Katika ukurasa 9, jambo hili limekuwa chungu kwa Rosa (Mamake Mayaka) ambaye hata anashindwa kuelewa ni vipi mtu ambaye anamshinda umri atamwita mama-mkwe naye kamridhie kuwa mkaza mwana. Sure anapigana kwa jino na ukucha dhidi ya jambo hili ili kuhakikisha kuwa jamii yao kwa jumla imeondolewa soni na aibu ya kuchekwachekwa pembeni.

Kuna upinzani mkali kuhusu suala hili. Kulingana na Atisa, ndoa ni uamuzi wa hiari na la kibinafsi wala si suala la kijamii ambalo halifai kuingiliwa na mtu yeyote. Baadaye, Atisa anakuja kuona kuwa uamuzi wa nduguye Mayaka ni kinyume na matarajio ya jamii. Kwa Atisa, nduguye ameolewa na mama Bisase na wala si yeye amemwoa.

Umasikini ni maudhui mengine ambayo yanajitokeza katika tamthilia hii. Mayaka kupitia kwa kumbukumbu zake (ukrasa75), anatufichulia wazi kuwa umasikini ndio umechangia pakubwa kwa Mayaka kuwa katika hali waliyonayo kwa sasa. Babake Mayaka hakuwajibika kwani kwa wakati mwingi alikuwa nchini Tanzania akipasua mbao. Pesa

alizopata hawakuziona ila baadaye alipoletwa nyumbani karibu anachungulia kaburini. Pengine mapato aliyoyapata yalikuwa ni madogo na ambayo hayangetoshea kuhikimu familia. Yawezekana pia kwa sababu ya umasikini mkubwa ilikuwa ni njia moja ya kuyakwepa majukumu muhimu ya kimsingi. Hali hii ya umasikini nyumbani kwao Mayaka ndiyo inayomfanya kuhamia kwa Bi.Kizee Bisase. Licha ya umri wake mkubwa, ana mali ya kutosha ya kujikimu na kuwakimu wengine kama vile mpenziwe Mayaka, mjukuu wake Lema na kuwalipa mishahara walinzi wake. Mayaka anakiri kuwa Bisase amekuwa mfadhili wake mkubwa wakati kidau chake cha maisha kilitishiwa na mawimbi (Ukrasa 39). Katika muktadha huu mawimbi ni hali ngumu ya umaskini wanayoipitia wahusika kama vile Mayaka anayemwona Bisase kama mwokozi wake.

Wanaume wengi wamesawiriwa kama viumbe ambao hawawajibiki katika malezi ya familia zao. Babake Mayaka ni mfano wa kwanza mkuu. Sela ni bintiye Lema tena ni mtoto wa shule. Nyanyake Bisase, anamtizimia kila mahitaji muhimu. Anasomea shule nzuri, anakula na kuvaa vizuri lakini kila siku anabaki akichekwa darasani anaposhindwa kumtambua babake mzazi ndiye nani na kazi wanazozifanya wazazi wake.

> **Sela**:wakati kila mtu anatoa maelezo kuhusu kazi wanazozifanya wazazi wao, mimi simjui babangu ..... (Ukurasa15).

Licha ya hayo yote, Bisase anajitahidi kuona mjukuu wake hakosi mahitaji muhimu ya kimsingi kama vile elimu, mavazi na malezi bora. Licha ya kutowajibika huko kwa baadhi ya wanaume katika kuzikimu familia zao, baadhi ya wahusikwa kike wamedhihirisha wanaweza kutekeleza jukumu hili kwa hali ya juu. Rosa (mamake Mayaka) ni mmojawapo. Mbali na kutorokwa na mumewe anahakikisha kuwa anafanya kila awezalo kuhikimu familia yake. Anampigania mwanawe Mayaka apate mwelekeo

mzuri maishani. Bisase anahakikisha kuwa mjukuu wake hakosi mahitaji muhimu ya kimsingi. Hata ingawa wanawake hawa wanaonekana kuonyesha uwajibikaji mkuu. Baadhi yao ni watovu wa heshima kama vile Bisase ambaye anawakosea vijana wadogoheshima kama vile Mayaka jambo ambalo ni kinyume na matarajio ya jamii. Wahusika wa kiume ambao wanaonyesha kuwajibika ni Sure na Mayaka ambao wanafanya kila wawezalo kumtafuta Mayaka aliye mjini na kumsihi aubadilishe msimamo wake kuhusu suala la ndoa ili kuhakikisha kuwa familia yao imeondolewa soni na mamake karejelea hali ya kawaida hata kama ni kubidiwamdanganye ilimruradi apate kupona.

Uchumi mbaya ndicho chanzo cha migogoro mingi kati ya wahusika wengi katika jamii ya wanaChamchela. Mara ya kwanza katika ukrasa30 tunapokutana na Rukia na Kofa barabarani, wanalalamikia kuhusu uchumi. Hawa ni wasomi wenye shahada za digrii lakini vibarua wanavyofanya ni vya vichungu jiko tu. Mahali wanapoishi ni '*servants quarters.*' Wao kama vijana, wanatoa mchango mkubwa kulijenga taifa ambalo haliwajengi ila linawatupa na kuwaacha ganda tupu. Wengi wao wanatumia madawa ya kulevya kutokana na hali ngumu ya maisha na uchumi uliozoroteka. Teknolojia pia ina mchango wake mkubwa katika mabadiliko ya vijana wengi. Uamuzi wa Mayaka wa kuishi na Bisase ni kutokana na uchumi mbaya. Babake Mayaka kutorokea mjini Tanzania ni kwa sababu ya uchumi mbaya. Wanaume wengi hawataki kuwajibikia watoto waliowazaa nje na ndani ya ndoa kwa sababu ya uchumi mbaya.

Uchambuzi wa wahusika hawa na mchango wao kuhusu uendelezaji wa maudhui na dhamira ndio msingi na kigezo kikuu katika kazi za mwanzo za Arege ambazo zitakuwa zikitumika kama kigezo cha kupimia ikiwa Arege alikuwa anakipiga hatua yoyote

kuhusu masuala ya wahusika, maudhui na dhamira katika tamthilia nyingine za *Kijiba Cha Moyo* na *Mstahiki Meya* mtawalia.

### 3.3 Mchango Wa Wahusika Katika Kuendeleza Dhamira Na Maudhui Katika *Kijiba Cha Moyo*

Wahusika katika *Kijiba cha Moyo* ni wachache ikilinganishwa na wale wa *Chamchela*. Hili ni badiliko mojawapo katika kipengele hiki cha kupimia ukuaji wa muundo na mawazo. Ni kupitia kwa kupungua huku kwa wahusika ambapo tunapata kuwa hata katika suala la maudhui nayo si mengi ikilinganishwa na *Chamchela*. Hii ni kwa sababu wahusika ndio huchangia katika ujenzi wa maudhui (mawazo) katika kazi yoyote ile ya kifasihi. Kila muhusika huwa na ujumbe fulani anaowasilisha katika sanaa. Ndiposa kwa maoni yetu, kupunguka kwa wahusika ndiko kupunguka kwa maudhui.

Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* ni tamthilia ambayo imewasilisha sifa za wahusika kwa njia kadha wa kadha. Upambanuzi wetu umetoa mifano mwafaka kwa kunukuu baadhi ya mazungumzo kati ya wahusika kutoka katika tamthilia hii.

#### 3.3.1 Wahusika na Nafasi Zao

Wahusika katika *kijiba cha moyo* ni pamoja na Sele (Mumewe Aisha aliye na umri wa miaka 30), Aisha (Mkewe Sele mwenye umri wa miaka 25), Zainabu (Mamake Sele), Musa (Babake Sele), Amri (Babuye Sele) Bi.Rahma (Shangaziye Zainabu), Daktari (Tabibu wa Sele) na Jamila (Kijana muuguzi wa kijijini mwao Sele). Kama ilivyo katika *Chamchela*, hatuwezi kuzungumzia wahusika bila ya kuyashughulikia maudhui kwa wakati mmoja. Hii ni kwa sababu wahusika ndio hutumika kuwasilisha ujumbe muhimu katika kazi ya sanaa.

Sele ni mhusika mkuu ambaye ana nafasi kubwa katika kazi hii. Kazi nzima tamthiliani inamzunguka yeye. Mhusika huyu ana kijiba cha moyo yaani matatizo ya moyoni yanayomgadhabisha na hata kumkinai. Hali hii inafanya familia yao kukosa utulivu. Mwandishi amemtumia mhusika huyu kuonyesha matatizo yanayokumba mataifa mbalimbali na hata kuvuruga uhusiano baina yao. Tangu mwanzo kabisa hadi mwisho wa tamthilia tunakutana naye akionekana mwenye mawazo pevu na anayewazia mambo tofauti na wahusika wengine. Anakiri kuwa haumwi wala kuhisi maumivu yoyote.

Mkewe Aisha anajaribu kwa kila njia kumwondolea mumewe hali hii lakini hafaulu. Haya ni pamoja na kuzuru baharini kuogelea na kucheza muziki aupendao. Katika ukrasa9, Aisha ananukuliwa akimdokezea mumewe "ufukuze upweke bwana kwa kucheza." Hali hii ya upweke imekuwa tishio si kwa mkewe tu bali kwa jamii nzima. Bi Rahma anapomtembelea Sele nyumbani kwake, anamkuta katika hali ya mawazo tele lakini anapoulizwa anakiri kuwa yeye ni mzima kama kigongo. "Mzima mimi." "Mzima kama kigongo buheri wa afya kabisa." Baadaye anapotembelewa na mamake Zainabu, anamkuta Sele akiketi ukumbini akishika tama akiwa katika hali ya kujiinamia. Hata Zainabu katika Ukurasa 40, Anadadisi hii basi ndio hali yake, huwa kama aliyechanganyikiwa."

Sele ni mkereketwa lakini mwoga. Anakumbuka safari yao na mkewe kwenda baharini kuogelea. Mambo yanayomchukiza anapopiga mbizi ni mapambano dhidi ya mawimbi ya bahari. Anakiri kuwa anaogopa mambo mengi ya bahari.

> **Sele**: Bahari ina mengi naiogopa.
> Naiambaa"(*Ukurasa16*).

Anaogopa kuwa huenda akaangamia baharini kwa kupigwa dafrao na maji. Pia Sele anakereketwa na jinsi vidagaa vinavyohangaishwa na papa baharini. Kunguruma kwa papa huvitia vidagaa katika hali ya kiwewe. Kulingana na Sele vidagaa ni wanyonge na papa ni wenye nguvu. Huku kuangamizwa kwa vidagaa ni unyanyaswaji wa wanyonge kutokana na wenye nguvu. Anapozungumzia kuhusu papa na vidagaa anaashiria namna nchi zenye nguvu za kiutawala zinavyokandamiza nchi zizizo na nguvu.

Anaona uhuru wa wasio na nguvu za kiutawala umethibitiwa.Nchi hizi zinafanyiwa maamuzi na wenye nguvu hizi za kiutawala. Sele ni mhusika aliyekuzwa kuonyesha namna uhuru ulivyothibiwa. Anafanyiwa uamuzi na watu wa familia yake, kiasi kwamba wanamwona kwamba yeye ni mgonjwa ilhali yeye mwenyewe anajihisi kuwa mzima kabisa. Isitoshe, wanamfanya hata uamuzi wa chakula atakachokula. Anayadhihirisha haya akiwa hospitalini. Anasema:

> **Sele**: Nilijua tangu hapo kuwa sina tatizo.Sikulihisi. Hamkutaka kunisikiliza.Mnataka kwamba mtake wenyewe ndo
> Iwe sina tatizo. Njia rahisi kunitawala fikra na mwili na wewe hupendi. Nikuulize zaidi nikidadisi upembuzi . Wangu kunihusu. Daktari ni hata zaidi......(Ukurasa 62)

Muziki anaowekewa aucheze ili kuufukuzilia mbali upweke unamkereketa. Anakereketwa na baadhi ya miziki kwa mfano ule unaomfanya airushe mikono yake juu. Anadai kuwa ule ni utumwa. Inamfanya kuwa mtumwa wa jambo hilo. Sele anapotoka hospitalini anaelekea kwa babuye Amiri badala ya kwenda kwake nyumbani. Anadai kuwa maswali ya Daktari yalikuwa yanamchukiza na kumkera.

Anakiri kuwa nyumbani huulizwa maswali ambayo yanamsumbua.

> **Sele**:Mimi nimetoka pale hospitalini. Daktari amenichosha nikaona nitoke niende nyumbani. Lakini nilijua wananisumbua kwa maswali. Wananifanya nijihisi mfungwa" (Ukurasa 66).

Sele ni mdadisi na mpinzani hodari wa mambo. Kwake Sele anapinga kila jambo kuanzia mwanzo hadi mwisho wa tamthilia. Akiwa hospitalini anamuuliza daktari maswali mengi ili kupata ushawishi wa kutosha kabla ya kufanya uamuzi wa kufanyiwa '*Plastic Surgery.*" Badala ya Daktari kumhoji, yeye ndiye anayemhoji Daktari. Maswali haya yanamuudhi na kumchosha Daktari lakini Sele hakati tamaa.

> **Sele**: Naelewa lakini nipe nafasi kuuliza swali kabla ya kuanza
> **Daktari:**(*Hana stahamala tena*) sitaki maswali yako mengi. Siku ile nyingine umeniuliza maswali mengYa kunipotezea muda. Mimi ndiye daktari; nakuuliza maswali wajibu,(*kimya*) Wewe ni wa kujibu. Sasa wewe. Unataka kunihoji na wewe ndiye muhojiwa.
> **Sele**: (*kwa upole*) Mara hii si mengi Daktari (Ukurasa5)

Sele anauliza maswali mengi kabla ya kufanya uamuzi wowote kwa sababu anataka kutegua kitendawili itakachotuliza moyo wake. Si jambo rahisi kufanya uamuzi wa kubadili maumbilie, Lakini tatizo kuu ni kwa nini anataka kubadili sura yake? Ni baadhi ya maswali yanayomsumbua Sele. Dhihirisho kwamba kuna baadhi ya watu katika mataifa yanayotawaliwa ambao hawajithamini kama watu wa mataifa yao bali wanawaonea fahari mataifa yaliyo na nguvu za kiutawala na hata kuwa na tamaa ya kuwa watu wa mataifa hayo. Anaonekana akipinga kila kitu na hali. Hata Zainabu anakiri kuwa humwezi Sele kwa kusema. Kwa pande mwingine Daktari ni mtu mwenye pupa wa kutenda mambo. Hataki kumpa Sele muda wa kuuliza maswali kwa sababu anadai kwamba anapasa kushughulikia wagonjwa wengine. Anasema:

> **Daktari:** Maswali tu ni ya kupoteza wakati.Nina wagonjwa wenye kuhitaji huduma kama unavyohitaji wewe. Sitaki Kupoteza muda hapa *"Time is money bwana!"***Sele:** Nafahamu Daktari...
> **Daktari:** (Anamkaribia Sele. Anaonyesha ukali kiasi)Kama wafahamu usingeuliza unayouliza.(Ukurasa 53)

Madaktari wana lengo na nia sawa. Wanajishughulisha na ugonjwa wa Sele na kila mmoja wao anataka kutatua tatizo la Sele ili kutuliza familia yake. Sifa zao ni pamoja na ubinafsi. Wanaenda wote nyumbani kwa Sele kumtibu na wote wanataka kumhudumia Sele kwa wakati mmoja.

> **Sele:** Yule daktari mfupi alikuwa hasemi sana, Hali wasiwasi zaidi. Mwisho niliona kama kuna jambo ambalo halikukumfurahisha. Yule daktari mwenzake kuwa karibu naye. (Ukurasa 80)

Ni wanafiki wasio na uhakika kuhusu tatizo la Sele. Wanabahatisha tu na wanatarajia hata jawabu kutoka kwa Sele, Wanampa dawa ambazo hawana uhakika zinatibu nini na hawana uhakika kama Sele ni mgonjwa.

> **Sele:**Basi wale madaktari wakawa wananizungukazunguka mara wanashauriana kuhusu kitu fulani na kuniashiria halafu kwa kauli moja wote wakasema, "Bado amelala" wakawa wananipekuapekua kila mahali kwanza nguo, halafu mwili na nywele. Waliposhindwa kupata chochote. Nikaona wamechukua vyembe vyao. Niliogopa. Wazo likanijia la kuwatapikia. Moyo wangu. Pale pale nikautapika.
> Wote wakaukimbilia. Nilitazama nikaona. Unafanana na kidagaaa cheusi. Wakakitoa huku. Wakikipigania. Nikajua hawakuja kunitibu mwili wangu. Bali kuutwaa moyo wangu. Nikapatwa na huzuni(Ukurasa 80)

Madaktari hawa wametumiwa na mwandishi kuonyesha namna mataifa yenye nguvu za utawala yanavyong'ang'ania kuzitawala nchi hasa za kiafrika kwa manufaa yao wenyewe lakini kwa lengo la kuendeleza uchumi wa nchi zao. Aisha ni mkewe Sele anayemjali mumewe. Anajali maslahi ya Sele ndiposa anamjulia hali kwa sababu anamwona mumewe kabadilika. Pia, anajaribu kumfurahisha kwa kuzungumza naye, kucheza densi naye ili asiwe na mawazo mengi. Baada ya mumewe kuondoka nyumbani bila kumjulisha yeyote anakoenda, Aisha anafanya kila juhudi za kumtafuta. Ni mdadisi kwa vile anafanya uchunguzi kuhusu jambo aliloambiwa na Sele ili apate kujua maana yake. Anapekuapekua vitabu kwa matumaini ya kutegua vitendawili. Anasema:

**Aisha:** Sivyo bibi (*kimya*) Baada ya kusema na Sele. Kuna jambo alilosema na mimi nikahisi. Kama nimelisikia au kulisoma mahali. Ila sikuwa na hakika. Ninaona kuwa nikiliachilia litanichenga na kunitoka. Akilini maana ninahisi kama ninayechezewa. Na mimi fikra zikanielekezea katika. Maandishi fulani ambayo sikumbuki vizuri. Kama yalikuwa kitabu au kitumeme. Ndiyo sababu ya kunifanya nije moja kwa moja. Mpaka hapa. Samahani sana (*kimya*) (Ukurasa19)

Wahusika wa kike akiwemo Aisha, Bi.Rahma na Zainabu wana sifa bia. Wao ni wanawake wanaotekeleza majukumu yao ya kinyumbani kama wanawake. Zainabu anajishughulisha na kuandalilia familia yake chakula. Bi.Rahma naye anawapa mawaidha namna ya kukiandaa chakula na chakula ambacho wanaweza kumwandalia Sele. Hawa ni wahusika wenye kujali familia zao. Wote wanajishughulisha na namna ya kusaidia Sele. Bi.Rahma anamtembelea Sele nyumbani kwake ili kusikia kutoka kwake jambo linalomsumbua.

Mahangaiko na kuchanganyikiwa ni baadhi ya maudhui ambayo yametamalaki katika tamthilia hii ya *Kijiba cha Moyo*. Ndoa ya Aisha na Sele haina utulivu. Familia ya Sele na Aisha ni vile vile. Hata hao madaktari wamechanganyikiwa kuhusu ugonjwa wa Sele. Ni kama wanabahatisha tu. Haya ni kutokana na masimulizi ya Sele kuhusu jinsi walivyoyakimbilia matapishi yake alipokuwa pale hospitalini kwa lengo la kubuni chanzo cha maradhi yake. Hili ni funzo kuwa amani ndicho chanzo cha utulivu wa ndoa yoyote ile. Mawasiliano pia ni muhimu katika ndoa. Kuamua kunyamaza sana kama vile Sele anavyofanya kunaashiria hali ya wasiwasi katika ndoa. Sele anapotoka hospitalini bila kuwasiliana na familia yake, kunasababisha wasiwasi mkuu katika familia nzima kwani hawalali kwa kumtafuta hadi wanapomkuta Sele kwa babuye.

### 3.4 Mchango wa Wahusika katika Kuendeleza Dhamira Na Maudhui Katika *Mstahiki Meya*

Idadi ya wahusika katika tamthilia hii ni kubwa ikilinganishwa na ile ya *Kijiba cha Moyo* na *Chamchela*. Maudhui anayoyawasilisha Arege ni mengi kuliko kazi zake mbili za awali. Jambo hili ni ishara thabiti ya ukuaji wa mwandishi tukirejelea kipengele hiki cha uhusika, maudhui na dhamira.

Mhusika mkuu katika *Mstahiki Meya* ni Meya Sosi ambaye pia ndiye mkuu wa Baraza la Mji wa Cheneo. Wahusika wengine ni Diwani III (Bw.Kheri), madiwani II na I, Siki (Daktari wa Mji wa Cheneo) Bili (Rafikiye mkubwa wa Meya Sosi), Tatu (Mwakilishi wa wafanyikazi katika Baraza la Mji wa Cheneo) Wahusika wadogo au wajenzi katika tamthilia hii ni kama vile Gedi (mpambe wake Meya) Waridi (nesi) Mama (Mfanyikazi wa baraza la mji wa Cheneo) Beka na Medi (Wawakilishi wa wafanyikazi) polisi na sauti.

Katika kipengele hiki cha uchambuzi pia tumeamua kujumuisha maudhui, dhamira na wahusika kwa wakati mmoja kwani yote matatu yanategemeana. Timothy Arege, ameangazia maudhui mbalimbali. Baadhi ya maudhui makuu ni kama vile utawala mbaya, utabaka, ufisadi, unyanyasaji, utegemezi uliokithiri, ukosefu wa ajira, uongo, ujinga na ukosefi wa uadilifu.

Utawala au uongozi mbaya tamthiliani unaendeshwa na Mstahiki Meya pamoja na washirika wake. Diwani I na Diwani II. Mji wa Cheneo una matatizo mengi kwa sababu ya utawala mbaya unaodhihirika kwa njia mbalimbali. Kwanza, zahanati katika Mji wa Cheneo haina dawa. Utawala wa Meya Sosi unawashauri wahudumu wake

kuwafahamisha wagonjwa wangoje kwa muda mrefu ndipo wapate kuhudumiwa.(Ukurasa 2)

Wafanyikazi wa nyumbani kwa Meya hawashughulikiwi mahitaji yao vilivyo na Meya. Mama mmoja ameungama kuwa wakati mwingi wao hula chakula kilichopimiwa mbwa huko kwa Meya. Haya yanadhihirika pale zahanatini mama anapomleta mtoto mgonjwa anayeendesha kutokana na kula maharagwe yaliyolala nyumbani kwa Meya.

Kupanda kwa bei ya bidhaa muhimu kunashuhudiwa kila kunapokucha. katika ukurasa 5, mama mwenye mtoto mgonjwa anadai kuwa ni vigumu kwao kupata makaa kwani yamepanda bei. Pia anaongeza kuwa bei ya mafuta ya taa nayo inapanda kila uchao. Meya anaelezwa na Beka kuwa kuna mfumko wa bei unaosababisha kupanda kwa gharama ya maisha.

Ni vigumu kuwatawala watu wenye njaa. Meya anaelezwa na Siki kuwa watu wana njaa na kiu. Anatoa mfano wa kitoto kinachofia mikononi mwake kwa sababu ya njaa na ugonjwa. Anasisitiza kuwa watu wanakufa kwa kula mizizi na matunda mwitu. Katika (Ukurasa 19), Gedi anaeleza Meya kuwa harufu inayomfikia ni ya taka zinazolundikana barabarani.

Hali hii inatokana na viongozi kutowajibikia usafi wa mji. Mji wenyewe ni mchafu na unatoa harufu ya uvundo (Ukurasa 50). Meya Sosi, anaamuru kuwa Diwani anayesimamia hazina asitoze mishahara ya madiwani kodi.Anatoa sababu kuwa madiwani wana mizigo mikubwa ya kuhudumia baraza (Ukurasa 23). Diwani husika anakubali kutekeleza amri hiyo licha ya kwamba baraza lina nakisi ya shilingi milioni mia moja ishirini.

Meya anatumia mamlaka yake kubuni kamati nyingi zitakazosaidia kuleta usalama. Wanachama katika baraza hili wanalipwa vizuri ingawa halina umuhimu wowote kwa baraza la Cheneo(Ukurasa 22). Ahadi za uongo ni sura mbaya za uongozi mbaya. Meya na viongozi wengine wanatoa ahadi za uongo kwa umma kuwa dawa zimeagizwa na zitawazili hivi karibuni. Katika ukrasa21, ukweli ni kwamba dawa hizo hazifiki zahanatini.

Utawala wa Meya haufanyi lolote kuboresha viwango vya elimu. Meya anadai kuwa elimu ya kwao haina lolote la kumfaa mtoto wa mzazi anayeona mbali. Watoto wake meya wanasomea nchi za nje (Ukurasa 26). Wafanyikazi wanafanya kazi katika mazingira mabaya na magumu. Mishahara yao ni kidogo na inachukua muda mrefu kulipwa. Wengi wa wafanyikazi huwa na madeni na hushindwa kuwa na hazina yoyote wanapostaafu (Ukurasa 67). Meya na madiwani wawili wanavunja sheria wanapopitisha kwamba, mishahara ya madiwani iongezwe. Hayo wanayafanya bila kumshirikisha Diwani III ambaye ni msimamizi wa fedha kulingana na mujibu wa kanuni za baraza (Ukurasa 52-53). Baadhi ya wahusika wanapata kazi kwa njia ya mapendeleo. Mfano mzuri ni mhazili wa Meya. Meya anadai kuwa mhazili wake hakustahili kazi hiyo. Haya ni baada ya mfanyikazi huyo kuondoka ili kuunga mkono wanaogoma.(Ukurasa 77)

Kupitia kwa utawala mbaya, Meya, Bili na Diwani II wanapanga njama ya kuiuza fimbo ya Meya bila kumhusisha Diwani III. Wanaamua kuyafanya hayo kisiri ili Diwani III asipate malipo yoyote kwa kushiriki katika njama hiyo ya kuuza fimbo ya gharama kubwa.

Uongozi wa kuwakandamiza watawaliwa na kuwafanya watumwa katika nchi yao Jamhuri ni mfano mwafaka wa ukoloni mamboleo. Kutowajibika kwa viongozi hawa ni sura nyingine ya utawala mbaya.

Katika nchi au jamii yoyote huwa kuna tabaka la juu na lile la chini. Katika hali kama hiyo, viongozi hutumia mamlaka waliyonayo kujichumia mali. Kwa sababu hiyo, mpaka baina ya matajiri na maskini unaendelea kupanuka. Katika Baraza la Mji wa Cheneo utabaka unadhihirika kupitia kwa sura mbalimbali.

Vyakula wanavyokula viongozi ni tofauti na vile vya watawaliwa. Kiamshakinywa cha Meya kinahusisha chai, mayai na vyakula vingine vya aina mbalimbali ilhali wafanyikazi wake wanapewa vyakula vinavyoliwa na umbwa (Ukurasa 5). Wafanyikazi wa ngazi za chini hawapati nyongeza yoyote ya mishahara ilhali walinda usalama wanaongezwa kwa asilimia ishirini.Haya yanafanywa ili kuwalinda na kuwaendeleza viongozi mamlakani (Ukurasa 22). Wafanyikazi wa viwango vya chini wanatwikwa mzigo mzito wa kuwalipa viongozi kupitia kwa kodi wanazotozwa. Meya anatoa amri kwamba, madiwani wa Baraza la Mji wa Cheneo wasitozwe kodi katika mishahara yao. Madiwani hawa vile vile wanapata mishaara yao kwa wakati ilhali ile ya wafanyikazi wa chini inachelewa mara kwa mara(Ukurasa 68).

Watoto wa viongozi kama vile wa Mstahiki Meya wanasomea katika nchi za ng'ambo zilizo na viwango vya juu vya elimu. Wale wa masikini wanasomea shule za nyumbani ambapo elimu ni ya kawaida, jambo ambalo linazidisha mpaka baina ya matajiri na maskini.

Familia za viongozi wanasafiri ng'ambo kwa huduma za matibabu. Mkewe Meya, ameenda kujifungulia ng'ambo huku Meya akidai kuwa madaktari wa hapa nyumbani ni wa kubahatisha tu (Ukurasa 27).

Huduma za afya zinazotolewa ni duni kwa wenyeji masikini. Madiwani na familia zao wana bima ya matibabu katika hospitali kubwa ilhali wananchi wenye mapato ya chini wanatakiwa kugharamiwa huduma zao za matibabu. Hali hii inakuwa ngumu kwani ni vigumu hata katika kumudu chakula. Hata hizo dawa hazipo katika hospitali za kawaida (Ukurasa 69). Watoto wa madiwani wanachukuliwa na kupelekwa nyumbani kwa magari ya baraza la mji wa Cheneo. Watoto hao wanalipiwa karo na baraza ilhali wa masikini wanahangaika kutafuta karo. Wafanyikazi wa ngazi za chini wanatembea kwa miguu kwenda kazini ilhali madiwani wanachukuliwa nyumbani na kupelekwa ofisini. Wafanyikazi wa chini hawana mtetezi katika vikao vyao vya baraza vinavyofanya maamuzi ya maana. Haya ni kulingana na Beka ambaye ni mmojawapo wa wasimamizi wa wafanyikazi (Ukurasa 71)

Maudhui ya utabaka yanajitokeza sambamba na yale ya utajiri na umasikini. Maskini ni wa tabaka la chini na matajiri ni wa tabaka la juu. Maskini wanaona ugumu wa kukidhia mahitaji yao muhimu kama vile chakula. Ufisadi ni mojawapo ya maudhui ambayo yanadhihirika katika jamii ya Cheneo. Wahusika kama Meya, Bili pamoja na wandani wake Diwani I na II wanachangia pakubwa katika ufisadi.

Ardhi ambayo ni mali ya umma inatumika vibaya kwa manufaa ya wachache. Meya anaviuza vipande vitatu vya ardhi kugharamia safari ya mkewe ng'ambo. Vipande vingine vinne vya ardhi anamgawia afikiye Bili. Meya anakiri kuwa, asipokuwa na pesa

hakuna mwingine anayeweza kuwa nazo.(Ukurasa 27). Katika (Ukurasa 28-30), Bili anagundua njia ya kujinufaisha pamoja na Meya kupitia kwa mwanakandarasi mmoja aliyezuiwa asilete bidhaa hadi Cheneo. Anataka kesi iende kortini halafu alipwe fidia na baraza. Baada ya kulipwa mwanakandarasi huyo alitakikana ampe Meya fungu la pato hilo.

Ufisadi zaidi unajitokeza pale ambapo Meya anamtaka mhubiri afike mara moja kwa juma kuliombea baraza na kuahidi kugharamia pesa ya petroli ya kumleta na kumrudisha. Licha ya hilo baraza litakuwa likimlipa sadaka.ya shilingi laki moja kila mwezi.

Bw.Kheri anakiri kuwa lazima Meya amejipatia pesa nyingi katika kipindi kifupi cha umeya (Ukurasa 50).

Yeye ni mfisadi. Hawasikilizi wafanyi kazi wala kuyakabili matatizo yao kwa njia ya kuridhisha. Katika mazungumzo baina ya Diwani Kheri na Siki, Kheri anakiri kuwa ingawa umeya hauna pato kubwa, ofisi hiyo ina mianya mingi ya kujipatia pesa. Mojawapo ya mianya ni jukumu la jinsi viwanja vya umma vinavyotumiwa.

Meya, Diwani I na II wanashawishika kwa urahisi kuiuza fimbo ya Meya na kutangaza moja kwa moja kuwa ilipotea wakati wa rabsha za migomo ya wafanyikazi. Pato watakalopata kupitia kwa fimbo hiyo wagawane.(Ukurasa 61)

Ni ufisadi mkubwa watoto wa madiwani kupelekwa shuleni kwa gari la baraza la mji. Mafuta ya baraza hilo yanalipwa na baraza. Aidha baraza hilo ndilo linalogharamia karo ya watoto hao licha ya madiwani hao kupata mishahara ya juu.

Ni ufisadi kutowajibika baraza kukosa kutoa fedha kwa hospitali kununua dawa. Wahudumu wa hospitali wanadanganywa kuwa shehena ya dawa ingali njiani na ingefika baada ya siku tatu. Jambo hili linazidi kufilisi baraza huku wagonjwa wakiendelea kufa hospitalini.

Maudhui zaidi yanayojitokeza katika tamthilia hii ni unyanyasaji (udhalimu au ukandamizaji). Wengi wa viongozi katika Baraza la Mji wa Cheneo wanawafanyia wananchi unyama. Wagonjwa wanakufa kutokana na ukosefu wa dawa hospitalini. Wananapodai haki yao, uongozi wake yeye Meya hauwasikilizi. Kila wanapojaribu kuandamana huzimwa na askari kwa kutumia virungu ili kuizima migomo hiyo.

Wafanyikazi wananyanyaswa kwa kulipwa mishahara kidogo na kucheleweshwa kila mara. Zaidi ya hayo wanatozwa kodi ihali wafanyikazi wa mishaara ya juu kama vile madiwani hawalipi chochote. (Ukurasa 22)

Kupitia kwa usemi wa Meya, wafungwa wanateswa gerezani. Chakula chao ni mchuzi na maharagwe. Mazingira wanamokaa mna chawa. Medi anadai kuwa wafanyikazi wanaosha vyoo bila hata glavu. Wamegeuzwa kuwa watumwa. (Ukrasa 17) Kunakuwa na vitisho kila wanapogoma kuwa wataachishwa kazi na wengine waliosoma waajiriwe. Hata nyimbo za migomo zinadhihirisha wazi jinsi ambavyo wafanyikazi wanadhulumiwa. Japo haya yanafanyika migomo yao inazimwa kwa milio ya risasi inayowafanya watu kuukimbilia usalama wao (Ukurasa). Utegemezi uliokithiri ni mojawapo ya maudhui yanayodhihirika katika jamii hii. Waridi ambaye ni muuguzi zahanatini anadai kuwa wazungu wanahimiza mfumo wa kugawana gharama kutumiwa

hospitalini. Jambo hili linakuwa vigumu kwa wagonjwa wasioweza kuimudu gharama ya kuhudumiwa. (Ukurasa 3)

Mstahiki Meya anaungama kuwa atawapa wageni mapokeo ya kupigiwa mfano kwani hawa ndio wafadhili wake wakuu katika Baraza la Mji wa Cheneo. Anataka mishahara ya madiwani iongezwe kwa kutarajia misaada ya wageni ambao ni washirika wao wa maendeleo watawapa mikopo ya kulipia mishahara hiyo. Kwingine Diwani II anahofu kuwa migomo ya wafanyikazi itakuwa hatari kwa misaada ya wageni wanaotarajiwa baada ya kuwazuru (Ukurasa 73)

Viongozi wengi wanavunja sheria katika harakati za kujinufaisha wenyewe. Ukiukaji wa sheria ni maudhui yanayojitokeza kupitia kwa baadhi ya viongozi wakuu serikalini pamoja na washauri wakuu wa Mstahiki Meya. Ni ukiukaji wa sheria Meya kukatisha kandarasi ya anayeliuzia baraza bidhaa bila kuzingatia sheria. Uwajibikaji wa pamoja, unamhitaji Diwani aungwe mkono na uamuzi wa wengine katika baraza hata kama uamuzi huu hauna umuhimu wowote. Mbali na hilo, baadhi ya sheria nyingine zinampa Meya mamlaka mengi. " *Mayor's act* na *riot act*" ni mifano wa sheria hizo.

Dini inafaa kuwakuza watu kiroho na kimaadili. Katika tamthilia hii, dini imesawiriwa kama asasi inayotumiwa kuendeleza uongozi mbaya. Mhubiri anamuunga Meya mkono huku akijua vizuri kwamba, si jambo nzuri. Hatumwoni akimrekebisha Meya pahali popote. Huo ni unafiki. Kwenye maombi ya mhubiri anamsihi Mungu amwondolee Meya nuksi ya maadui na kinyongo cha mahasidi akijua maadui wa Meya ni wananchi wanaodai uongozi wenye uadilifu. (Ukurasa 33)

Mstahiki Meya anamwambia mhubiri kuwa mara mbili alitaka kuacha kazi ya Bwana na kumfuata ili washirikiane na Meya(Ukurasa 41). Hapa Meya anatafuta njia ya kujidumisha mamlakani ili azidi kujinufaisha. Mhubiri naye anachangia unafiki kwa kudai kuwa Meya atachangia kwa kueneza kazi za Bwana huku akijua kuwa Meya hajabadilika wala kukubali wokovu wa Bwana. Ni unafiki kwa muhubiri kukubali ahadi ya Meya kuwa baraza litampa zawadi ya shilingi laki moja kila mwezi. Ni vigumu kwa jambo kama hili kutekelezwa na baraza kwani halitakuwa na uwajibikaji. Ni dhahiri kuwa watu wengi katika Cheneo hawana ajira. Baraza la mji halifanyi chochote ili kubuni nafasi za kazi. Kupitia kwa Diwani III tunapata kujua kuwa watu wengi hawana ajira. Diwani huyu anaendelea kudai kuwa watu watafurika kuja kutafuta kazi iwapo nafasi za kazi za wale waliogoma zitatangazwa kuwa wazi. Anaongeza kuwa waliosusia kazi pia watarudi mbio kudhihirisha kuwa watu wengi hawana kazi.

Meya na wahusika wengine kama vile Bili, Diwani I na II wana ubinafsi. Katika Ukurasa50, Meya anajigawia yeye na walio na uhusiano wa karibu naye vipande vya ardhi vya baraza.. Bili naye anatafutanjia ya kujinufaisha kwa kupendekeza fimbo ya Meya kuuzwa ili apate mgao wa pesa.

Mazingira katika Mji wa Cheneo ni machafu. Uchafuzi huu umetokana na harufu mbaya ya taka inayotoka barabarani. Tatu anamweleza Meya kuwa vyoo ni vichafu. Anaongeza kuwa bado kidogo kipindupindu kitakuwa hali halisi na sio tishio tu (Ukurasa72). Diwani III anamwambia Siki kuwa harufu mbaya ya taka iliyopamba mji ni kiwakilishi cha uozo ulio ndani (Ukurasa51)

Usaliti ni maudhui mengine ambayo yamejitokeza katika *Mstahiki Meya*. Viongozi wanaowakilisha usaliti tamthiliani ni pamoja na Diwani I na Diwani II. Wahusika hawa wanaunga mkono mateso dhidi ya wafanyikazi. Diwani II anadai kuwa amekuwa ofisini akipanga miradi ya uzalendo vile ambavyo waliagana na baadhi ya viongozi. Miradi inayozungumziwa ni ya kuwanufaisha wao wenyewe. Diwani hawa wanamfuata Meya na kukubaliana naye hata kwa maovu anayoyafanya. Wanajipendekeza kwake ili kunufaika kutokana na utawala wake. Tabia kama hii inaitwa ubarakala.

### 3.5 Hitimisho

Katika sura hii tumejaribu kuonyesha jinsi uumbaji wa wahusika unavyohusiana na vipengele vingine. Kama vile maudhui na dhamira katika tamthilia tatu za Arege. Dhamira ya kufanya hivyo ni kupima utimilifu wa kifasihi wa kila kazi ili kuweza kuamua iwapo mwandishi alikuwa akipiga hatua za kukua katika uandishi wake.

Mwandishi amewasilisha sifa za wahusika wa kazi yake na kudhihirisha jinsi wahusika hawa wametumika katika ujenzi wa maudhui ya tamthilia. Kufaulu kumechangiwa kutokana na usemi wa wahusika hawa, nafasi zao katika tamthilia na kuwaangalia kimakundi kwa mfano wahusika wa kike.

Ama kwa hakika, tunaweza kuafikiana kuwa bila wahusika hakuna maudhui wala dhamira kwani hawa ndio nyenzo kuu katika kuendesha gurudumu la maudhui na dhamira. Kwa ujumla, dhamira na maudhui ya kazi hii yamewasilishwa kwa namna wahusika walivyosawiriwa.

# SURA YA NNE

# MCHANGO WA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA KUDHIHIRISHA UKUAJI WA MUUNDO NA MAWAZO KATIKA TAMTHILIA ZA AREGE

## 4.1 Utangulizi

Mbali na sanaa ya uchoraji na ususi, lugha ndio nyenzo muhimu katika uendelezaji wa sanaa yoyote ile. Uteuzi wa msamiati na matumizi tofauti tofauti ya tamathali za usemi huwa ni sehemu muhimu ya kuufanikisha utunzi wa msanii. Hata uchangamano katika ploti na mvuto wa tamthilia kwa msomaji hujengwa kwa matumizi mbali mbali ya mbinu za lugha. Mbinu ambayo imetumiwa kuendeleza tamthilia za Arege ni ile ya sadfa. Inatokea vizuri sana mwishoni mwa tamthilia. Kwa ujumla, mtunzi ametumia mbinu ya sadfa zikiwemo mbinu zingine kuzifanya kazi zake ziwe za kusisimua. Ni kupitia umuhimu huu ndiposa tukaamua tuishughulikie sehemu hii kama kipengele cha kuchangia ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za Arege.
Tamathali za usemi huchukua sehemu muhimu katika uchanganuzi wa mtindo katika matini au kazi za matini au kazi za kifasihi na kwa dhana hii tamathali inatumiwa kwa upana usiokuwa wa kawaida kujumulisha sifa nyingi za kimtindo ambazo hutumiwa katika kazi nyingi za kifasihi.

Mwenda Mbatiah (2001) anaeleza kuwa tamathali ya usemi katika kazi ya kifasihi ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya kisemantiki (maana) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Tamathali za usemi zinaweza kuzungumziwa kwa maneno "lugha ya kimathali." Lugha ya kimathali huwa na majukumu matatu makuu:

i) Urembeshaji wa kinachozungumziwa au kinachorejelewa na kukifanya kuwa na mvuto mkubwa wa kisanaa au kiumbuaji.

ii) Uthibitishaji, yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani, na kwa njia hii kuleta matokeo makubwa.

iii) Ufafanuzi au uelezaji wa kinachohusishwa na tamathali maalum.

Majukumu haya matatu yanaweza kuhusishwa na lengo kuu la kuzua lugha au usemi wenye lugha ya kiushawishi. Hii ina maana kuwa lugha ya kitamathali inaweza kuwa nyenzo katika ujengaji au uimarishaji wa hisia. Tamathali hurejelea maana ambayo hayakuwa wazi na ambayo msomaji anaweza kuzindua ili aweze kuelewa.

Katika tamthilia, mwandishi amewasilisha tamathali za usemi kikamilifu kupitia kwa mazungumzo ya wahusika. Timothy Arege ametumia mbinu mbali mbali katika kazi zake. Miongoni mwa mbinu hizi ni:

### 4.2 Tashhisi/uhuishi/uhaishaji

Hii ni mbinu mbinu ambayo vitu ambavyo havina sifa ya kibinadamu vinapewa sifa au wasifu wa kibinadamu. Inawezekana pia maneno fulani dhahania yakahusishwa na sifa za kimaumbile. Aghalabu tamathali hii ya usemi hutumiwa kuwapa wanyama sifa za kibinadamu. Tamathali hii inasemekana kuwa na uwezo mkubwa wa kugusia hisia za msomaji au msikilizaji. Mathalani, katika *Chamchela*, Sure analalamikia mabadiliko ya ulimwengu akisema hivi:

**Sure**: Uzungu unatumeza kwa pupa (Ukurasa 2)

Haya ni matamshi ya Sure kwa Atisa akidhihirisha mshangao wake kuhusu mabadiliko ya ulimwengu hasa ile hatua ya mwanao Mayaka. Uzungu hapa umepewa uwezo wa kibinadamu kumaanisha mila na tamaduni za mwafrika zimeathiriwa pakubwa. Mifano zaidi ya mbinu hii katika tamthilia hii ni:

> "Njia ingemweleza msafiri kitakachomkabili mbele, angekwepa mabaya yote ila tu maisha yangekosa udadisi na umakini" (Ukurasa7).

Hili ni tamko la Sure kwa Mbiki asubuhi ile alipowatembelea kwenda kuwajulia hali kwao nyumbani. Katika mbinu hii, njia imepewa uwezo wa kibinadamu wa kutoa maelezo.

> "Baadhi ya mambo yanapomshinda mlimwengu, hubidi kuyakuyakubali yajavyo na kuyapokea. Lau sivyo, ulimwengu utamfanyia maonevu makubwa"(Ukurasa7).

Haya ni maoni ya Sure akiwa kwao Mbiki kumaanisha kuwa ni heri Rosa akubaliane na hali ilivyo. Ulimwengu umebinafsishwa na tabia ya kuonea aliyo nayo binadamu. "Tayari wamemezwa na upepo wa wakati" (Ukurasa10).

Haya ni matamshi ya Sure baada ya kuyashuhudia mabadiliko ya mitindo ya vijana kama vile kujipaka rangi, kusonga nywele na kutoga masikio. Upepo katika usemi huu umetundiwa kiungo cha mdomo cha kukimezea kitu. "Mkondo wa mto hata ukawa mrefu vipi hahusahau chanzo chake." (Ukurasa29).

Huu ni ushauri wa Atisa kwa nduguye Mayaka alipomtembelea mjini kumsihi kubadilisha uamuzi wake kuhusu ndoa na akubali kuitikia wito wa mamake wa kurudi nyumbani. Mkondo hapa umepatiwa uwezo wa kuweza kuyakumbuka mambo kana kwamba ni mtu.

Katika *Kijiba Cha Moyo*, mbinu ya tashihisi inajitokeza kwa njia zifuatazo:

"Unaona kama muziki una uwezo wa kuliwaza nafsi yako?" (Ukurasa 6)
Swali hili linaelekezwa kwake Aisha mkewe Sele wakiwa kwao nyumbani. Hapa neno "muziki"
umepewa uwezo wa kutenda kama binadamu yeyote.

"Maji yaliyoujenga mto jana ni tofauti na yanayoujenga leo" (Ukurasa17)

Haya ni matamshi ya Bi.Rahma akimwelezea Zainabu wakiwa kwao Sele. Katika usemi huu maji ndiyo yamepewa uwezo wa kujenga kama ilivyo kwa binadamu.

"Mtu mzima akisema jambo, upo uhakika kuwa kaliona. Ndio maana wakasema kuwa ikiwa halipo, lipo njiani laja." (Ukurasa27)

Aliyeyatamka haya ni Bi.Rahma alipomtembelea Sele nyumbani kwao. Jambo lililo njiani, katika usemi huu limepewa uwezo wa kusafiri kama afanyavyo mtu.

**Sele**: Kibuyu chake hiki kitaniangamiza kabla ya ugonjwa wenyewe (Ukurasa80).

Vile binadamu wengine wanavyowaangamiza wenzao ndivyo kilivyohaisishwa kibuyu.

Katika *Mstahiki Meya*, Siki ameipa njaa sifa ya kiumbe hai. Anasema, "njaa ina nguvu imeangusha miamba." (Ukurasa34). Anazungumza haya akiwa katika ofisini mwake.

Diwani III anasema , "Cheo kinaweza kumlevya mtu asahau alipokuwa jana." Cheo kimepewa uhai."(Ukurasa 47) Anasema haya wakiwa na Siki nyumbani kwake Diwani III akimaanisha Mstahiki Meya ambaye amebadilika kwa sababu ya madaraka.

Bunduki imepewa uhai na Dida anapodai kuwa inatema risasi tatu tatu. (Ukrasa64) Vile vile magari yamehaisishwa Dida anapozungumzia kuwa yanatapika maji." (Ukurasa 65).Meya anaipa harufu uwezo wa kutawala. (Ukurasa73)

### 4.2.1 Matumizi ya balagha

Hii ni mbinu ya matumizi ya maswali ambayo hayajibiwi kwa kuwa majibu yake yako wazi au yanachochea fikira au hisia kwa upande wa msomaji au msikilizaji. Haya ni maswali muhimu sana katika sanaa ya usemaji. Ikiwa maswali haya hayawezi kuchochea fikira zozote za msomaji au msikilizaji kwa mfano, uelewa wa matini nzima utakuwa ni ngumu. Mifano ya maswali ya balagha katika *Chamchela* yametumika ifuatavyo:

Hata mila zetu zinauliwa huku tukiona bila hata kuatama jambo? (Ukurasa4)

Swali hili la kibalagha ni la Sure akiwa na Atisa akimtaka amtafute alipo nduguye Mayaka ili arejee nyumbani ii kiwadokezea kuhusu uamuzi wake dhidi ya ndoa yake na Bisase. Itakuwa vipi mtu aliyekushinda kwa umri kukuita mamkwe? (Ukurasa9)

Swali hili la kibalagha liliulizwa na Rosa akiwa na Sure wakiongea kuhusu uhusiano wa mwanao Mayaka na Bisase Nilikulea wewe kwa mikono hii yangu. Tena nimlee mtoto wako wewe?"(Ukurasa18)

Hapa ni nyumbani kwake Bisase akiwa na bintiye Sera wakizungumzia kuhusu Lema ambaye ni mtotowe Sera ambaye pia ni mjukuu wake Bisase. Sera hamjali mtoto wake kwa sababu ya kuzurura kwake mjini. Lema ni mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa.

"Mayaka, lakini si ulikuwa unampenda sana Sabina?" (Ukurasa27)

Hili ni swali lake Atisa akiwa na nduguye Mayaka baada ya Mayaka kukiri kuwa hampendi Salima kwa kuwa ameyabadilisha mawazo yake. Kwa sasa anampenda Bisase kwa hivyo Salima yuko huru.

Ikiwa Mayaka anaziba pengo mliloacha pana tatizo gani? (Ukurasa22)

Swali hili ni lake Bisase akiwa na bintiye Sera nyumbani kwao. Haya ni baada ya Sera kumkosoa mamake kuwa uhusiano wake na Mayaka kimapenzi unaitia familia yao aibu. "Mayaka, hivi ndio mwanzo unajifunza lugha? Mbona lugha inakuwa ngeni kwako?" (Ukurasa41)

Hapa ni nyumbani kwake Bisase akiwa na Mayaka ambaye ameshindwa kujieleza kwa njia ya uwazi kutokana na midomo ya watu kuhusu uhusiano wake na Bisase. Katika tamthilia ya *Kijiba Cha Moyo*, maswali ya balagha yamejitokeza kama ifuatavyo:

"Madaktari washindweje na wao ndio manyakanga?"(Ukurasa22)

Swali hili la kibalagha liliulizwa naye Bi.Rahma akiwa kwao wazazi wake Sele. Ni njia ya kuonyesha mshangao wa kutowezekana kwa jambo. "Mimi ni nani?niko wapi?ninakwenda wapi? wanawatoa wapi?Wao ni nani?wanatoka wapi? Wanakwenda wapi?wanawatoa wapi?Wanawape leleka wapi?(Ukurasa 96)

Maswali haya yanaulizwa na Sele mwishoni mwa tamthilia akiwa katika chumba chake cha kulala.Mathalani katika tamthilia ya *Mstahiki Meya,* mbinu ya balagha inajitokeza kupitia mifano hii:

"**Waridi**:mbona nisiwe na hakika?(Ukrasa2)

Swali hili la kibalagha liliulizwa na Waridi akiwa na Daktari Siki zahanatini. Siki hana uhakika kuhusu uwezekano wa madawa kuwepo zahanatini baada ya kipindi cha muda wa siku tatu.

**Siki**: Aliyesema nchi hii maskini nani? (Ukurasa 3)

Siki angali zahanatini akiwa na Waridi. Siki haamini usemi wa Waridi kuwa nchi ya Cheneo ni masikini.

"Sina haja na hadithi zako za pole. Amekutuma nani kunichoma kwa chai mapema hii? Una njama gani? (Ukurasa9)

Matamshi haya ya hasira yanamtoka Mstahiki Meya wakati wa asubuhi akila chamshakinywa. Anamwambia mfanyikazi wake Dida baada ya kuchomwa na chai na baada ya kugundua kuwa mayai sahanini yalikuwa madogo zaidi kuliko ilivyo kawaida.

**4.2.2 Uzungumzinafsia**

Hi ni mbinu ya lugha ambayo mhusika fulani hujisemea lakini hadhira inapata fursa ya kusikia yale yanayompitia. Aghalabu mbinu hii hutumika kuonyesha mchafuko au mkanganyiko fulani wa kimawazo aliyonayo mhusika au mawazo fulani yanayomsumbua.

Mathalani mhusika mkuu Mayaka katika tamthilia ya *Chamchela* akiwa nyumbani kwa Bisase wakati wa jioni anaonekana mwenye wasiwasi. Mara anarandaranda na kujizungumzia hivi:

> **Bisase**:Kweli inapodhihiri, shaka huondoka. Lakini je,ikiwa shaka itadhihiri wema utafanya nini? Dunia kweli msongamano wa mambo. *(Anaketi huku akishika tama)* Bisase*!* Mfadhili wangu wakati kidau cha maisha kilitishwa na mawimbi. *(kwa sauti zaidi)*. Rosa!Rosa! Kama si wewe nisingekuwa katika jukwaa hili la maisha. Nafasi niichezayo katika mchezo huu wa kuishi umenipa wewe. Lakini ......" (Ukurasa39)

Kwingine tunakumbana na Atisa chumbani mwake. Anakuwa na haya ya kusema:

> **Atisa**:Tazama.Tazama mlimwengu anavyotawaliwa na ubinafsi wake.
> Ubinafsi uliochochewa na kiburi. Kiburi cha kujiamini na kuamini katika nafsi yake. Moyo wake hasa.(pole pole) kiini cha vuta n'kuvute! mapenzi! kupenda na kuchukia ndio mapenzi.Ni kama sarafu ya pande mbili (Ukurasa57)

Musa, katika *Kijiba cha Moyo,* ana wasiwasi kuhusu ugonjwa wa Sele unaomfanya kuwazia sababu za kuwepo na hali kama hii ambayo mtu hahisi kuwa mgonjwa lakini wengine wanamwona ni mgonjwa.

> **Musa**: (*Akijisemea*) kitu gani hiki kitamfanya mtu. Asihisi kama yeye mgonjwa lakini. Wengine wasadiki kuwa anaumwa? Tena mtu mzima! Si mtoto. (*kimya*) kweli mambo kangaja. Anachukua bilauri yake na kuizungusha mkononi. *(Anairudisha mezani.Baada ya muda anaigia Sele.)(*Ukurasa 49*)*

Mbinu hii ya uzungumzi nafsia inajitokeza katika *Kijiba Cha Moyo*. Haya ni kupitia kwa mhusika Sele.

> **Sele**:Nahisi mimi na wao tumo jukwaani tunaucheza. Mchezo mmoja ila wao wameutunga na kuuelekeza. Mimi ni mwigizaji wao ni waelekezi na waigizaji. Lazima niicheze sehemu yangu watakavyo wao. Nisiulize swali wala kukaidi." (Ukurasa 97)

Mathalani katika *Mstahiki Meya*, Meya anapokuwa afisini mwake akipanga namna ya kupokea mameya wageni, anaongea peke yake kuhusu dhifa murua atakayowapa wageni ili apate sifa kubwa pamwe na baraza lake. Anaanza hivi kabla ya rafikiye Bili kuingia:

> "Safi (*kimya*) huyu nitamfurusha. Hata akashitaki ni bure…"(Ukurasa25)

Kupitia uzungumzi nafsia huu tunatambua ubinafsi wa Meya na namna anavyobinafsisha mali ya baraza la mji wa Cheneo na kuzitumia tu namna anavyotaka. Maudhui ya ubinafsi wake na sifa yake ya maringo inajitokeza.

### 4.2.3 Kuchanganya ndimi

Hii ni mbinu ambapo mtunzi anatumia lugha mbili au zaidi katika maongezi yake. Kupitia mbinu hii tunaweza kutambua kwamba mhusika fulani ana uelewa sawa wa lugha hizo zote kwa pamoja au ni msomi hasa pale ambapo anatumia lugha ya Kiingereza. Mbinu hii pia inaweza kujitokeza ikiwa mhusika alikuwa na wepesi wa

kuzungumza na akakosa msamiati ufaao wa kutumia katika kugha yake ya kimaongezi. Matumizi ya mbinu hii huenda yakachangia au kutatiza uelewwa wa muundo mzima wa tamthilia pale ambapo au endapo msomi hatakuwa na uelewa wa lugha ngeni iliyotumika. Mifano ya matumizi ya mbinu hii katika *Chamchela* ni kama ifuatayo:

"Kwa nini unapenda *kunienjoy* kiasi hiki *brother*?"(Ukurasa24)

Ni mazungumzo kati ya Mlinzi I na Mlinzi II wakiwa nyumbani kwa Bisase. Mlinzi II anamsihi Mlinzi I aaje kumfanyia utani. Anampa habari kuhusu uhusiano wa kimapenzi wa Mayaka na Bisase "Wewe unaona kama maisha yetu kilele ni kuishi katika *servant quarter*?" (Ukurasa30)

Haya ni mazungumzo kati ya wasomi wawili; Kofa na Rukia wakiwa barabarani wakilalamikia kuhusu ugumu wa maisha ambao licha ya kuwa na digrii, bado wanakaa kwenye chumba cha wafanyikazi wa nyumbani.

"Umesahau yote tuliyofundishwa chuoni katika ile kozi ya *Rural sociology*?" (Ukurasa34). Hili ni swali lake Rukia kwa mwenzake Kofa akimkumbusha waliyoyasoma kuhusu mojawapo ya kozi inayoangazia maisha ya mashinani.

"Sisi bwana ni *patrons* wa kila siku hapa" (Ukurasa 65)

Haya ni madai ya Mteja I akiwa mkahawani. Anamtaka mhudumu amwondoe nje Atisa kwa madai kuwa anasababisha ukosefu wa utulivu pale mkahawani. Anamaanisha kuwa wateja ni watu wenye umuhimu mkuu katika biashara. "Jambo hili bwana limemtia *mapressure*" (Ukurasa 67)

Hili ni tamko la Mteja I kwa Mteja II wakiwa mkahawani akimwelezea vile uamuzi wa Mayaka umemwathiri kimawazo mamake hadi kumpelekea kulazwa hospitalini.

"*Yes boss*, niwape nini?" (Ukurasa69)

Hili ni swali la mhudumu kwake Atisa akiwa mkahawani na dadake Mbiki. Anamwita hivi ili kumsifu na pia kuonyesha heshima kwa mteja wake.

Matumizi ya kuchanganya ndimi katika *Kijiba Cha Moyo* ni kama ifuatavyo:

> **Daktari**:Sitaki kupoteza muda hapa. *Time is money*" (Ukurasa 53)
> Anayeambiwa haya ni Sele akiwa hospitalini baada ya Sele kumdadisidadisi kwa maswali ambayo yaelekea kwake yalikuwa ni ya kumpotezea Daktari muda wake.
> **Sele**: Ni kweli nilitaka kujua kama *grafting* nyingine inawezekana"(Ukurasa 57)
> Anamwambia Daktari maneno haya akiwa hospitalini ili kutaka kujua ikiwa kuna uwezekano wa kuibadilisha rangi ya ngozi yake.
> **Jamila**:Si Sele bado ndo yule wa Mikanjuni *secondary*?"(Ukurasa59).
> Swali hili laelekezwa kwake Sele wakiwa hospitalini wakikumbushana walipokuwa katika shule ya upili ya Mikanjuni.
> **Jamila**: Ulikuwepo lakini si sana. Unajulikana katika lugha ya kitabibu kuwa *Body Dysmorphic Disorder* yaani B.D.D".
> Haya ni maelezo ya Jamila kwake Bi.Rahma kumaanisha hali inayomkumba mtu kutoipenda sehemu fulani ya mwili wake na kuichukia.
> Katika *Mstahiki Meya* kuchanganya ndimi kunajidhihirisha hivi:*What do you think this food is?food poisoning*? (Ukurasa5)

Hili ni swali la Waridi kwake Daktari wakiwa zahanatini kuhusu ugonjwa wa mtoto ambaye alikuwa amekila chakula kilichotolewa kwa Mstahiki Meya. Usemi huu unamaanisha kuwa tayari chakula chenyewe kilikuwa kimeharibika na hivyo basi kudhuru afya ya mtoto. *Oh,yes* (Ukurasa 5)

Huyu ni Siki akikubaliana naye Waridi kuhusu uamuzi wa hapo juu. *I understand* (Ukurasa 5)

Huyu ni Siki ambaye anaonekana kukubaliana naye Waridi baada ya kumuamuru ampeleke mtoto kwa wadi.

Dawa zilizopo ni *pain killers* tu (Ukurasa 6)

Huyu ni Siki akimhakikishia Waridi wakiwa katika zahanati kuwa dawa zilizopo zilikuwa za kuyapunguza maumivu na wala sio za kuutibu ugonjwa.*Yes, sir* (Ukrasa 15)

Huyu ni Gedi akikubaliana naye Mstahiki Meya kuwa kamwe asimruhusu Daktari Siki kukaribia kwake nyumbani. Haya ni baada ya Mstahiki Meya kukataa kuyasikliza mawaidha ya Siki kuhusu hali mbaya pale zahanatini.

Nina *entertainment vote* ya Meya yangoja uhalisi tu (Ukurasa 27)

Hiki ni kibali cha kumruhusu Meya kuburudika na gharama kulipwa na Baraza la Mji. Huyu ni Meya akimhakikishia rafikiye Bili kuwa yuko tayari kumpeleka nje kwa ziara yeye na familia yake wakati wowote ule na gharama iwe ni juu yake Meya Sosi.

Hasa ile *prime plot* (Ukurasa 27)

Hiki ni kipande cha ardhi Meya alikuwa amemgawia Bili. Alikuwa anamshauri akiuze kwa ajili ya kugharamia mahitaji yake na watoto.

*Gentlemen's agreement* Mstahiki Meya (Ukurasa 29)

Haya ni makubaliano kati ya Meya na rafikiye Bili baada ya kukubaliana kushindwa kesi na mwanakandarasi mmoja lakini pato atakalolipata kutokana na fidia amgawie Meya na Meya kumkumbuka Bili.

Kuna *mayor'act* na *riot act* (Ukurasa 48)

Hiki ni kifungu cha sheria kinachompa Meya mamlaka ya kutumia nguvu katika kuzima migomo au maandamanaji. Kinachoitwa *collective responsibility* (Ukurasa 49)

Hii inamaanisha kuwa ili hoja ipitishwe katika kikao, lazima ipitishwe kulingana na wingi wa kura za wanakamati hata kama ni mbaya. Hii ni *grand idea* (Ukurasa 62)

Ni matamshi yake Meya kumaanisha kuwa ni wazo zuri kuiuza fimbo na vyombo vya habari kutangaza kuwa iliibwa wakati wa rabsha za mgomo wa wafanyikazi.

### 4.2.4 Tashbihi

Hii ni tamathali ya usemi ambayo vitu viwili au zaidi hulinganishwa kwa kutumia maneno kama vile mithili ya, mfano wa, fanana na, sawa na na mengine. Mathalani katika *chamchela* mifano ifuatayo imetumika:

Rukia anamwambia Kofa:"na ndivyo mlivyo siku hizi. Mifano ya wanaume(Ukurasa 33)

Anasema haya wakiwa njiani wakijadili kuhusu baadhi ya waume ambao wameyakwepa majukumu ya malezi ya watoto waliowazaa.

"Lazima mwanamume kusimama tisti (*Akionyesha kwa kidole*) wima baba."

(Ukurasa 45)

Hapa ishara ya kidole inaonyesha kuwa wima kama kidole. Huyu ni Bisase akimhimiza Mayaka kuwa na msimamo wima akiufananisha kama kidole chake cha mkono.

"Maisha ami ni kama safari ndefu ya angani" (Ukurasa 49)

Atisa aliyasema haya wakiwa kwenye kikao cha wazee nyumbani kwa mzee Sure kutafuta suluhu kumhusu Mayaka. Alimjibu Sure baada ya kudai kuwa vijana hawawakaribii sana wazee.

"Kupenda na kuchukia ni kama safari ndefu ya angani" (Ukurasa 49)

Huyu ni Atisa akizungumza peke yake katika chumba chake. Anailinganisha hali ya kimapenzi inayomkabili Mayaka na mpenziwe Bisase na safari ndefu ya angani. Ifuatayo ni mifano ya matumizi ya tashbihi katika *Kijiba cha Moyo*:

> **Bi. Rahma**: Na hiyo ndiyo dunia. Mfano wa mto "(Ukurasa17)
> Anamfananishia Aisha dunia sawa na mto ambao unajengwa na maji tofauti lakini unabaki kuwa mto. Hivyo ndivyo ilivyo katika dunia ambapo licha ya kuwa na mabadiliko, bado dunia ndio ile ile haibadiliki.
> **Bi.Rahma**: Ni kama kisima. Kila mtu atachota na kila kiumbe kunywa apendavyo." (Ukurasa19)

Hapa anamlinganishia Aisha elimu ya wazee na ile ya leo kama kisima kilichochotwa maarifa na kuingishwa vitabuni.

> **Sele**:Na mimi nahisi kama sisi tunayumbishwa mithili ya miti msimu wa kipupwe."(Ukurasa 29)
> Anamweleza Bi.Rahma kwa kuyalinganisha mataifa makubwa na kipupwe na yale madogo kama miti ambayo haiwezi kustahimili msimu mkali wa kipupwe. Masharti yaliyowekewa mataifa haya madogo ndiyo yamewafanya akina Sele kuachishwa kazi. Hali hii ndiyo imechangia hali aliyo nayo Sele hivi:
> **Sele**: Mchanganyiko labda ila yote hunjjia mfano wa kitu na kivuli chake." (Ukurasa 42)

Hapa Sele analinganisha mchangayiko wa habari za wajihi wake na papa baharini kama vitu viwili ambavyo haviachani vile ilivyo katika kitu na kivuli chake.

Katika *Mstahiki Meya* matumizi ya mbinu ya tashbihi yanajitokeza katika mifano ifuatayo:

Meya anapokuwa na Daktari Siki ofisini mwake anaelekea kutoelewana naye kuhusu mipango na taratibu zake Meya Sosi. Anamwonya kwa kusema:

> **Meya**: kupinga haya ni sawa na kumkama simba mwenye watoto"Ukurasa14.

Meya anatumia tashbihi hii ili kumwonya Daktari Siki asithubutu kupinga hoja zake. Mifano mingine ya tashbihi ni kama ifuatayo:

> Watu kujifia kama nzi (Ukurasa38)

Huyu ni Tatu akilalamikia kufa kwa wingi kwa wagonjwa mfano wa nzi.

Mimi na Meya ni mfano wa mafuta na maji (Ukurasa45).

Huyu ni Siki akimwambia Diwani III kuwa hawasikizani wala hawapatani na Meya. Tayari Siki alikuwa amefurushwa kwake Meya alipomtembelea kumshauri kuhusu hali ya pale zahanatini.

Vitu hivi (njaa na tamaa) viwili kwa pamoja ni ugonjwa mbaya kuliko tauni (Ukurasa47)

Haya ni matamshi yake Diwani III akiwa na Siki. Walio na njaa na tamaa ni madiwani ambao sharti wajipendekeze kwa Meya ili kujinufaisha wao kwanza bila kujali maslahi ya wananchi waliowachagua. Juzi mtoto wa Kerekecha amekufa kama nzi (Ukurasa 69) Huyu ni Medi ambaye pia ni mwakilishi wa wafanyikazi akiongea kwa hasira kuhusu kisa cha mtoto aliyekufa kwa njia rahisi kwa kukosa dawa hospitalini.

### 4.2.5 Methali

Methali ni usemi au kauli fupi zenye busara na mafunzo. Methali kama mbinu ya matumizi ya lugha inapotumika huwa ni nyenzo katika mazungumzo. Kuna methali nyingi ambazo zimetumika katika tamthilia hizi. Ifuatayo ni baadhi ya methali kama ilivyotumika katika *chamchela*:

"Mtu hujikuna ajipatapo" (Ukurasa9)

Haya ni maneno ya busara kutoka kinywani mwa Sure aliyomwambia Rosa alipomtembelea kwake nyumbani. Anamsihi ayakubali mambo vile yajavyo na aache kusumbuliwa sana na uamuzi wa mwanawe Mayaka.

"Safari ndefu, huanza na hatua moja" (Ukurasa 11)

Huu ni usemi wa Sure kwake Rosa akimhimiza kuwa na uvumilivu na utaratibu. Anayasema haya wakiwa nyumbani kwake Rosa wakijadili hatua ya uamuzi wa mwanao Mayaka ya kumwoa Bisase. "Haraka haraka,haina baraka" (Ukurasa19)

Ni usemi wa Sera kwa mamake Bisase akimhimiza kuwa wakati wa kuambiwa Lema babake mzazi ni nani haujafika. Jambo hili limekuwa likimtatiza sana Lema hasa pale anapochekwa na watoto wengine shuleni. Bisase anamtaka Sera amjulishe Lema babake mzazi ndiye nani ili amwondolee mwana huyu tatizo hilo la moyoni. "Kipendacho roho hula nyama mbichi" (Ukurasa 36). Usemi huu ni wa Kofa akimwambia Rukia wakiwa

njiani. Anamaanisha kuwa, uhusiano kati ya Mayaka na Bisase kuwa ingawa ni jambo ambalo linaonekana kuwa geni ni kwa sababu ya mapenzi. "Akufaaye kwa dhiki, ndiye rafiki" (Ukurasa41).

Ni ushauri wa Bisase kwa Mayaka kuwa asiyasikilize mambo ya watu eti anachekwa na pia akumbuke kuwa yule ambaye anakusaidia wakati wa shida ndiye rafiki wa kweli.

"Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu" (Ukurasa52).

Tamko hili ni onyo aliyoitoa Mzee Sure kwa vijana hasa akimlenga Mayaka kwa kukosa kuwasikiliza wazazi wake kuhusu msimamo wake mkali wa hatua aliyoichukua ya kumwoa Mayaka.

(vi) "Lisemwalo, lipo" (Ukurasa52)

Huu ni usemi wa Abaya wakiwa katika kikao cha wazee walipoitikia wito wa mzee Sure kuja kutafuta suluhu la uamuzi wa Mayaka kuhusu ndoa. Anamwambia Sure baada ya kutoa laana kwa Mayaka kuwa kwa vile amekataa kusikiliza wazazi wake ataangamia.

"Aliliaye wembe hupewa (Ukurasa 61).

Aliyeyasema haya ni Salima akimwambia Atisa kuwa huwezi kumlazimisha mtu kulitenda jambo au kumkataza mtu ambaye tayari ameazimia kufanya jambo fulani. Ni vyema ajilaumu mwenyewe baadaye baada ya kupatwa na maafa. Matumizi ya methali kama tamathali mojawapo ya usemi imetumika ifuatavyo katika *Kijiba Cha Moyo*:

"Heri huvutwa na subira" (Ukurasa14).

Huu ni ushauri wa busara kutoka kwa Bi.Rahma akimtolea Zainabu wakiwa nyumbani kwake Zainabu. Ameitumia methali yenyewe kumaanisha kuwa Aisha hafai kuharakisha katika kumuandalia Sele mapishi. Yafaa achukue muda ndipo chakula kiweze kuwa na ladha ya kuliwa. "Mhitaji siku zote mtumwa" (Ukurasa 25).

Haya ni maneno ya busara ya Musa akiwa na mkewe Zainabu kwao nyumbani. Mhitaji katika muktadha huu ni nchi maskini (wanyonge) ambazo hazina budi kuitikia agizo lolote liwe zuri au baya. Kwa mfano kusimamishwa kazi kwa Sele kunarandana na methali hii.

"Polepole ndio mwendo" (Ukurasa 26).

Haya ni maneno ya busara ya Musa aliyomshauri mkewe Zainabu kabla ya kuondoka nyumbani kwake. Ni ushauri wa kuwaongoza kuwa wasiharakishe kumtibu Sele kabla ya kufuata utaratibu muhimu kama vile kuongea na mkewe kwanza. "Ikiwa halipo,basi lipo njiani laja"(Ukurasa 28).

Methali hii ilitumiwa na Bi.Rahma wakiwa na Sele chumbani kwake. Imebidi ayaseme haya baada ya Sele kukiri kuwa hana maumivu yoyote na huku ameipa familia nzima waziwazi wa kubadilika kwa mwenendo wake. Bi.Rahma anamaanisha kuwa ikiwa Sele angali anakataa kwamba si mgonjwa akumbuke kuwa jambo lisemwalo lipo na lawezekana. "Mwenye nguvu mpishe" (Ukurasa 29).

Methali hii ilitumiwa na Bi.Rahma akiwa na Sele chumbani kwake. Maelezo yake yanafanana na yale ya methali, "Mhitaji siku sote mtumwa"

*Mstahiki Meya* imetumia methali nyingi katika mikitadha maalum. Mathalani wakati Daktari Siki na Nesi wanaongea kuhusu namna ugonjwa usivyoweza kungoja madawa Kwa muda mrefu, Siki anamwambia Waridi, "Hujui ngoja ngoja huumiza matumbo?'' (Ukurasa 2) Hii ni kumaanisha kuwa wagonjwa wanaweza kungojea madawa lakini ugonjwa hauwezi kungoja dawa. Mifano zaidi ya methali ilivyotumika ni kama ifuatavyo:

"Haraka haraka haina baraka"(Ukurasa 2).

Siki na Waridi wanapokuwa hospitalini wakizungumzia kucheleweshwa kuingia kwa dawa hospitalini, Waridi anamshauri Siki aendelee kusuburi na asiwe na haraka kwa vile haraka haraka haina baraka.

"Ganga ganga za mganga humlaza mgonjwa na matumaini"(Ukurasa 6)

Baada ya Siki na Waridi kukosa dawa za kuwatibu wagonjwa inabidi wamwandalie mgonjwa mchanganyiko wa chumvi na sukari angalau mgonjwa aone anahudumiwa ili apone kutokana na kujawa na tumaini. Ndiposa Siki anamwambia Sele kuwa ganga ganga za mganga huleta tumaini. "Wasemao mchana usiku watalala"(Ukurasa 31)

Bili na Meya wakiwa afisini wakipanga njama ya kunufaika kutoka kwa mwanakandarasi, mara kelele za wagomaji kinasikika pale nje. Bili anayapuuza hayo kwa kutumia methali, "wasemao mchana usiku watalala" "Mbio za sakafuni huishia ukingoni" (Ukurasa 33)

Huu ni ushauri wa Bili kwa Meya wakiwa ofisini akimaanisha kuwa kelele za wagomaji bila shaka kitaisha kwa kuzimwa na milio ya bunduki za polisi. "Sikio la kufa halisikii dawa" (Ukurasa 46).

Mstahiki Meya ndiye sikio la kufa kulingana na methali hii kama ilivyotumika na Diwani III. Amekataa kusikiliza ushauri wake Diwani kama alivyokuwa akifanya hapo awali.

### 4.2.6 Dhihaka

Hii ni tamathali ya usemi ambayo inatumika kujengea ucheshi. Kauli inayosemwa kwa dhihaka huwa kimsingi inaonyesha kuwa msemaji alifahamu jambo fulani analomweleza anayezungumziwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja na labda kwa njia hiyo kumcheka au hata kumbeza.

Mathalani katika *Chamchela* Mlinzi I na II wakiwa nyumbani kwa Bisase wanamkejeli Mayaka katika mazungumzo yao wanapomwita Mayaka "mzee" (Ukurasa 24) kumaanisha mumewe Bisase. Matumizi ya mbinu hii katika *Kijiba Cha Moyo* ni kama ifuatavyo:

> **Sele**: Mimi nimewaambia siumwi, wanasema naumwa. Nao wanaamini kuwa naumwa
> na mimi sihisi kuumwa. (*kwa Bi. Rahma*). Wewe pia ulipokuja siku ile nilikwambia,
> ila hata wewe hutaki kuniamini. Tuseme mimi naumwa na nyinyi kuhisi maumivu? (Ukurasa 42).

Katika *Mstahiki Meya*, tunaelezwa vizuri kuwa Meya Sosi ni mtu aliye na moyo mgumu na wa kishetani anayeitendea jamii mambo mabaya sana huku mwenyewe na wandani wake wanafaidika kutokana na rasilimali za umma ambazo wamezihodhi. Lakini katika kisa kimoja Meya akiwa na mhubiri anajifanya mtu aliyepata wokovu kamili na anadanganya kuwa anaguswa na kuwepo kwa mhubiri hata baadhi ya wakati hufikiria kuacha kazi ya umeya akajiunga na kazi ya kanisa. Anatoa matamko ya kidini ''aameni ! aameni !''kana kwamba kaokoka kumbe ni unafiki (Ukrasa41-44). Kisa cha Meya kujifanya mtu aliyeokoka na kutoa matamko ya kidini ni cha kuchekesha.

### 4.2.7 Mdokezo

Hii ni mbinu ambapo kauli au maneno huachwa bila kukamilishwa au hutundikwa tu. Utundikaji huchochewa na sababu kadha. Kwanza inaweza kuwa ni mbinu ya kujenga taharuki kwa kuacha pengo fulani la kiusemaji na kwa njia hii kuwa mkakati muhimu wa kuchochea mtagusano katika usomaji wa matini au kazi ya kifasihi ambapo msomaji anaalikwa kukamilisha sehemu iliyopaki.

Pili, mbinu ya utundikaji inaweza kuchochewa na tasfida–kuacha jambo ambalo vinginevyo lingekera. Katika kazi yetu kwenye *Chamchela* mifano hiko katika sehemu zifuatazo:

> **Atisa**: (anashangaa) Lakini…"(Ukurasa1)
> Anakatizwa usemi huu na Sure kabla hajamaliza kujieleza ni kwa nini ilivyo vigumu kumpata nduguye Mayaka. Baadaye anaaukamilisha usemi huu kwa madai kuwa nduguye alikuwa tayari amehamia kwingine na hivyo basi imekuwa vigumu kumpata
> **Atisa**: Si kwamba inapenda. Ni……..(Ukurasa4)
> Atisa anataka kukamilisha usemi huu kuwa si kuwa sheria inapenda ila inapendelea. Mayaka: Lakini wenyewe wanasema eti..eti..(Ukurasa41)
> Katika mdokezo huu Mayaka anataka kusema kuwa watu wanasema kuwa eti yeye haoni katika uchaguzi wake lakini Bisase kwa kuudhika anamkatiza usemi wake kabla hajaukamilisha. Katika *Kijiba Cha Moyo* mifano ya mdokezo ni kama ifuatavyo:
> **Aisha**:halafu……"(Ukurasa 2)

Hapa Aisha anamhimiza Sele kumsimulia zaidi kuhusu ziara yao ya kwenda kuuogelea baharini wakiwa nyumbani kwao.

**Sele**:Unaona ni mwili wa mtu unaenda huku umeelea………"(Ukurasa 3)

Amekatizwa usemi na Aisha kabla Sele hajamaliza kujielezea.

**Sele**: Mwenyewe nimeuomba lakini………. lak..(Ukurasa 9)

Katika utundikaji huu, Sele hakuwa na sababu nzuri ya kujitetea hivyo basi kuonekana kukosa muda wa kutosha wa kufikiria.

Kwingine katika *Mstahiki Meya* mbinu ya mdokezo inajitokeza hivi:

**Waridi**:Amesema mwenyewe Meya.."(Ukurasa 2)

Hapa Siki anamkatiza Waridi usemi kuonyesha kuwa hana uhakika sana na ahadi za uwongo za Meya.

**Siki**:Tatizo………la utapiamlo(Ukurasa 6)

Katika hali kama hii Siki anaonyesha hali ya kutoamini kuwa hali kama hii inaweza kuwakumba watu.Vile vile ni kutokana na utawala mbaya.

**Diwani III**: "Watu sasa wanataka vitendo,si maneno.Tusi…."(Ukurasa16)

Angeendelea zaidi ya haya pengine angemuudhi zaidi Diwani I ila akauacha usemi wake bila kukamilika.

### 4.2.8 Sitiari

Katika sitiari vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia au kimaumbile huhusishwa kwa njia moja. Kitu kimoja husemwa kuwa kingine mara nyingi kwa kutumia hivyo kwa maana ya kuleta msisitizo katika usemi. Hivyo ni kusema kuwa msingi wa sitiari ni uhamishi wa maana. Sitiari pia ni mojawapo ya tamathali za usemi ambayo huweza kutumiwa kujenga na kuimarisha ucheshi katika matini au kazi ya kifasihi.

Mathalani katika *Mstahiki Meya,* Siki anapozungumza na Bw.Kheri kuhusu ukakamavu wa watu mashuhuri wenye mamlaka makubwa katika Baraza la Mji anamwambia Bw.Kheri, "Lakini bwana, himizeni hiyo miamba kuangalia maslahi ya watu. Anazungumzia watu wakakamavu wenye mamlaka makubwa (Kama vile Meya na madiwani) Tunajua kuwa miamba ni mawe makubwa yaliyoenea mahali, lakini hawa viongozi vigogo wamelinganishwa na miamba. Hii ni sitiari"(Ukrasa 50). Mifano mingine ya sitiari ni kama ifuatayo:

"Unakanyaga nyoka mkia" (Ukurasa 15).

Sote tunaelewa kuwa nyoka ni kiumbe hatari ambaye akikuuma anayo sumu hatari inayoweza kuua. Siki analinganisha wananchi waliomchagua Meya kama nyoka ambao tayari wamekasirizwa na uongozi mbaya wa Meya.

Siku zote tumeshuhudia wasiotosheka wakipuliza tarumbeta zao za uzushi nazi tukizima kwa kukohoa tu" (Ukurasa16). Mbiu ya mgambo inapolia, kuna jambo. Wanaopuliza tarumbeta za uzushi kulingana na Diwani III ni wachochezi ambao wanawachochea wafanyikazi kushiriki migomo ya kumshinikiza Meya kuyasikiliza malalamishi yao. Kukohoa nako kunamaanisha matumizi ya milio ya bunduki kuwatawanyisha makundi ya wagomaji.

Lazima kwanza muhakikishe kuwa huyo sumu hapati hata fununu juu ya jambo hili. Hii ni bomu inayoweza kutulipukia usoni"(Ukurasa 62-63) Meya anafananishwa na sumu au bomu ambalo ni hatari. Yeye pamoja na madiwani wenzake wanahofia kuwa ikiwa Diwani III atapokea habari kuhusu njama wamepanga ya kujinufaisha wao wenyewe, ataisambaza na hivyo basi kuwachochea wafanyikazi wa baraza la Mji. Dunia kuna watu na viatu" (Ukurasa 64)

Kulingana na Dida anamaanisha kuwa kuna matabaka. Wanaojiweza na wenye vyeo ndio watu. Maskini ndio viatu.

## 4.3 Kinaya

Ni mbinu ambayo mtunzi huzua kichekesho kwa kutumia kejeli. Hufanya hivi aghalabu kuonyesha sura ya ujinga wa wahusika. Katika *Chamchela*, ni kinaya walinzi wanapomwita Mayaka "mzee" na Mayaka haelewi kabisa ni kwa nini anaitwa hivi. Hana habari kuwa anachekwa na wenzake kutokana na uhusiano wa kimapenzi kati yake na Bisase. Mayaka anaonyesha sura ya ujinga aliyonayo.Katika *Mstahiki Meya*, Meya Sosi anamwambia mhubiri kuwa ameguswa mara mbili na kushawishika ili aiache kazi ya umeya na amfuate. Pale ambapo askari I na II wanatoa amri ya kila mtu kulala chini.

Wanadhani Meya amefamiwa wakati wa maombi ya mhubiri pale ofisini. Wanalala chini. Askari wanaomba radhi wanapobaini kilichokuwa kinaendelea. Haya ni katika (Ukurasa 42-3).

Kicheko zaidi kinazuliwa katika usemi wa Diwani I. Anasema kuwa Mstahiki Meya ndiye aliye na uwezo wa kuchemua na kila mtu kubanwa na mafua. Anamgeukia Meya na kumwambia kuwa wote hawawezi kuchemua yeye apate mafua hata kidogo (Ukurasa59) Mbinu hii aidha imebainika pale ambapo Meya anafurahi kuwa askari I na II wanafika. Anawapokea akidhani wameitikia mwito. Anasema kuwa amefurahia kufika kwao kila mara anapowahitaji. Ukweli ni kwamba wamekuja kumkamata yeye na wenzake.

### 4.4 Hitimisho

Sura hii imechunguza tamathali za usemi na mchango wake katika kuendeleza muundo na kudhihirisha kukua kimawazo kwa Timothy Arege. Tumebainisha tamathali zilizotumiwa na Arege katika matini au kazi za kifasihi katika utunzi wake. Tumetathmini matumizi yake na kuangalia yipi zinavyoathiri ukuaji wa muundo na mawazo wa kazi husika. Kwa hivyo tumezihusisha tamathali hizo za usemi na miktadha yao ya kimatumizi na dhima yao kikamilivu katika *Chamchela*, *Kijiba Cha Moyo* na *Mstahiki Meya*.

## SURA YA TANO

## MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.1 Utangulizi

Tumefanya utafiti kuhusu tatizo la ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za Timothy Arege. Katika sura hii tutapitia kwa muhtasari mijadala tuliyoishughulikia katika utafiti wetu. Kwa kuhitimisha kazi yetu, tutataja tajriba kutokana na matumizi ya nadharia ya umuundo kama tulivyotekeleza kazi na kutoa mapendekezo katika tahakiki za baadaye. Jambo lingine tutakalopitia ni kuonyesha jinsi mtunzi Arege alivyopiga hatua katika kipindi cha uandishi wake. Aghalabu kazi za utafiti hukumbwa na matatizo kadha wa kadha. Tutayataja matatizo yaliyotusibu katika utafiti wetu na pia mafanikio yetu kwa jumla. Mwisho tutatoa mapendekezo kuhusu uhakiki wa muundo unaoweza kufanywa na wahakiki wa baadaye kuhusu uandishi wa Timothy Arege.

Tumeona katika utafiti wetu kuwa vipengele vya kazi ya fasihi yaani ploti, wahusika, maudhui na matumizi ya mbinu za lugha vinaingiliana na kushikamana. Katika hali kama hii haiwezekani kushughulikia kipengele kimoja bila kuvihusisha na vingine. Baada ya kuzitalii kazi zake Arege, jambo lililotubainikia kuhusiana na miundo ya kazi zake ni kuwa muundo wa kila tamthilia umeathiriwa na yaliyomo. Mtunzi Arege amejikita zaidi katika maudhui ya uwajibikaji katika kila tamthilia aliyoitunga. Jambo hili kwa kiasi fulani limeathiri hatua ya ukuaji wake.

Pili, mtunzi anaweza kuiandika tamthilia yake kitambo lakini kwa sababu fulani kazi yake ichelewe kuchapishwa. Kwa hivyo uchunguzi wetu umeegemea sana mwaka wa uchapishaji kama kigezo cha

kupimia ukuaji wa mwandishi. Mgala muue na haki umpe. Kwa upande mwingine mwandishi huyu amefaulu kusawiri hali halisi ya maisha kwa jumla. Arege ameonyesha hatua za kukua kutoka tamthilia moja hadi nyingine. Taswira zake za mandhari mbalimbali ni angavu na zinatilia nguvu zaidi kipengele cha uyakinifu.

Tamthilia alizotunga Arege kwa kipindi cha miaka miwili mtawalia ni ithibati nyingine ya kuendelea kukua kwa mwandishi. Anajaribu kuleta upya kwa kila kazi anayoitunga. Kurudiwa kwa baadhi ya maudhui ndiko kunakofanya kazi zake kufanana kwa kiasi fulani. Hata hivyo, vipengele vingine ni tofauti. Nadharia hii imetufaa katika uchanganuzi wa kazi za Arege. Kupitia kwayo, tumegundua kuwa kuna mwingiliano mkuu katika muundo na mawazo tunaporejelea suala la ukuaji.

## 5.2 Matatizo Wakati wa Utafiti

Katika kutumia nadharia ya umuundo kwenye utafiti wetu, tulikumbana na baadhi ya matatizo ambayo yalichangia kuathiri ubora wa matokeo ya kazi yetu. Tatizo la vitabu pamoja na maandishi mengine ya marejeleo ni tatizo tulilokumbana nalo. Wakati mwingine ilitubidi kutafuta marejeleo mengine kutoka kwa mtandao. Rejelea hizi zilikuwa za kiingereza na kwa hivyo ilitubidi kuzitafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Bila shaka haikuwa kazi rahisi. Kulikuwa na shida ya ufaafu wa matumizi ya nadharia ya umuundo katika kuhakiki baadhi ya vipengele vya muundo kwa kazi yetu.

Zaidi ya yote, suala letu la utafiti lilikuwa pana sana kiasi kwamba ilikuwa vigumu katika kukichunguza kila kipengele na jinsi kimeathiri katika mada yetu ya utafiti. Hili kwa njia moja au nyingine lilikuwa kikwazo cha kutoingilia kwa undani katika uchanganuzi wa vipengele hivi.

## 5.3 Mapendekezo Zaidi ya Utafiti

Utafiti huu umeshughulikia ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za Arege. Baadhi ya vipengele vya kimuundo tulivyovishughulikia ni pamoja na ploti, wahusika, maudhui na mbinu za matumizi ya lugha katika tamthilia tatu. Kwa sababu ya muda hatukuweza kuvishughulikia vipengele zaidi vya kimuundo. Tunapendekeza kuwa tahakiki za baadaye zinaweza kuchanganua haya kwa upana.

Aidha, baada ya kutalii kazi hizi, tumegundua kwamba kuna uhusiano mkubwa hasa katika maudhui. Tunapendekeza uchanganuzi wa kazi hizi kwa kuangazia namna kazi hizi zinahusiana, kuumana na hata kuchangiana. Hata hivyo, hatuwezi kudai kuwa utafiti wetu hauwezi kufanyiwa uchunguzi zaidi. Utafiti wetu uliegemea zaidi ukuaji kulingana na mwaka wa uchapishaji. Jambo hili linaweza kupingwa kwa kufanyiwa utafiti zaidi. Hebu tukomee hapa kwa kusema kuwa utafiti huu ni muhimu kwa kuwa umeweka msingi wa tafiti zitakazofuata baadaye katika taaluma ya fasihi kwa mtazamo wa nadharia hii.Ni matumaini yetu kuwa vizazi vya sasa na vijavyo vitanufaika kutokana na utafiti wetu

# MAREJELEO


Culler, J. (1975). *Sturacturalist Poetics*. London; Routledge&Kegan.

Kuhenga, C. (1975). *Tamathali za Usemi*. Dar-es-Salaam: East Africa Literature Bureau.

Mathew, M.L.B (1981). *Fasihi Simulizi na Andishi.* makala ya semina.

Mbatiah, M. (2000). *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi, Standard Textbooks, Graphics and Publishing.

Mbele, M. (1980). *View Points-Essays on Literature* and *Drama*.Nairobi, Kenya; Kenya Literature Bureau.

Mukarovsky, J. (1977). *The Word and Verbal Art*. Yale University Press.

Mulokozi, M. (1989). *Tanzu za Fasihi Similizi katika milika.* Dar- es-Salaam.

Murasi, M. (2011). *Mwongozo wa Mstahiki Meya.* Lurambi publishers, Nairobi.

Musyoka, M. (1996). *Uhakiki wa Fani katika Tamthilia za Jay Kitsao*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Hakijachapishwa)

Mwangi, D.K. (2005). *Uhakiki wa Fani katika Tamthilia Za K.W Wamitila*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Njogu na Chimerah (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: nadharia na mbinu*. Nairobi; Jomo Kenyatta Foundation Publishers,

Robey, D. (1973). *Sturacturalism: An introduction*. Oxford, Clarendon Press.

Timothy, M. A. (2007). *Chamchela.* Nairobi-Kenya; Jomo Kenyatta Foundation.

Timothy, M. A. (2011). *Mstahiki Meya*. Nairobi –Kenya; Vide-Muwa Publishers.

Timothy, M. A. (2009). *Kijiba Cha Moyo*. Dar -es - Salaam Tanzania;Longhorn Publishers

TUKI, (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar-es-Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa TUKI.